# Nipashe

Jumatano Aprili 24, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579900

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Madaktari Muhimbili wabaini ugonjwa unaomtesa Mariam

UKURASA 3




UKURASA 13

# Ripoti IMF yazua jambo bungeni

• **Prof.** Lipumba atoa ushauri kwa serikali...*Uk.2*





Mamia ya wakazi wa maeneo ya Moshono, Sekei na Moivaro, jijini Arusha, wakiangalia tukio la uokoaji wa watu watano waliofukiwa katika machimbo ya moramu, ambapo watu watatu walipoteza maisha na wengine wawili kujeruhiwa. **PICHA: ALLAN ISACK**

## Kibano kipya wakopaji elimu ya juu

UKURASA 4

## Mgodi waua watu watatu

UKURASA 2


MASUMIN PRINTWAYS & STATIONERS LTD

WYSEN FiveStar mondi business paper CASIO hp Canon nashuatec DELL EPSON APC Microsoft KYOCERA Datacard CITIZEN kangaro NATARAJ DYMO Pritt logitech ZEBRA Fellowes UNOMAT SanDisk uni-ball FALCON SAFE

Masumin Tower, Jamhuri / Mrima Street, P.O. Box 20073, Dar es Salaam, Tanzania
Mob: +255 (0) 626 333 000 / (0) 622 325 488 / (0) 713 325 488
Tel: +255 (22) 2117090, Email: info@masumin.co.tz

TOLL FREE: 0800-11-00-24

www.masumin.co.tz Masumin printways



Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba (wa pili kulia), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, akiitaka serikali iweke hadharani taarifa ya Shirika la Fedha Duniani (IMF), kuhusu hali ya uchumi wa Tanzania. Wengine ni Katibu Mkuu wa chama hicho, Khalifa Suleiman Khalifa (kulia) na Mbunge wa Mchinga, Hamidu Bobali (kushoto) na Mkurugenzi wa Ulinzi wa CUF, Masoud Mhina. **PICHA: JOHN BADI**

# Ripoti IMF yazua jambo bungeni

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

RIPOTI ya hali ya uchumi ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), imezua jambo bungeni baada Mbunge wa Tunduma, Frank Mwakajoka (Chadema), kudai serikali imelizuia shirika hilo kuchapisha ripoti ya hali ya uchumi wa Tanzania.

Mwakajoka aliibua suala hilo bungeni jijini Dodoma jana alipochangia mjadala wa hotuba ya makadirio ya bajeti ya fedha kwa mwaka 2019/2020 ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mwakajoka alisema: "Juzi tumepata taarifa kwenye mitandao na vyombo vya habari, IMF wamesema kwamba wanatakiwa waruhusiwe tu na Tanzania watoe habari ya jinsi gani uchumi wa nchi yetu unakwenda.

"Mpaka sasa hivi kimya, tunaomba pia waziri aseme, ni kwa sababu ya kutokuwa na uhuru wa vyombo vya habari. Vyombo vya habari vinasema wanaogopa kuandika kwa sababu wanasoma kwenye mitandao."

Kutokana na kauli hiyo, Spika wa Bunge, Job Ndugai, aliingilia kati na kumuuliza mbunge huyo (Mwakajoka) kama kweli shirika hilo limeiomba Tanzania litoe taarifa hiyo.

"Una uhakika IMF imeomba itoe habari?" Spika Ndugai alimuuza Mwakajoka.

Mbunge huyo alijibu: "Ndiyo, wameomba serikali ya Tanzania iruhusu ili wachapishe hali ya uchumi wa nchi yetu kwa jinsi ambavyo wameangalia, wamezuiliwa wasiitoe, sasa kama wamezuliwa na walipakodi wanataka kujua."

Baada ya majibu hayo, Spika Ndugai alihoji tena akiuliza: "Hivi Tanzania inaweza kuzuia IMF wasichapishe taarifa yao?"

Mwakajoka akajibu: "Ni lazima nchi ihusike na Tanzania haijaruhusu ili wachapishe ile na ni taarifa."

Kutokana na majibu hayo ya Mwakajoka, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alisimama na kuomba utaratibu akidai Kanuni ya 64(I)A ya Kanuni za Kudumu za Bunge imekiukwa.

Kanuni hiyo inasema mbunge hatatoa ndani ya Bunge, taarifa ambazo hazina ukweli.

Mhagama ambaye pia ni Mnadhimu Mkuu wa Shughuli za Serikali bungeni, alisema: "Mheshimiwa Spika, ndani ya serikali, tunavyojua sisi bado tunaendelea kufanya mazungumzo na IMF kuhusu ripoti hiyo na si kweli Tanzania imezuia ripoti hiyo isitolewe.

"Sasa ninaomba Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mimi ninafahamu na Waziri wa Fedha yupo hapa anafahamu na ana maelezo tu ya kutosha kuhusu jambo hilo ambalo linapotoshwa na Mheshimiwa Mwakajoka.

"Mheshimiwa Spika, ama naomba afute hizo 'statements' (kauli) zake za kuituhumu serikali kwamba imeficha hiyo ripoti na haitaki ripoti hiyo itolewe ama alithibitishie Bunge kwamba taarifa anazozisema ni sahihi na ripoti aliyonayo ni sahihi na hakuna jambo lolote ambalo linaendelea kwa sasa ndani ya serikali."

Kutokana na maelezo hayo ya Mhagama, Spika Ndugai alisema kilichoelezwa na Mwakajoka ni kwamba Tanzania imewazuia IMF wasitoe taarifa, kisha akam

INAENDELEA UK. 8

# Kifusi chaua watatu mgodini

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WATU watatu wamefariki dunia na wawili wamejeruhiwa na kulazwa Hospitali ya Mkoa Mount Meru, baada ya kufukiwa na kifusi kwenye machimbo ya Moram inayotumika kwa ajili ya shughuli za ujenzi, yaliyopo eneo la Moivaro Kata ya Moshono.

Tukio hilo limetokea umbari wa Kilometa nane kutoka katikati ya Jiji la Arusha, baada ya mabonge makubwa ya Moram kuporomoka, wakati watu hao wakiwa kwenye shughuli ya uchimbaji.

Akizungumzia tukio hilo Kamanda wa polisi Mkoa wa Arusha, Jonathan Shana, alisema tukio hilo lililotokea jana asubuhi.

Alisema tangu kutokea ajali hiyo vikosi vya uokoaji, kutoka mamlaka za ulinzi na usalama vilikusanyika eneo la tukio na kuendelea na shughuli ya kufukua udongo, kuwatafuta watu waliofukiwa. "Lakini pia vifaa mbalimbali vya uokoaji viliwasili mara moja ili kufanikisha zoezi la ufukuaji kifusi linaenda kwa haraka na vizuri," alisema.

Shana alisema watu watatu waliofariki walikuwa wamefunikwa na gema lililobomoka kutoka na mvua zilizonyesha usiku wa kuamkia siku hiyo na wawili walijeruhiwa na kukimbizwa hospitalini.

Alilishukuru Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), askari Mgambo, viongozi mbalimbali, na kuwa Jeshi lake lipo eneo hilo kufanya zoezi hilo kuwa rahisi.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Gabrie Daqarro, alisema hiyo ni mara ya pili kwa machimbo hayo kuporomoka na kusababisha maafa, ambapo mwaka 2013 hali kama hiyo ilijitokeza na kuua watu 13 na wengine kadhaa kujeruhiwa.

# ... Prof. Lipumba ashauri taarifa ichapishwe

**Na Mary Geofrey**

MWENYEKITI wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, amemshauri Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, aruhusu Shirika la Kimataifa la Fedha (IMF), lichapishe Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Tanzania ya mwaka 2019 ili wabunge wapate fursa ya kuisoma na kuichambua.

Prof. Lipumba amesema anaamini kuwekwa hadharani kwa ripoti hiyo kutatoa nafasi kwa wataalamu kushughulikia kasoro na upungufu uliobainika kwenye ripoti hiyo kwa ustawi wa taifa.

Mtaalamu huyo wa uchumi aliyasema hayo alipozungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, akidai kuwa ripoti ya IMF inatabiri kuporomoka kwa ukuaji wa uchumi wa Tanzania kutoka asilimia 6.6 mwaka 2018 hadi kufika asilimia nne mwaka huu.

"Kwa nia safi na uzalendo, namshauri Waziri wa Fedha na Mipango na serikali kwa ujumla iruhusu IMF ichapishe taarifa hiyo kwenye tovuti yake. Wabunge wapate fursa ya kuisoma na kuichambua. Ikiwa kuna ushauri mzuri waisisitize serikali itekeleze na kama haufai ielezwe kwa nini haufai," Prof. Lipumba alisema.

Aliongeza kuwa kwa mujibu utabiri wa IMF kuhusu ukuaji wa uchumi wa Tanzania uliofanyika Oktoba mwaka 2018, pato la taifa litakua kwa wastani wa asilimia 6.5 kati ya mwaka 2019 na mwaka 2023.

"Utabiri wa sasa unaonyesha kuporomoka kwa ukuaji wa uchumi na kufikia wastani wa asilimia 4.5 katika kipindi hicho. Huenda taarifa ya hali ya uchumi ya IMF ina ufafanuzi wa sera zinazosababisha mtazamo wake wa kuporomoka kwa ukuaji wa uchumi," Prof. Lipumba alisema.

Alidai kifungu cha nne cha mkataba wa IMF kinaipa mamlaka shirika hilo kufanya uchunguzi na utafiti wa sera za uchumi, fedha na thamani ya sarafu za nchi zote wanachama ili kuhakikisha kuwapo kwa ufanisi katika mfumo wa fedha wa dunia.

"Tathimini hii hufanywa kwa nchi zote 189 ambazo ni wanachama wa IMF, tangu mwanzoni mwa miaka ya 2000, karibu nchi zote hukubali taarifa zao kuchapishwa kwenye tovuti ya IMF," Prof. Lipumba alidai.

Alidai kitendo cha taarifa hiyo kutochapishwa kwenye tovuti ya

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA

# Madaktari Muhimbili wabaini ugonjwa unaomtesa Mariam

**Na Romana Mallya**

TIMU ya madaktari wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), imekutana jana kujadili majibu ya ugonjwa unaomsumbua, Mariam Rajab (25), mkazi wa Kitongoji cha Inung'una mkoani Singida mwenye kidonda sugu mgongoni.

Mariam alipokelewa hospitalini zaidi ya wiki moja iliyopita baada ya kuonekana mtandaoni akiomba msaada wa kufikishwa hospitali ya Muhimbili kwa matibabu kutokana na familia yake kuwa maskini.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano kwa Umma na Huduma kwa wateja wa hospitalini hapo, Aminiel Aligaesha, aliliambia Nipashe kuwa timu hiyo ilikutana jana, na majibu ya ugonjwa unaomsumbua Mariam yameshatoka.

"Mariam baada ya kufika hospitalini hapa kama tulivyowaeleza awali, madaktari walichukua vipimo na tayari majibu yameshatoka. Leo (jana) timu ya madaktari itakaa kuyajadili na kesho (leo) tutatoa taarifa kwa vyombo vya habari," alisema.

Daktari Bingwa Mkuu wa Idara ya Upasuaji Hospitali ya Muhimbili, Dk. Ibrahim Mkoma, ambaye ndiye anayemtibia Mariam alipoulizwa hali ya msichana huyo alisema anaendelea vizuri na taarifa kamili ya nini kinachomsumbua itatolewa kesho (leo).

Mwishoni mwa wiki iliyopita, Mariam ambaye amelazwa wodi namba 15 jengo la Kibasila, alisimulia namna ambavyo ameteseka na kidonda hicho ambacho chanzo chake ni moto.

Msichana huyo alisimulia kuwa miaka mitano iliyopita baada ya kuungua na moto eneo hilo la mgongo, alitibiwa hospitali ya Mkoa wa Singida hadi kidonda kilipoonekana kimepona.

Alisema baada ya kupona kovu la moto eneo hilo la mgongo lilitokea jibu ambalo baadaye lilipasuka.

"Lilipopasuka nikawa nakwenda hospitalini kusafishwa lakini kadri siku zilivyoendelea kidonda kiliongezeka na gharama za kusafishwa kila siku ilikuwa ni Sh. 5,000, kama nilivyoeleza familia yetu ni masikini hivyo haikuweza kuzimudu," alisema.

Mariam alisema aliendelea na huduma ya kusafishwa kila siku hospitali na kuanzia Agosti mwaka jana ilibidi awe anapewa huduma hiyo nyumbani na ndugu zake kutokana na hali ya kimaisha waliyonayo.

"Kadri kilivyokuwa kinasafishwa nyumbani kidonda kikawa kinaendelea kukua na mwisho wa siku kikafikia ukubwa huu, wakati nasafishwa nyumbani kuna mtu alimshauri awe anapaka unga wa dawa ya flagyl mara baada ya kukisafisha, hivyo nikawa nafanya hivyo," alisema.

Mariam alisema licha ya kuweka unga wa dawa hiyo kwenye kidonda, lakini haikusaidia zaidi kiliendelea kuongezeka ukubwa.

Alisema kutokana na hali ya kimaisha ya kwao ilifikia hatua marafiki zake aliosoma nao, wal

INAENDELEA UK 7



Mkurugenzi wa kampuni ya Zenon Oil Gas Ltd, Frolencia Membe, akiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kesi inayomkabili ya uhujumu uchumi na utakatishaji fedha kuahirishwa. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Serikali yatoa neno kila mtu kumiliki laini moja ya simu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa hakuna sehemu ambayo serikali ilitamka kuwa kila Mtanzania anatakiwa kuwa na laini moja ya simu.

Aidha, kampuni za simu zimeagizwa kusajili kwa kutumia alama za vidole na zoezi litaanza Mei Mosi, mwaka huu.

Hayo yalibainishwa bungeni jana na Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Atashasta Nditiye, wakati akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Rombo (Chadema), Joseph Selasini.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema Waziri huyo amenukuliwa kwenye vyombo vya habari Mei mosi, mwaka huu kutakuwa na usajili mpya wa kutumia alama za vidole na kwamba hakutakuwa na ruhusa ya kumiliki laini mbili hadi ruhusa maalum ya maandishi.

"Kuna maeneo mengine laini hazipatikani, kuna mengine Vodacom ipo, Airtel haipo sasa hamuoni kama mtawasumbua wananchi?" alihoji.

Akijibu, Nditiye alisema kilichozungumzwa ni kwamba anatamani kila Mtanzania awe na laini moja ya simu kwa mtandao

INAENDELEA UK. 7

# Mapya ya daktari anayetuhumiwa kukataa kurejea kazini Ijumaa Kuu

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Kituo cha Afya cha Ngarenalo, Dk. Japhet Kivuyo, ambaye sauti yake inadaiwa kusikika kwenye video fupi iliyosambaa mtandaoni akikataa kwenda kituoni kutoa huduma Ijumaa Kuu, ameshushwa cheo na Mkurugenzi wa Jiji la Arusha, Dk. Maulid Maden.

Kupitia video fupi iliyosambaa mtandaoni ilisikika sauti inayodaiwa ya daktari huyo, akikataa kurudi kituoni baada ya kiongozi mmoja wa Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Levolosi, Arusha iliyofika kituoni huko siku hiyo, kumpigia simu na kuweka sauti ya juu.

Dk. Maden alisema jiji limechukua hatua dhidi ya daktari huyo kwa nafasi yake ya Mkuu wa Kituo cha Ngarenalo kuchukuliwa na daktari mwingine.

"Ofisi yangu inatoa taarifa kwa umma kuwa kuanzia leo (jana) imamvua uongozi Dk. Kivuyo na kumfanya kuwa daktari wa kawaida na nafasi yake itachukuliwa na daktari aitwaye David Mng'anya. Jiji la Arusha linaomba radhi kwa wananchi walioguswa na kadhia hii," alisema.

Dk. Maden pia alisema kutokana na tukio hilo, ofisi ya jiji itafanya uchunguzi na kuchukua hatua zaidi dhidi ya daktari huyo.

Alidai katika video hiyo, sauti inayodaiwa ya Dk. Kivuyo inasikika akikataa kurejea kituoni kutoa huduma kwa sababu siku hiyo ilikuwa ni sikukuu.

"Video hiyo ilikuwa ni ya mazungumzo ya simu kati ya Mkuu wa Kituo cha Ngarenalo na kamati ya siasa ya Kata ya Levolosi. Katika mazungumzo hayo mkuu wa kituo hiki akieleza kuhusu ratiba ya kutoa huduma kituoni hapo," alidai.

Dk. Maden alisema taratibu za utoaji huduma katika vituo vyote vya afya ni kwa saa 24 kila siku na kwa siku za mapumziko tabibu au daktari lazima awapo kituoni.

"Wananchi wafahamu kuwa huduma za afya zinapatikana kila siku na siyo vinginevyo, nasisitiza kuwa viongozi mbalimbali na wananchi wawasilishe taarifa katika mamlaka stahiki wanapokutana na changamoto au kero zozote ili taratibu stahili za ufumbuzi zifuatwe," alisema.

Dk. Maden alidai kamati ilikwenda kituoni huko siku ya mapumziko na ilibaini Dk. Kivuyo alikuwapo kituoni kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa tisa alasiri na baadaye aliondoka.

INAENDELEA UK. 8


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
Tarehe 17/04/2019.

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya ALHAMIS tarehe **25/04/2019** kampuni ya **S.S.F Co.LTD** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka DAR kuelekea **KAGERA** gari hilo lenye namba za usajili:

   **T785 CAD /T 166 ADN .**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

   Urefu - mita 21.80
   Upana - mita 3.20
   Kimo - mita 5.20

3. NJia itakayotumika **DAR** hadi **KAGERA** kupitia **MWENDAKULIMA** gari litasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

215191102

## HABARI KITAIFA

# Jaji Mkuu ataja sababu zinazochelewesha haki

**Na Elizabeth Zaya**

JAJI Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, ametaja baadhi ya sababu zinazochangia kutotolewa haki kwa wakati mahakamani kuwa ni tabia za uvivu, uchonganishi, ulalamishi, kuchelewa na ubishi usioeleweka.

Alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua mkutano wa mwaka wa kutathmini utendaji wa Mahakama ya Rufani.

Prof. Juma alisema majaji wana wajibu mkubwa wa kutoa haki kwa mujibu wa sheria na kutoa uamuzi hata katika mambo yasiyo na sheria.

Aliwataka majaji pamoja na kuzingatia sheria na katiba katika kutoa haki, kutosahau masuala ya kiutamaduni ya mahakama na tabia ambazo hazijaandikwa ili kusaidia utoaji wa haki.

Alisema pamoja na kutakiwa kutegemea sheria na katiba, pia yapo mambo ya kiutamaduni na tabia ambazo hazijaandikwa sehemu yoyote hivyo wanapaswa kuyazingatia katika kutoa haki.

"Mnatakiwa kuwa na uelewa wa sheria kwa sababu wananchi wanategemea watapata haki kutoka kwenu tena kwa wakati," alisisitiza Jaji Mkuu.

Aliongeza kuwa upo mkakati wa miaka mitano wa mahakama unajenga tabia ya kutoa haki kwa kutumia utamaduni.

"Hakuna mahali ambapo pameandikwa kuwapo kwa uharakishaji wa utoaji haki, lakini majaji wanapaswa kutambua suala la kutoa haki hiyo kwa wananchi ni muhimu sana, kwa sababu wananchi wanahitaji kupata haki kwa wakati, lakini pia mnatakiwa kufanya kazi kuendana na karne ya 21," alisema. Alisisitiza yapo mambo mengi ya kuwezesha utoaji haki kwa wakati na kwamba katika utafiti alioufanya amegundua kuwa utamaduni unaweza kuwa sehemu ya kusaidia utoaji wa haki.

Jaji Juma alisema idadi ya majaji imeongezeka kutoka 15 hadi 21 na kufanya kuongeza nguvu kwa mahakama na kwamba lengo ni kuondoa mashauri yaliyokuwa yakichelewa.

"Katika masuala ya utoaji haki majaji hawapaswi kuangalia mtu yoyote kutoka nje ya mahakama, na ndiyo maana katika mkutano huu, majaji watapata mafunzo ya namna ya kuendesha majopo mahakamani kuwezesha utoaji wa haki kwa wakati,"alisema Jaji Juma.

## Wasakwa na Polisi tuhuma kuua baba

**Na Stevie Chindiye,**
TUNDURU

WATOTO wa familia moja katika Kijiji cha Airport Kata ya Mbesa katika Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma, wanatafutwa na polisi kwa tuhuma za kuua baba yao mkubwa kwa kipigo katika tukio linalo daiwa kuwa chanzo chake ni ugomvi wa mashamba.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Saimon Marwa, alisema katika tukio hilo watuhumiwa hao walimshambulia na kumpiga marehemu Omari Mohamed Omari (60) kwa kitu kizito kichwani.

Kamanda Marwa aliwataja majina watuhumiwa hao kuwa ni Rashid Bakari Mohamed na Yahaya Bakari Mohamed.

Mganga aliyeufanyia uchunguzi mwili wa marehemu, Dkt. Vitaris Lusasi alisema kuwa chanzo cha kifo hicho ni kupasuka kwa fuvu la kichwa kutokana na kipigo hicho.

alisema kwamba Polisi wanaendelea na uchunguzi ili kubaini chanzo cha tukio hilo.



Mchuuzi wa vikapu akisaka wateja katika Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, eneo la jirani na Ubalozi wa Ufaransa, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**




# RITA yabana waomba mikopo elimu ya juu

**Na Salome Kitomari**

WAKALA wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), umeanza usajili wa vyeti vya kuzaliwa na vifo wa wanafunzi wanaotaka kujiunga na elimu ya juu kwa kupata mikopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Kaimu Kabidhi Wasii Mkuu na Afisa Mtendaji Mkuu wa Rita, Emmy Hudson, alisema wanafunzi watatakiwa kujaza fomu maalum kwenye mtandao na kuambatanisha vyeti vyao ili kuhakikiwa kama walivyonavyo ni sahihi.

Alisema baada ya uhakiki majina ya wahusika yatapelekwa Bodi ya Mikopo kwa ajili ya mchakato wa kupatiwa mikopo kwa mujibu wa sifa, na kwamba ambao watashindwa kufanya hivyo watakuwa wamepunguza sifa za kuhudumiwa.

"Mwaka jana tulifanya uhakiki na kati ya vyeti 108,000 vyeti 2,000 vilibainika kuwa na kasoro mbalimbali, ikiwamo vya kughushi, wahusika walijulishwa na baadhi kufikishwa polisi," alisema.

Alisema kwa mwaka huu wametangaza kuanza kwa usajili mapema ili kuwawezesha wanafunzi wanaotarajia kuomba ufadhili wa masomo kukamilisha utaratibu huo mapema badala ya kusubiri muda wa mwisho.

Hudson alisema vyeti vinavyohakikiwa ni vya kuzaliwa na vya wazazi kama walifariki na kwamba uhakiki huo unaanza sasa na utakuwa endelevu kwa kuwa ni lazima kila cheti kihakikiwe.

"Kila mtu ataweza kufungua mtandao wetu na kuingiza taarifa zake muhimu na itafika mahali atatakiwa kuingiza nakala ya cheti, baadaye atajulishwa juu ya uhalali wa taarifa zake, taarifa tutakazozipata tutazipeleka Bodi ya Mikopo na kuanzia hapo mtu atakuwa huru kuendelea na maombi yake," alibainisha.

Kwa mujibu wa mtendaji huyo, ada ya uhakiki ni Sh. 3000 ambayo italipwa moja kwa moja kupitia benki na kwa simu, na kwamba malipo yatakamilika baada ya muombaji kupokea stakabadhi kwa njia ya ujumbe wa simu.

Naye, Kaimu Mkurugenzi wa Tehama, Cliff Maregeri, alisema Rita imeboresha mfumo tofauti na mwaka jana, na kwamba mifumo hiyo imeunganishwa na huduma mbalimbali ikiwamo Uhamiaji, Bodi ya Mikopo na taasisi nyingine za serikali ili kuwa na taarifa kamilifu.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uchunguzi simu, dawa za kulevya gerezani hatua nzuri

**KATIKA** toleo la jana tulichapisha kuwa baada ya kubaini uwapo wa changamoto ya baadhi ya wafungwa kutumia simu na dawa za kulevya wakiwa gerezani, serikali imeunda timu ya kuchunguza uingizwaji wa vitu hivyo gerezani.

Uamuzi huo umechukuliwa na serikali baada ya kupokea malalamiko ambayo yamekuwapo kwa muda mrefu kuhusiana na suala hilo. Machi 22, mwaka huu, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, akiwa ziarani mkoani Mbeya, aliagiza kuundwe timu ya kuchunguza kadhia hiyo na maofisa wanne waliodaiwa kuhusika, wasimamishwe kazi.

Akizungumza na Nipashe juzi, Masauni alisema timu ya kuchunguza suala hilo katika Gereza la Ruanda mkoani Mbeya imeshaundwa na inaendelea na kazi.

Masauni alisema anaamini ripoti ya timu hiyo itatoa ufumbuzi wa kudumu wa changamoto hiyo.

Alieleza kuwa maagizo yake aliyotoa siku hiyo yametekelezwa na mengine yanaendelea kutekelezwa, na kuwa aliagiza baadhi ya maofisa waliohusika wasimamishwe kazi, utekelezaji wake umeshafanyika.

Kwa mujibu wa Masauni, wapo maofisa kadhaa wamesimamishwa kazi na kufafanua zaidi kwamba aliagiza kuundwe tume ya uchunguzi, ambayo imeshaundwa na inaendelea na utekelezaji.

Aliongeza kuwa timu imechukua muda kwa sababu wanataka kupata ufumbuzi wa kudumu wa masuala ya uingizaji simu magerezani na matumizi ya dawa za kulevya ambayo ni kinyume cha sheria.

Hatua ya kuundwa kwa timu hiyo ni ya msingi na tunapongeza jitihada za serikali za kulifuatilia kwa karibu suala hilo, kwa lengo la kuhakikisha kuwa magereza ni sehemu ya kuwafanya wahalifu kubadilika na kuwa raia wema pale watakaporejea katika jamii.

Kama magereza yanashindwa kutekeleza majukumu yao ya kuwabadilisha tabia wafungwa wakawa na tabia njema, badala yake kuwaacha wakaendelea kufanya uhalifu ikiwamo matumizi ya dawa za kulevya, yanafanya kinyume, na hivyo wahalifu kuendelea kuona magereza ni sehemu nzuri ya kuishi.

Matumizi ya simu kwenye magereza pia ni jambo lisilokubalika. Ikumbukwe kwamba mtu anapohukumiwa kifungo maana yake ni kumtenga na jamii, hivyo kumruhusu matumizi ya simu magerezani ni kumaanisha kuwa wenye mamlaka ya kusimamia magereza wanakwepa kutekeleza majukumu yao pamoja na kuvunja sheria za nchi.

Mbali na kuundwa kwa timu hiyo, tumetiwa moyo na hatua zilizochukuliwa na mamlaka husika za kuwasimamisha kazi maofisa kadhaa wa magereza kutokana na matukio hayo pamoja na simu tisa na dawa za kulevya aina ya bangi, alizikamata Naibu Waziri Masauni siku ya ziara yake.

Ushauri wetu ni kuwa viongozi wa serikali wawe wanafanya ziara mara kwa mara katika magereza kwa ajili ya kutafutia ufumbuzi wa changamoto mbalimbali pamoja na malalamiko yanayotolewa na jamii.

Tunasema hivyo kwa sababu matatizo mengi yamekuwa yakielezwa kutendeka katika magereza yetu kwa muda mrefu bila kutatuliwa.

Tunaamini kuwa bado kuna changamoto zingine kwenye magereza mengine, hivyo ni wakati mwafaka kwa mamlaka husika kuweka utaratibu endelevu wa kuyetembelea magereza na kupata taarifa sahihi kuhusiana na yanayoendelea. Kwa kufanya hivyo, ni dhahiri kuwa matatizo mengi kwenye magereza yatapatiwa ufumbuzi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mhariri Wikiendi:** Epson Luhwago
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Idara ya Matangazo:** 0745 700710
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Salome Kitomari

# Maboresho Daftari la Wapigakura yaende na Elimu ya Mpigakura

**TUME** ya Taifa ya Uchaguzi (Nec), imeanza maboresho ya daftari la wapigakura kwa ajili ya uchaguzi wa Novemba mwaka huu na Oktoba mwakani.

Lengo la maboresho hayo ni kuondoa waliofariki na kuongeza waliofikisha umri wa kupigakura ambao kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania ni waliofikisha au watafikisha miaka 18 ifikapo Oktoba mwakani.

Aidha, waliohama mtaa, kijiji, kata, jimbo au mkoa, ikiwa ni pamoja na waliopoteza vitambulisho. Ili wote hao wawe na sifa ya kuchagua ni lazima kuwa na kitambulisho cha sasa cha wapigakura.

Maboresho yatawezesha Tanzania kujua idadi ya wapigakura watakaokuwa na sifa katika dhima nzima ya kuboresha daftari ambalo lilianza kwa njia ya kielektroniki mwaka 2015.

Baada ya uandikishwaji wa awali, lilitolewa daftari la kwanza ambapo wahusika walitakiwa kuhakiki taarifa zao.

Yalibainika mambo mbalimbali yanayohitaji mabadiliko, likiwamo la muingiliano wa taarifa.

Kasoro zilizobainika wakati huo zilikuwa ni pamoja na picha kuchanganywa, yaani picha A kupewa B, kukosekana picha sahihi kwa maana ya picha za maeneo na vitu kujitokeza kwenye daftari, huku yakikosekana majina sahihi.

Maandalizi ya uandikishaji wa wapigakura kwa mfumo wa BVR ulifanyika mikoa mbalimbali kwa mujibu wa ratiba iliyokuwa imetengwa, ambapo watu wote waliandikishwa na kupatiwa vitambulisho.

Hayo yalifanyika wakati uchaguzi wa serikali za mitaa ukiwa umeshapita, hivyo kilichokuwa kinafanyika ni maandalizi ya uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

Kwa mwaka huu ni tofauti kwa kuwa daftari hilo litatumika kuanzia uchaguzi wa serikali za mitaa Novemba mwaka huu.

Hivi karibuni Nec ilitangaza kuanza kwa maboresho katika kata tatu za mfano, na baadaye watasambaza maboresho hayo maeneo mbalimbali nchini.

Lengo ni kuhakikisha maboresho yamefanyika hatimaye kuchapisha daftari litakalotumika kwenye uchaguzi wa mwaka huu na mwakani.

Muungwana anapendekeza kutolewa kwa elimu ya uraia na mpigakura kwa wananchi ili wajitokeze kwa wingi kuboresha taarifa zao.

Elimu hiyo itajenga umakini na kuepusha makosa yaliyojitokeza kipindi cha nyuma, lakini pia kuwapo taarifa sahihi za wapigakura.

Elimu inahitajika kutokana na ukweli kuwa wapo baadhi ya wananchi ambao wataona kwamba kwa kuwa tayari wana vitambulisho vya kupigia kura, basi hawana haja ya kuhuisha taarifa zao hata kama wamehama maeneo ya awali, hali inayoweza kuwanyima fursa ya kuchagua mwenyekiti wa mtaa au kijiji.

Na kwa hali hiyo, hawataweza kuchagua diwani na mbunge kutokana na kutojiandikisha kwenye eneo walilopo sasa.

Wapo wananchi wamehama mkoa, wilaya, kata, mtaa na kijiji, na hawajui kwamba kuna umuhimu wa kupeleka taarifa zao ili kuwa na uhalali wa kuwapigia kura viongozi wote wa kuchaguliwa.

Katika kitambulisho cha kupigia kura kuna taarifa za jina kamili, tarehe ya kuzaliwa, jinsia, kata, mtaa au kijiji na kituo cha kujiandikishia.

Vyote hivyo ndivyo vinavyompa mpigakura uhalali wa kupigakura kwenye eneo husika kwani katika kila kituo kunakuwa na daftari lililogawanywa kutoka kwenye daftari kubwa ili kupata dogo ambalo litatumiwa na wananchi wa eneo husika kupunguza ukubwa wa kazi.

Katika daftari hilo, kila mpigakura hupewa namba yake ambayo haifanani na ya mtu mwingine na kitambulisho kimoja kinachotumiwa na mtu mmoja kwa ajili ya kukamilisha shughuli ya upigajikura.

Yote haya yanatakiwa kufahamika kwa wananchi ili kuepuka kuwa na baadhi ya wapigakura wakaotafika kwenye uchaguzi wa Novemba wakiwa na vitambulisho vya zamani, jambo litalowanyima haki yao ya kupigakura.

Muungwana ana imani kuwa yote yatawezekana iwapo asasi zisizo za kiserikali na serikali yenyewe watashirikiana kutoa elimu ya uraia, vipeperushi na mabango yatakayobandikwa sehemu muhimu kufikisha elimu.

Aidha, ni vyema ratiba ya uandikishaji wapigakura ikajulikana mapema ili kuwawezesha wananchi kupanga ratiba zao vyema.

HABARI KITAIFA

## Madaktari Muhimbili wabaini ugonjwa unaomtesa Mariam

INATOKA UK. 3

imchangia kiasi kidogo cha fedha ambacho kilimuwezesha kununua baadhi ya vitu vilivyokuwa vinahitajika kwa ajili ya kukiosha kidonda hicho.

"Matumizi ya flagyl hayakuwa ushauri wa daktari, kuna mtu alituambia kuwa tukifanya hivyo kidonda kitapona, hali ilivyoendelea kuwa mbaya rafiki yangu ambaye nimesoma naye elimu ya sekondari alikuja kunitembea nyumbani na alinishauri nirekodi video fupi ya kuomba msaada mtandaoni, ndipo nikafanya hivyo," alisema.

Alisema kitendo hicho ndicho kilichomwezesha kufika hospitali ya Muhimbili kwa msaada wa serikali na anapatiwa matibabu ya bure.

Akizungumza siku hiyo, Dk. Mkoma alisema kwa kawaida kidonda chochote kinachotokea kwenye kovu siyo cha kuchukuliwa kwa wepesi bali mhusika apelekwe hospitali.

Pia alisema mtu huyo akifikishwa hospitalini wataalam wanatakiwa wasiishie kukisafisha kidonda bali wachunguze kama ni cha kawaida au saratani.

"Mara nyingi vidonda vinapotokezea kwenye kovu ni saratani na mara nyingi huwa kinaanza kama kiuvimbe alafu baadaye huwa na tabia kinapasuka na unatumia dawa hazisaidii, kadri unavyokisafisha ukikifungua unakuta kimeongezeka. Hivyo hali hiyo ikizidi miezi mitatu ujue hicho siyo kidonda cha kawaida," alisema.

Mariamu alifikishwa hospitali ya Muhimbili baada ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu kuiona video hiyo fupi mtandaoni na kuuagiza uongozi wa Muhimbili kumfuatilia ili apelekwe hapo.

## Serikali yatoa neno kila mtu kumiliki laini moja ya simu

INATOKA UK. 3

mmoja na akihitaji laini nyingine aseme. "Tunaepuka utitiri wa laini nyingi nyie ni mashahidi mnaombwa hela kila siku tuma kwa namba hii mara hii hayo ni malaini yasiyo na tija kwa Watanzania," alisema.

Alibainisha kilichozungumzwa ni kuwa na laini moja kwa mtandao mmoja.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Anna Gidarya, alihoji serikali itapeleka lini huduma ya mawasiliano kwenye baadhi ya vijiji vya jimbo la Babati ambavyo kwa muda mrefu havina huduma hiyo.

Akijibu, Nditiye alisema serikali inaendelea kuratibu utekelezaji wa jitihada muhimu za kuwezesha maeneo yote nchini kufikiwa na huduma za mawasiliano sawasawa na maelekezo ya sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016.

"Kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote serikali itaviainisha vijiji vya Yorotonik, Endagwe, Hoshan na Endakiso kwa kuangalia ukubwa wa eneo, idadi ya wakazi wake pamoja na kufanya tathmini ya mahitaji halisi ya ruzuku kwa ajili ya kufikisha huduma hiyo.

# Majaliwa aagiza ofisi za serikali

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amekagua ofisi mpya za wizara saba katika mji wa Serikali ulioko Mtumba, Dodoma na kusisitiza waweke vibao vya ofisi na kukamilisha mazingira ya nje.

"Kuna wizara hazina majina kwa nje. Hakikisheni majengo yote yanawekwa majina haraka ili kuondoa usumbufu kwa wananchi wanaokuja huku kutafuta huduma. Kama kuna wizara mbili ziko jirani, pale njia panda wekeni kibao kuonesha majina ya wizara zote mbili. Nia ya Serikali ni kutoa huduma zote kutokea hapa Mtumba," alisema.

Alitoa agizo hilo jana wakati akitoa majumuisho ya ziara hiyo fupi kwa maafisa wa Serikali waliokuwepo kwenye ukumbi wa mikutano wa Wizara ya Nishati ambako ndiko alimalizia ziara yake.

Waziri Mkuu alitembelea wizara saba ambazo ni Maliasili na Utalii; Ofisi ya Rais - TAMISEMI; OWM - Sera, Uratibu na Bunge; Ofisi ya Rais - Utumishi na Utawala Bora; Mifugo na Uvuvi, Ulinzi na JKT na ya mwisho ilikuwani ni Wizara ya Nishati.

"Nimefurahi kukuta Mawaziri, Naibu wao na Makatibu Wakuu pamoja na wakuu wa idara wako huku na kazi zinaendelea, lakini ni lazima nisisitize kwamba idara zinazohamia huku ziwe ni zile zenye kutoa huduma za kila siku kwa wananchi," alisema.

"Ni lazima tuwaeleze wananchi na wadau wetu ili watambue kwamba Serikali imehamia huku, lakini wakija kutaka huduma wasikute idara inayowahusu iko mjini au wengine wako huku na wengine wako kule."

Kuhusu miundombinu ya barabara, umeme na TEHAMA, Waziri Mkuu alisema Kamati ya Kitaifa ya kuratibu zoezi la Serikali kuhamia Dodoma inasimamia kazi hiyo ikiwemo suala la ujenzi wa kituo kikubwa cha afya ambacho kitakuwa na huduma zote kwa viongozi lakini pia kitatoa huduma kwa wananchi waishio vijiji vya jirani.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu aliwataka mawaziri walioko Mtumba wajiandae kwani kuna siku atakwenda kufanya vikao vyake kwenye wizara zao kwa sababu amebaini kuwa kila wizara ina ukumbi mkubwa wa mikutano.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akionyeshwa mfano wa kamera na Waziri wa Maliasili na Utalii, Khamis Kigwangalla, kwenye ofisi ya wizara hiyo, wakati akikagua ofisi za wizara katika mji wa serikali eneo la Mtumba, jijini Dodoma jana. **PICHA: OWM** .

## Tembo waua mwanamke

**Na Stevie Chindiye, TUNDURU**

MKAZI wa Kijiji cha Mpanji kata ya Mbati wilayani Tunduru Mkoa wa Ruvuma, Mussa Kumambi (52), amefariki katika tukio la kushambuliwa na tembo.

Mume wa marehemu, Hamad kisanje Sandali, alisema yeye na mkewe walivamiwa na kundi la tembo hao wakati wakielekea shambani, hivyo kila mmoja aliamua kukimbilia sehemu yake ili kujiokoa.

Alisema wakiwa katika harakati hizo, mkewe alishindwa kujiokoa baada ya tembo mmoja kumuona na kumfukuza na hatimaye kumkamata na kumkanyaga kanyaga hadi kufa.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti Diwani wa kata hiyo, Rajab Hamissi Mussa, Mtendaji wa kata, Joseph Juma Simeo na Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji hicho, Yusuf Issa Rashid, walisema marehemu alikumbwa na mkasa huo April 21, mwaka huu majira ya saa 1.00 asubuhi akielekea shambani.

Walisema baada ya kupokea taarifa za tukio hilo walipeleka taarifa kwa viongozi wa serikali kwa ajili ya kuomba usaidizi wa kisheria.

Mganga aliyeufanyia uchunguzi mwili wa marehemu kumambi, Dk. Fredi Mabena, alisema chanzo cha kifo hicho ni kutokwa na damu nyingi.

Kamanda wa Polisi wa mkoa wa Ruvuma, Simon Marwa, alithibitisha kuwapo kwa tukio hilo na kwamba Polisi inaendelea na uchunguzi.

# Mashahidi 30 kujenga ushahidi kesi vigogo Rahco

**Na Elizabeth Zaya**

UPANDE wa mashitaka katika kesi ya uhujumu Uchumi inayowakabili vigogo wa Kampuni Hodhi ya Mali za Shirika la Reli (Rahco), unatarajiwa kuita mashahidi 30 pamoja na vielelezo 80 wakati wa usikilizwaji wa shauri hilo.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Mei 6 mwaka huu itakapoanza kusikilizwa baada ya jana kupelekwa mahakamani hapo mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba ambapo upande wa mashitaka uliwasomea hoja za awali washitakiwa hao.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji, Benhadard Tito, Mwanasheria wa Rahco, Emmanuel Massawe na mfanyabiashara ambaye pia ni mwakilishi wa kampuni ya Rothschild (South Africa) Proprietary Limited, Kanji Mwinyijuma.

Washitakiwa hao walipewa nakala za hoja hizo kwa ajili ya kuzipitia wakishirikiana na mawakili wao wa utetezi ambapo baada ya kuzipitia na kuhojiwa na mahakama walikiri majina yao, vyeo na kwamba waliletwa mahakamani na kusomewa mashitaka huku wakikana mashitaka pamoja na hoja zote zilizobaki.

Kwa mujibu wa hoja hizo, ilidaiwa kwamba, mshitakiwa Mwinyijuma ambaye ni Raia wa Kenya kati ya Septemba 2014 na Desemba 30 mwaka 2015 aliteuliwa na Waziri wa Uchukuzi kipindi hicho Harrisson Mwakyembe kutoa ushauri na mapendekezo yake kwa wizara hiyo na Rahco kuhusu mradi wa ujezi wa Reli ya kati.

Ilidaiwa kwamba, pamoja na mambo mengine, mshitakiwa Massawe pamoja na wadhifa wake huo, pia alikuwa mjumbe wa bodi ya Rahco na alikuwa na mamlaka ya kusimamia mchakato wa kumpata mzabuni na kumsainisha mkataba wa mzabuni kwa mujibu wa sheria.

Ilidaiwa kwamba,kati ya Desemba mosi 2014 hadi Desemba 30, 2015 washitakiwa wote waliingia katika mazungumzo kuhusu ujenzi wa Reli hiyo na kuielekeza Rahco kupata ushauri kutoka kwa kampuni ya Rothschild (South Africa) Proprietary Ltd kama mshauri wa mradi wa uimarishaji wa reli hiyo kwa gharama ya dola za Marekani 1,357,000 bila kushirikisha bodi ya Rahco.

Kwamba, washitakiwa hao waliwasilisha mkataba kati ya kampuni hizo mbili kwa Mwanasheria Mkuu wa serikali kwa ajili ya kuupitia na kopi zingine zilipelekwa kwa Mamlaka husika kama Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Mkaguzi wa ndani na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa mujibu wa sheria.

Ilidaiwa kwamba,Februari 27,2015 kwa kupitia barua EA224/355/01, Tito aliikagua kampuni Rothschild (South Africa) Proprietary Ltd kama mshauri wa mradi wa uimarishaji wa reli hiyo.

Ilidaiwa Machi 12, mwaka 2015 Tito na Mwinyijuma waliipitisha kampuni hiyo ya Afrika kusini kuwa mshauri wa mradi wa uimarishaji reli ya kati na kutoa huduma za ushauri wa kifedha kuhusu mradi huo bila kushirikisha bodi ya zabuni ya Rahco.

Pia ilidaiwa Mei 20, mwaka huo 2015 washitakiwa hao walisaini mkataba kati ya kampuni hizo mbili kwa gharama ya dola 1,000,000 bila kodi bila kuhusisha bodi ya wazabuni ya Rahco na kuuwakilisha mkataba huo kwa Mwanasheria Mkuu wa serikali (AG) kwa ajili ya kuupitia.

Ilidaiwa kuwa kati ya Machi Mosi hadi Septemba 2015, washitakiwa wote walipitisha malipo ya awali ya dola 500,000 kwa kampuni hiyo ya Afrika Kusini na kusababishia Rahco kupata hasara ya jumla ya Dola 527,540.

Ilidaiwa Agosti 18, 2015 Tito akiwa na wadhifa wake, aliipitisha Kampuni ya M/s China Railways Construction Corporation kufanya ujenzi wa Reli kwa kilometa mbili eneo la Songa kwa gharama ya Dola 2,312,229 bila idhini ya bodi ya zabuni ya Rahco kinyume cha sheria.

# Ripoti IMF yazua jambo bungeni

INATOKA UK 2

ruhusu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango kutoa ufafanuzi kuhusu madai hayo.

Katika maelezo yake, Dk. Mpango aliwataka wabunge wasiwahishe mjadala kwa kuwa serikali bado inazungumza na IMF na hakuna sehemu ambapo wamezuia, akisisitiza kuwa ni utaratibu wa IMF yenyewe.

Waziri Mpango alisema: "Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi katika majadiliano ambayo yanaitwa 'Article Four Consultations', timu ya IMF ilikuwa hapa nchini kuanzia Novemba 26 mpaka tarehe 7 Desemba mwaka jana na baada ya pale walitoa taarifa.

"Na kwa utaratibu ni kwamba wakitoa ile rasimu ya taarifa inarudi serikalini ili tuweze kuitolea maoni na wao waweze kuyazingatia kabla ya kuichapisha hiyo ripoti.

"Hiyo ripoti nilikuja kuiona tarehe 18 Machi na hiyo ripoti baada ya kuwa sisi tumemaliza maoni yetu, maoni yetu hayajazingatiwa kwenye hiyo taarifa.

"Na Mheshimiwa Spika, nilipokuwa Washington (Marekani) juzi, nilizungumza na Bwana Abebe Selassie, Mkurugenzi wa African Department na mpaka leo (jana) saa tisa, bado tutaendeleza majadiliano kuhusu jambo hili na kwa utaratibu ni kwamba baada ya 'Executive Board' (Bodi ya Wakurugenzi) ya IMF kuijadili hiyo taarifa, serikali inakuwa na siku 14 za kuipitia na kusema itolewe au isitolewe."

Dk. Mpango aliwataka wabunge kutowahisha mjadala kwa kuwa serikali bado inazungumza na IMF na hakuna sehemu ambapo wamezuia, bali ni utaratibu wa IMF yenyewe.

Baada ya Dk. Mpango kutoa ufafanuzi huo, Mwakajoka alisimama na kueleza kuwa anashukuru kwamba waziri huyo amekiri maoni yao hayakuzingatiwa ndiyo maana hawajaruhusu.

"Kwa hiyo, sikuwa muongo kama alivyokuwa anazungumza Mnadhimu Mkuu wa Serikali (Mhagama), niko sahihi kabisa," Mwakajoka alisema.



Wafanyabiashara wa viazi mbatata wakisubiri wateja katika Soko la Ilala, jijini Dar es Salaam jana. Ndoo moja ya viazi iliuuzwa kwa bei ya 13,000/-. **PICHA: MIRAJI MSALA.**

## ... Prof. Lipumba ashauri taarifa ichapishwe

INATOKA UK 2

IMF kinaiweka Tanzania kwenye picha mbaya kuwa haiko wazi, serikali haitaki kukosolewa au haiko tayari kurekebisha makosa au upungufu wa sera zake.

"Mimi sijaona taarifa hiyo, hata hivyo kuna mambo ya wazi ambayo huenda yamejadiliwa kwa kina," Prof. Lipumba alidai.

Kuhusu viashiria vya kushuka kwa uchumi, Prof. Lipumba alisema Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), wanafanya makadirio ya ukuaji wa uchumi kwa kujumlisha uzalishaji, uwekezaji wa vitega uchumi kama ununuzi wa ndege na ujenzi wa reli ya kisasa.

Alisema uwekezaji mwingine huenda usilete matunda katika siku za karibuni na wakati mwingine ukaleta hasara badala ya faida.

Prof. Lipumba alisema uchumi unapimwa kwa hali ya maisha ya wananchi, akitania kuwa kuna kelele za vyuma kukaza.

"Suala la vyuma kukaza linatokana na kasi ya uchumi wa kaya kwa maana ya matumizi ya kaya hayakui kwa kasi kubwa bali yanakuwa kwa kasi ndogo kuliko idadi ya watu na hiyo inatoa taswira ya vyuma vimekaza," Prof. Lipumba alidai.

Alidai mzunguko wa fedha umepungua nchini kulinganisha na miaka ya nyuma ambapo ulikuwa kwa tarakimu mbili, lakini sasa ni tarakimu moja.


MASETO COMPANY LIMITED

MULT INSURANCE AGENT — DEBT COLLECTOR — AUCTIONEER

P.O. BOX 75087, DAR ES SALAAM, TANZANIA.
Mobile: + 255 784 622 019, +255 715 622 019, +255 765 999 000
Tel: +255 0222181477 Fax +255 0222181477
Email: shabani.chuki@yahoo.com

**NOTISI/TANGAZO LA MNADA**

Kwa ishini tuliyopewa na Banki ya AKIBA COMMERCIAL BANKS PLC tunatangaza kuuza dhamana za wadaiwa sugu walioshindwa kulipa mikopo yao katika Benki ya Akiba. Pia hii ni taarifa ya kulipa deni ndani ya siku 14 tangu kutolewa kwa tangazo hili kabla yam nada.

| S/N | JINA LA MTEJA | UMILIKI WA DHAMANA | AINA YA DHAMANA NA MAHALI ILIKO | TAREHE NA MUDA WA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 001 | PETER MATHEW SHIRIMA (TAWI LA AGGREY) | PETER MATHEW SHIRIMA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO KIMARA TEMBONI CHARANGA- DSM | 20/05/2019 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 002 | FREDRICK BALTAZARY PETER (TAWI LA AGGREY) | FREDRICK BALTAZARY PETER | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO MTAA WA ULONGONI 'A' UKONGA-DSM | 22/05/2019 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 003 | IZZACK SHAMTE MTANDIKA (TAWI LA TEMEKE) | IZZACK SHAMTE MTANDIKA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO MSONGOLA SANTIAGO – DSM | 23/05/2019 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 004 | REVOCATUS LUCAS BEKEEZA (TAWI LA TANDALE) | REVOCATUS LUCAS BEKEEZA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO MTAA WA KIPUNGUNI – WILAYA YA ILALA | 24/05/2019 SAA 06:00 MCHANA |
| 005 | VICK SYLIVESTER MUSHI (TAWI LA TANDALE) | HAMAD RASHID CHANDE | KIWANJA CHENYE MSINGI CHENYE HATI YA MAUZIANO KILICHOPO TABATA KIFURU-DSM | 27/05/2019 SAA 08:00 MCHANA |
| 006 | HAMAD ABDALLAH MNEMBWE (TAWI LA TANDALE) | HAMAD ABDALLAH MNEMBWE | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI INAPATIKANA TANDALE | 28/05/2019 SAA 04:00 ASUBUHI |

**Masharti ya Mnada**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku hiyo hiyo yam nada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14) kukamilisha malipo yote, ukishindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25% na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, na zingine zinazoambatana na hili ni juu ya mnunuzi.

Kwa taarifa zaidi wasiliana na:
MKURUGEZI MTENDAJI
AKIBA COMMERCIAL BANK PLC AU COLLECTION
P.O. Box 669
DAR ES SALAAM
Tel: 255 02221183403

MKURUGENZI MTENDAJI
MASETO AUCTIONEER AND DEBT
P.O. Box 25087
DAR ES SALAAM
Tel: +25502184653/0765999000

115191702


# Mapya ya daktari anayetuhumiwa kukataa kurejea kazini Ijumaa Kuu

INATOKA UK 3

"Daktari alikuwapo, asubuhi aliingia saa mbili na kutoka saa tisa alasiri, hata hawa wajumbe kamati ya siasa ya CCM Kata ya Levolosi walifika kituoni, kwa bahati mbaya akawa ameshatoka," alidai.

"Muda wa kukaa kituoni ulikuwa umekwisha, lakini kuondoka kwake hakukufanya huduma nyingine zisitolewe, ilitakiwa lazima awapo daktari mwingine, haiwezekani kituo kibaki bila daktari yeyote, daktari huyu alipopigiwa simu akitakiwa arudi kituoni, lakini alijibu kuwa harudi."

Dk. Maden alidai majibu yaliyotolewa na daktari huyo siyo majibu ya kiuongozi kwa kuwa alitakiwa atoe kauli ya kufariji.

"Alitakiwa kutoa majibu ya kufariji kwamba jamani eeh, nimepata dharura nimekuja sehemu fulani, nisubirini hapo nitarudi. Ingetokea mgonjwa akafariki dunia ingekuwaje?" Dk. Maden alihoji.

Hata hivyo, Dk. Maden alisema jiji halijazungumzia kuhusu kamati ya siasa kufika hospitalini japo anatambua zipo taratibu za kuzingatiwa ili kutembelea hospitali au kituo cha afya.

Alisema jiji linawajibika na majibu yaliyotolewa na daktari kwa mbele ya kamati hiyo iliyokwenda kituoni siku hiyo.

Kaimu Mganga Mkuu wa Jiji la Arusha, Dk. Samson Joseph, alisema baada ya kuona taarifa mtandaoni na baadaye kupitia simu kwa kuwa ipo timu ya uendeshaji wa huduma vituoni ngazi ya wilaya na jiji, walifuatilia suala hilo.

Dk. Joseph alisema wamefuatilia na kubaini hapakuwa na madhara kutokana na kutokuwapo kwa daktari kituoni siku hiyo kwa kuwa wamebaini daktari huyo alikuwapo kituoni na baadaye alitoka kwa muda kufuatilia mambo yake binafsi.

"Baada ya timu ya ziara ya kamati ya CCM ngazi ya kata kufanya ufuatiliaji, majibizano yaliyokuwapo baina ya daktari na timu hayakuwa mazuri," alidai.

Alisema daktari alitakiwa kumkabidhi mwenzake kituo kabla ya kuondoka, lakini kuna uwezekano aliamua kutofuata utaratibu huo kwa kuwa alikuwa anarejea tena kituoni siku hiyo.

# Mazingira ya uwekezaji Tanzania yapongezwa

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

SERIKALI imepongezwa kwa kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji.

Pongezi hizo zimetolewa na kampuni inayojihusisha na utengenezaji wa vifaa tiba ya Radian Qbio ya Korea Kusini, ambayo pia imeishukuru serikali ya Tanzania kwa msaada wa kweli na wa kirafiki katika kutimiza ajenda ya kampuni hiyo kuwekeza nchini.

Akizungumza katika viwanja vya Bunge jijini Dodoma mwishoni mwa wiki na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto,

Ummy Mwalimu, Mkurugenzi Mtendaji wa Radian Qbio, Prof. Sang Young, alisema kampuni yake imejipanga katika kuwekeza katika kiwanda cha kutengeneza vifaa tiba.

"Tumevutiwa kwa namna ambayo maofisa wa serikali kutoka Bohari Kuu ya Dawa (MSD) na Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) walivyoshughulikia suala letu ili pamoja na mambo mengine tuweze kufanya shughuli za uwekezaji Tanzania,"alisema Prof. Young.

Prof. Young aliongeza kuwa kwa sasa kampuni yake ipo katika hatua za awali kuhakikisha inafuata sheria na taratibu za serikali ili kampuni hiyo iweze kuuza na kusambaza vifaa tiba nchini.

"Kwa sasa tupo katika majadiliano na serikali ili kuona namna nzuri ya kufuata taratibu na sheria zilizopo ili kampuni yetu iweze kuuza na kusambaza vifaa tiba hapa na mazungumzo ambayo yanaendelea vizuri," alisisitiza Prof. Young.

Alisema amevutiwa pia na Waziri kwa hatua yake ya kuviunganisha vyuo vikuu vya Tanzania vikiwemo Chuo Kikuu Dodoma na Chuo Kikuu cha Nelson Mandela na vyuo vikuu vya Korea ili viweze kushirikiana katika nyanja mbalimbali.

Kwa upande wake, Waziri Mwalimu alishukuru ujumbe huo kwa kuchagua kuwekeza Tanzania na kuongeza kuwa kuna maeneo mazuri ya kiuwekezaji hususani katika sekta ya afya.

"Karibuni kuwekeza Tanzania na serikali itahakikisha ndoto zenu za kuwekeza hapa zinakamilika," alisema na kuongeza kuwa kinachotakiwa ni kufuata taratibu na sheria zote zinazohusu uwekezaji.

"Tunao wataalamu na taasisi kama vile TFDA ambazo zina mamlaka ya kuthibitisha kifaa chochote cha matibabu ya kigeni, hakikisheni mnawasiliana na taasisi hiyo," Waziri Mwalimu alisema.

Waziri aliipongeza kampuni hiyo kwa kuandaa mpango huo ambao utatoa fursa kubwa kwa wanafunzi wa Tanzania kujifunza.

Ujumbe wa kampuni hiyo ulimtembelea Waziri kufuatia wito wa wizara kwa kampuni ya Radian Qbio ambapo ilikuwa ni fursa kwa watendaji wa vifaa tiba kuona namna kampuni hiyo inavyofanya kazi.

Radian Qbio imegundua mashine mpya ijulikanayo kama Cell Qube ya kupima magonjwa zaidi ya 12 kwa muda mfupi na gharama nafuu.

# Waziri asisitiza zuio mifuko plastiki

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), January Makamba, amesisitiza kuwa zuio la mifuko ya plastiki litakuwa la kisheria, hivyo hakutakuwa na msalie mtume.

Alizungumza katika mahojiano katika vipindi vya wakati mmoja vya radio na televisheni hapa jijini jana, Waziri Makamba alisisitiza kuwa marufuku ya mifuko hiyo lengo lake ni kulinda afya za wananchi na mazingira.

"Madhara yanayotokana na matumizi ya mifuko hiyo ni makubwa sana na hivyo siyo rahisi kwa mtu kuona katika hali ya kawaida", alisema na kuongeza kuwa wizara yao itahakikisaha zoezi hilo linafanikiwa bila vikwazo na kwamba wananchi wataendelea kuelimishwa.

"Katika kukabiliana na zuio hili changamoto ni nyingi ikiwamo kutokuwa na ufahamu mpana wa wananchi juu ya athari zake, lakini tumejipanga kuhakikisha linafanikiwa na hatua muhimu zaidi ni kutoa elimu kwa wananchi," alisisitiza na kuongeza:

"Katazo la kitu kama hiki halikosi vikwazo, kelele na hata vitisho kutoka kwa watumiaji na wazalishaji. Hivyo tumejipanga kukabiliana na yote hayo," ameeleza.

Alisisitiza kuwa elimu ya kutosha itatolewa kuhusu madhara ya mifuko ya plastiki na njia mbadala zitaanza kutumika wakati wa kipindi cha zuio.

"Tumejipanga kiasi cha kutosha juu ya namna ya kukabiliana na changamoto zitakazojitokeza na jambo muhimu sana ni ushirikiano wa kuwa mazingira ni suala muhimu kwa kizazi cha leo na kesho, hivyo ni jukumu la kila mwananchi kuyalinda," alisema Makamba.

Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) wiki iliyopita lilieleza kuwa litatekeleza kwa ukamilifu agizo la serikali kwa kutumia sheria.

Akizungumza na Waandishi wa Habari jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema Sheria ya Mazingira na Kanuni zake vinazuia utengenezaji na matumizi ya kitu chochote kinachoharibu mazingira, ikiwa ni pamoja na mifuko ya plastiki.

"Marufuku hii ina maana kubwa sana katika ustawi wa mazingira ya nchi yetu. Usimamizi wa marufu hii utaanzia ngazi ya mtaa hadi taifa maana katika ngazi zote hizi tuna ofisi za mazingira. Tutatumia sheria kwa nguvu zetu zote, bila ubaguzi. Tutatumia sheria bila kujali nafasi ya mtu katika jamii, cheo, rangi au mahali anakotoka," alifananua.

Marufuku ya matumizi ya plastiki ilitangazwa bungeni na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa katika kikao cha bajeti kinachoendelea jijini Dodoma. Marufuku hiyo itaanza Juni Mosi, mwaka huu.

Katika maandalizi ya kufanikisha utekelezaji wa marufuku hii hatua mbali mbali zimechukuliwa na serikali ikiwamo mkutano wa kueleza fursa za utengenezaji wa mifuko mbadala uliofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni.




Mtaalamu wa Uchumi kutoka Stanbic Bank, Jibran Quereishi, akizungumza katika Jukwaa la Kujenga Ujuzi kwa Wateja lilioandaliwa na benki hiyo, kwa ajili ya kuwaonyesha wateja wake fursa mbali mbali zilizopo katika kilimo cha biashara pamoja na utalii, hivi karibuni mkoani Arusha. Benki hiyo iliandaa jukwaa hilo ili kutekeleza ahadi ya kuwasaidia wateja wake kufikia mafanikio yao ya kifedha kwa kupitia fursa zilizopo katika sekta husika. **MPIGAPICHA WETU**

# 3,000 wahitimu chuo Diplomasia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

JUMLA wahitimu 3,421 wamehitimu masomo yao katika Chuo cha Diplomasia nchini tangu kuanzishwa kwake mwaka 1978.

Hayo yalielezwa bungeni jana na Naibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Damas Ndumbaro, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Malindi (CUF), Ally Salehe Ally.

Mbunge huyo alitaka kujua chuo kimetoa wahitimu wangapi toka kuanzishwa kwake mwaka 1978.

Dk.Ndumbaro alisema mpaka sasa kinafundisha lugha saba na kimetayarisha mtaala wa kufundisha lugha ya kiswahili kwa wanafunzi wa kigeni ili kusaidia kueneza lugha hiyo na mafunzo yataanza kutolewa kuanzia mwaka wa masomo 2019/20.

Aidha, alisema wahitimu wa ngazi ya Shahada ni 72, Stashahada ya uzamili katika Menejimmenti ya Mahusiano ya kimataifa ni 503, Shahada uzamili katika Diplomasia ya Uchumi ni 341, Stashahada ya kawaida 2084, ngazi ya cheti ni 347 ni wa mafunzo maalum ya maafisa waandamizi wa mambo ya nje.

Alibainisha kuwa katika idadi hiyo ya wahitimu katika chuo cha Diplomasia wanawake 1,060 na wanaume 2,361.

Alieleza wanafunzi hao walitoka nchi za Afrika Kusini, Algeria, Angola, Butswana, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Guinea, Kenya. Comoro, Libya, Malawi na Msumbiji.

Nyingine ni Namibia , Palestina, Rwanda, Sudan, Zambia na Zimbabwe.

Alifafanua toka kuanzishwa kwa chuo hicho mpaka sasa wanafunzi 500 toka Tanzania walihitimu na kufanya kazi katika maneo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Aliweka wazi kuwa kutokana na umuhimu wa lugha za kufundishia chuo kwa sasa inafundisha kwa kutumia ya lugha mbalimbali za kigeni katika kufundishia.

# Waziri awaonya 'trafiki' waviziaji

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, amewataka askari wa usalama barabarani wenye tabia ya kukamata daladala ovyo kwa kujificha chini ya mwamvuli wa Sheria ya Usalama Barabarani, waache mara moja.

Masauni alitoa onyo hilo jana bungeni jijini Dodoma alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum, Rose Tweve (CCM), aliyedai kumekuwa na changamoto ya askari hao kusimamisha daladala ovyo ili kukagua kama kondakta na dereva wamevaa sare wakati jambo hilo linatakiwa kufanyika kabla gari kuanza safari, hivyo kusababisha wananchi kuchelewa kuripoti kazini.


Masauni alisema sheria hiyo iliyorejewa mwaka 2002 inampa mamlaka askari kupitia kifungu cha 81 kusimamisha gari lolote barabarani au sehemu yoyote anapopolitilia shaka na kulikagua au pindi linapokuwa limetenda kosa.

"Kuwa na utaratibu wa lazima, kama serikali tumeshalitafakari kwa kina na haliepukiki katika karne hii kwa kuwa tunahitaji kuwa na magari salama," alisema.

Aliongeza kuwa katika mabadiliko ya sheria yanayokuja, suala hilo litasimamiwa na baraza jipya la usalama barabarani.

"Jeshi la Polisi limeshaandaa utaratibu wa kuwa na vituo maalum vya ukaguzi vya mabasi ya umma na tunataka utaratibu huu uanze haraka," alisema.

Katika swali lake la msingi, mbunge huyo alihoji ni lini serikali itaandaa utaratibu wa kuwa na vituo maalum vya ukaguzi ili kusaidia matumizi mazuri ya muda kwa magari




Na Augusta Njoji

yanayobeba abiria hususan daladala.

Masauni alisema ukaguzi wa pembezoni mwa barabara ambao huhusisha mabasi ya daladala na vyombo vingine vya moto, hufanyika katika vituo vya ukaguzi maalum ambavyo vipo katika barabara kuu na vingine vya miji na majiji.

Alisema uwapo wa ukaguzi ni jambo la msingi ili kuongeza mapato kwa Jeshi la Polisi na kwamba mabadiliko yajayo ya sheria yatasimamiwa na baraza jipya la usalama barabarani litakalokuwa na muundo mpya.

Mbunge wa Viti Maalum, Catherine Magige (CCM), alihoji ni lini stahiki za askari wanaopata ajali wakiwa kazini zitalipwa.

Katika majibu yake kwa mbunge huyo, Masauni alikiri kuwapo kwa changamoto nyingi kwenye malipo ya askari nchi nzima, lakini kwa sasa sehemu kubwa ya malimbikizo yameanza kulipwa.

"Malipo yaliyobaki yatakamilishwa kuendana na uhakiki na upatikanaji wa fedha zitakazotengwa kwa ajili ya zoezi hilo," Masauni alisema.



Waziri wa Afya , Ummy Mwalimu (kulia), akizungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Radian Qbio inayojishughulisha na utengenezaji wa vifaa vya tiba kutoka Korea Kusini, Prof. Sang Young, kwenye eneo la Bunge jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. Habari Uk. 9. **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

# Kodi taulo za kike bil. 5.5/-

SERIKALI imesema katika kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2016/17 hadi 2017/18, ilikusanya Kodi ya Ongezeko la thamani (VAT) Sh. bilioni 5.5 kwenye taulo za kike (sanitary pads) zilizoingizwa nchini kabla ya kodi hiyo kuondolewa Juni mwaka jana.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni jijini Dodoma na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Upendo Peneza.

Katika swali lake, Peneza alitaka kujua katika mwaka wa fedha 2016/17 na 2018/19, serikali ilikusanya kiasi gani cha kodi kwa taulo za kike zilizotengenezwa nchini na zilizoingia kabla ya VAT kuondolewa kwenye bidhaa hizo.

Katika majibu yake, Dk. Kijaji alisema katika mwaka wa fedha 2016/17, serikali ilikusanya VAT ya Sh. bilioni 3.01 na Sh. bilioni 2.54 kwa mwaka wa fedha 2017/18 kwenye bidhaa hizo zilizoingizwa nchini.

Hata hivyo, Peneza alihoji sababu za ukubwa wa bei ya bidhaa hiyo nchini licha ya kodi kuondolewa na pia mpango wa serikali kusimamia suala hilo ili bei zishuke.

Katika majibu yake kwa mbunge huyo, Dk. Kijaji alisema serikali iko kwenye soko huru kwa bidhaa zote na kwamba haijashindwa kusimamia na ndiyo maana baada ya kuondoa kodi, imeendelea kupokea maoni.

Alisema utafiti unafanyika na wameenda nchi za Afrika Kusini, Botswana na Kenya ambazo pia zilichukua uamuzi wa kufuta kodi kwenye bidhaa hizo, lakini zikagundua hatua hiyo haiwezi kuleta matokeo chanya.

"Hivyo, tunatakiwa kuhakikisha wanapewa taulo hizo bila kuhusishwa na kodi, tutafanya utafiti na kujiridhisha kama watoto wetu wanaweza kupewa hivyo alivyotaka mbunge, tutaleta ombi maalum bungeni," alisema.

# Spika aitaka serikali iajiri walimu

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, ameishauri serikali kuweka utaratibu wa kuajiri walimu wa somo moja moja, hususani Hisabati ambalo lina uhaba mkubwa wa walimu.

Alitoa ushauri huo hilo bungeni jijini Dodoma jana baada ya Mbunge wa Buhigwe (CCM), Albert Ntabaliba, kuitaka serikali kutaka idadi ya walimu wa masomo ya Sayansi na Hisabati waliopo nchini kwa sasa.

"Unakuta shule haina mwalimu wa hesabu hata mmoja, hebu angalieni tupate ajira ya walimu wa hesabu tupu," Ndugai alisema.

Katika majibu yake kwa mbunge huyo, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara, alikiri kuwapo kwa changamoto ya uhaba wa walimu huku akiahidi kuwa serikali itaendelea kuajiri walimu wa masomo ya Sayansi na Hisabati kadri inavyowezekana.

Alisema walimu wataajiriwa na watazingatia maeneo yenye upungufu zaidi.

"Hii ni awamu ya kwanza kuajiri, ikitokea awamu ya pili tutapeleka walimu wa masomo hayo," Waitara alisema.

Naibu waziri huyo alisema kwa sasa kibali cha kuajiri walimu 4,549 kimeshatolewa na kati yao, 1,374 ni wa masomo ya Sayansi na Hisabati.

Alisema utaratibu wa kuajiri walimu hao unaendelea na watapangwa kwenye halmashauri zenye upungufu mkubwa ikiwamo Buhigwe.

Alisema katika mwaka wa fedha wa 2017/18, Halmashauri ya Buhigwe ilipokea vifaa vya maabara kwa shule mbili za sekondari zilizokamilisha ujenzi wa maabara.

Aliongeza kuwa katika mwaka wa fedha wa 2018/19, serikali inatarajia kununua na kusambaza vifaa vya maabara kwenye shule za sekondari 1,250 zikiwamo shule za sekondari za Halmashauri ya Buhigwe.

Alisema kwa sasa, Halmashauri ya Buhigwe inao walimu wa masomo ya Sayansi na Hisabati 83, lakini mahitaji 155 na kwamba wataongezwa kwa mujibu wa taratibu za ajira serikalini.

# Wito kusaidia yatima, wenye uhitaji

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

WATANZANIA wametakiwa kusaidia watoto yatima ili na wao wapate faraja kwa kuona wana thaminiwa kuliko kuachia serikali pekee.

Mkazi wa Mji mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara, Jaqueline Momo, aliyasema hayo jana kwenye kituo cha Light In Africa, baada ya kutoa msaada wa vyakula wenye thamani ya Sh. 500,000 akishirikiana na mwenzake, Rose Kweka.

Momo alisema watu wanapaswa kutambua kuwa watoto hao ni sawa na wao, hivyo wanapaswa kupewa mahitaji mbalimbali na kufarijiwa, ili wajione kuwa na wao wana wazazi.

Alisema baada ya kutembelea kituo hicho akiwa na wanawake wenzake wa Wilaya ya Simanjiro, aliahidi kurudi tena na kutoa kidogo alichonacho kwa ajili ya watoto hao.

"Watoto hawa ni wetu sote tunapaswa kuwafariji, binafsi nashukuru kutimiza ahadi yangu kuwa nitafanya jambo kwa ajili yao na Mungu amesaidia tumekula nao Pasaka," alisema Momo.

Rose Kweka alisema ametoa msaada huo kwa kushirikiana na Momo na anamwomba Mungu azidi kumuongezea kipato ili azidi kuwasaidia watoto hao.

Kweka alisema anawapenda watoto hao, kwa kuwa hata yeye anawapenda ndiyo sababu akajitolea kidogo alichonacho kwa ajili ya kusherehekea sikukuu ya Pasaka.

"Rafiki yangu Jack Momo alinishawishi tuje kwenye kituo hiki tule sikukuu pamoja na watoto hawa, kweli tumekuja ila nawapenda kwa kuwa wamepata faraja kubwa kutuona leo," alisema Kweka.

Mmoja kati ya watoto wa kituo cha Light In Africa, Grace Shayo, aliwashukuru kwa kutolewa msaada huo na kuomba wadau wengine waige mfano huo. Shayo alisema siyo lazima mtu awe na msaada mkubwa ndiyo atake kuwasaidia watoto, hata akiwa na kidogo alichojaaliwa na Mungu atakuwa amewasaidia endapo atawapa kwa moyo wa kutoa.

Msaada uliotolewa na wadau hao ni mchele, sukari, mafuta ya kupikia, mafuta ya kujipaka, mikate, keki, nguo na kreti tano za soda.



Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Mhandisi Zephania Chaula, akizungumza na watumishi wa Halmashauri ya wilaya hiyo jana. Kushoto kwake ni Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Jackson Sipitieck. **PICHA: GIFT THADEY**

# Matejoo waagizwa kuvunja nyumba zao

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAKAZI wa Kata ya Sakina eneo la Matejoo jijini Arusha, wameagizwa kukubali kwa hiyari yao kuvunga nyumba zao zilizowekwa alama ya X, ili kupisha upanuzi wa barabara itakayowasaidia kuondoa maji ya mvua yanayoingia katika makazi yao.

Akitoa agizo hilo jana mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo pamoja na kamati ya ulinzi na usalama, Mratibu wa Wakala wa Barabaraza Mijini na Vijijini (Tarura), Mhandisi, Mwankenja, alisema eneo la Matejoo hujaa maji mara kwa mara, yanayoingia kwenye nyumba za wakazi hao, kwa sababu wamejenga kwenye mkondo wa maji.

Alisema ili wananchi hao waondokane na kero ya maji kujaa katika nyumba zao, nyakati za mvua ni vyema kwa hiyari yao wakakubali kuvunja nyumba zao zilizowekwa alama, ili kupisha upanuzi wa barabara.

Alisema Tarura haitafidia nyumba hizo zilizowekwa X, bali ni vyema wananchi hao wakaona umuhimu wa kuzibomoa wenyewe ili kupisha upanuzi wa barabara hiyo.

"Tunaomba mkubali kwa hiari yenu kuvunja nyumba zenu, ili kupisha upanuzi wa barabara hii ambayo kila mara maji hujaa na sisi tutawawekea vifusi hadi lini, ilhali mna uwezo wa kubomoa nyumba au ukuta, kupisha upanuzi wa barabara hii na mkawekewa mitaro," alisema.

Awali wananchi hao, Anna Mollel na Mwanahamisi Idd walilalamikia tatizo la uhaba wa maji pamoja na ukosefu wa shule za awali kwa ajili ya watoto wadogo kusoma na kuomba serikali iwatatulie changamoto hizo, na kwamba ingawa kata hiyo ni kubwa na ina watu wengi, lakini haina shule hiyo.

Naye Gambo alisisitiza wananchi hao kukaa vikao kwa pamoja na watendaji wa kata ili kuafikiana kuhusu uvunjwaji wa nyumba hizo na kuta kwa ajili ya kujengewa barabara.

Kuhusu kero ya maji, Gambo aliwaomba wananchi hao wawe wavumilivu hadi mwakani kwa kuwa hivi sasa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (Auwsa) wanajenga miundombinu maeneo mbalimbali, kwa ajili ya kuhakikisha tatizo la maji Jiji la Arusha na viunga vyake linaisha ifikapo 2020.

"Mhandisi Ruth Koya wa Auwsa amesema hapa kuwa kero ya maji ni ya muda tu mvumilie kwani mwakani maji yatakuja hapa na maeneo mengine, hivyo subira inavuta kheri na kuhusu shule za awali na sekondari kaeni angalieni maeneo ili wanafunzi waweze kusoma kwa sababu tunahitaji elimu

# Wajasiriamali washauriwa uboreshaji wa vifungashio

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAJASIRIAMALI wadogo na wa kati nchini, wameshauriwa kuboresha vifungashio vya bidhaa zao wanazozalisha ili kuvutia soko ndani na nje ya nchi.

Hayo yalisemwa na Meneja wa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (Sido) mkoani Arusha, Nina Nchimbi, wakati akizungumza katika hafla ya kufunga mafunzo ya wiki moja kwa wajasiriamali wa kutengeza sabuni za maji na kipande, dawa za kuua wadudu chooni pamoja na dawa za kusafisha vigae.

Nchimbi alisema wajasiriamali wanapaswa kuwa wabunifu wanapozalisha bidhaa zao ili kuongeza ubora katika biashara zao na kuwavutia wateja zaidi kutoka ndani na nje ya nchi.

Alisema wengi wao wamekuwa wakijitahidi katika kuzalisha, ila changamoto kubwa ni katika uboreshaji wa vifungashio, hivyo ambao aliwataka kuwa wabunifu zaidi ili kupata soko la uhakika ndani na hata nje.

"Unapozalisha bidhaa yako kila wakati inakuwa na muonekano ule ule, inakuwa ngumu kupata wateja wapya, hivyo ili muweze kupata wateja wapya ni lazima mbadili muonekano wa vifungashio hivyo viwe vya tofauti na viweze kuvutia wateja na kwa kufanya hivyo, mtapata soko la uhakika," alisema Nchimbi.

Naye Mkufunzi wa mafunzo hayo yalitolewa na Sido, Bahati Mkopi, alisema, mafunzo hayo ya utengenezaji sabuni ni awamu ya nne sasa ambapo zaidi ya wajasiriamali 80 wamehitimu mafunzo hayo na kuleta manufaa makubwa, ikiwamo kuanzisha viwanda vidogo vidogo na vya kati zaidi ya kumi.

Alisema mafunzo hayo yamekuwa yakiwasaidia vijana kujiajiri na kupata uhakika wa kipato kwa kujishughulisha wenyewe na shughuli hizo, kwa kuwa zinafanyika bila kuhitaji mtaji mkubwa.

Mmoja wa wajasiriamali, Mboka Mwakalinga, akisoma risala kwa niaba ya wenzake, alisema, kupitia mafunzo hayo wameweza kupata utambuzi wa kitaaluma ya vyeti ambavyo vitawawezesha katika mambo ya usajili, na kuanzisha viwanda vidogo.

Alisema wanakabiliwa na changamoto kubwa ya upatikanaji wa vifungashio, uhaba wa baadhi ya malighafi na gharama kubwa ya malighafi hizo, hivyo waliomba serikali kupitia Sido na wadau wengine wajengewe mazingira mazuri kwa ajili ya wawekezaji wa malighafi na vifungashio ili waweze kuvipata kwa urahisi.

# Vijiji vyahamasishwa utalii wa utamaduni

**Na MWANDISHI WETU,** SAME

WILAYA ya Same imeanza uhamasishaji wa jamii kuboresha makazi katika vijiji vilivyoko katika kata tatu vinavyopakana na Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi pamoja na msitu asilia wa Chome ili kupata nyumba zaidi ya tano kwa kila kata zitakazotumika katika utalii wa utamaduni.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, alisema mjini hapa kwamba hatua hiyo ni moja ya utekelezaji wa mpango mkakati wa mazingira na utalii Wilaya ya Same wa mwaka 2018 hadi 2023.

Senyamule alisema uboreshaji huo wa nyumba ni wa muhimu kwa ajili ya kuanza utalii wa utamaduni kwa watalii wanaopenda kushiriki katika utamaduni na asilia ya wenyeji.

Alisema uboreshaji huo katika kata za Chome, Kisiwani pamoja na Mwembembagu kwa kiasi kikubwa utazingatia nyumba kuwa na vyoo bora kabla ya kupitishwa kuwa sehemu ya utalii wa utamaduni.

"Utalii wa utamaduni au asili una nafasi kubwa ya kutengeneza ajira nyingi kwa vijana na wanawake wajasiriamali wilayani Same kwa watalii wanaopita maeneo mbalimbali kabla ya kufika katika maeneo ya utalii wa wanyamapori ya Mkomazi au kupanda Mlima Shengena," alisema.

Senyamule alisema katika mpango mkakati huo wamepanga kutangaza kwa kuunganisha pamoja vivutio vya utalii vilivyopo wilayani Same alivyovitaja ni Mlima Shengena uliopo ndani ya hifadhi ya mazingira asilia ya Chome na Hifadhi ya Mkomazi.

Adha, alisema kuwa katika kuunganisha kwa vivutio pia wataujumuisha na Mlima Kilimanjaro ambapo watahamasisha watalii wanaokwenda kupanda mlima huo mrefu kuliko yote Afrika waanze kwa kupanda Mlima Shengena kama sehemu ya maandalizi au mazoezi.

Alisema licha ya utalii wa wanyamapori na kupanda kilele cha Mlima Shengena, pia kuna idadi kubwa ya watalii wanaopenda kufahamu mila, silka, desturi, majengo ya kale, zana za kazi, ngoma, lugha, hadithi, vyakula na kilimo cha tangawizi kwa wenyeji kabila la Wapare.

"Mtalii anapokuja kutembelea mbuga za wanyama anashawishiwa kupita katika maeneo yenye utalii wa asili na kiutamaduni na kujifunza maisha ya wenyeji, na katika kupata huduma kuna malipo ya fedha yanabaki kwa wenyeji," alisema.



Wakazi wa jiji wakisaidia kulisukuma gari lenye namba za usajili T 317 BCN, baada ya kuzimika ghafla katika taa za kuongozea magari za Namanga, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**.

# Mkakati kufanya vizuri kitaaluma

**Na Mary Mosha,** MOSHI

KATIKA harakati za kuhakikisha Manispaa ya Moshi inaendelea kufanya vizuri katika mitihani yake ya kitaifa kwa shule za msingi, imeanzisha programu maalumu ya kutoa mafunzo kwa walimu wa shule za awali.

Lengo la mafunzo hayo ni kuhakikisha hakuna mwanafunzi hata mmoja atakeyefika darasa la saba bila kusoma wala kuandika.

Mafunzo hayo yalitolewa kwa walimu zaidi ya 70 wa shule za serikali na lengo ni kuimarisha mbinu za kufundishia watoto kwa vitendo katika mazingira yao.

Akifunga mafunzo hayo jana, Mkurugenzi wa Manispaa ya Moshi, Michael Mwandezi, aliwaasa walimu kuhakikisha wanatumia vifaa vinavyopatikana katika maeneo yao ya shule ili kuhakikisha watoto wa awali waelewa kwa haraka.

"Kwa kipindi cha miaka miwili mfululizo tumekuwa tukiongoza katika mkoa wa Kilimanjaro na hatutaraji kuiachia nafasi hiyo na hiyo ndiyo sababu ya kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa walimu wa awali kwa kuwa wamekuwa wakimpokea mtoto ikiwa bado ubongo wake haujaanza kuharibika na kuutunza," alisema Mwandezi na kuongeza:

"Manispaa ya Moshi tumeweka mkazo ili wazazi wachangie chakula na kwa shule za awali... wamekuwa wakipewa uji wa lishe, lengo watoto waweze kujifunza vizuri zaidi na kuondoa tatizo la utapiamlo kwa watoto."

Kwa upande wake Afisa Elimu wa Manispaa hiyo, Patrick Leana, aliwapongeza walimu waliopata mafunzo ya namna bora ya kuwafundisha watoto wa awali kwa kutumia rasilimali zinazopatikana katika mazingira yao ikiwamo majani, nyasi na udongo.

Alisema mbali na kutoa mafunzo kwa walimu wa awali, pia wametoa mafunzo kwa walimu wakuu kwa siku moja ambayo yatawasaidia kuhakikisha yanamsaidia mwalimu wa awali na wanafunzi kupata mahitaji ya msingi.

"Hatujaishia hapo pia tutatoa mafunzo kwa shule zote za binafsi ili kutokomeza tatizo la watoto watakaomaliza darasa la saba bila kujua kusoma na kuandika... sambamba na hilo kutakuwa na ufuatiliaji wa kutosha wa kuhakikisha mafunzo yaliyopatikana yanawasaidia watoto hao," alisema.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Winefrida Tarimo, alishukuru kwa mafunzo hayo na kuiomba serikali kuangali uwezekano wakutoa mafunzo hayo mara kwa mara ili kuwasaidia walimu na wanafunzi.

# Wazazi walalamikia bodi ya shule

**Na Mary Mosha,** MOSHI

BAADHI ya wazazi wa Shule ya Msingi Mwangaria katika Kata ya Kahe Mangaribi, Wilaya ya Moshi, wameiomba serikali kuvunja bodi ya shule hiyo kwa madai ya kutoshirikishwa miradi ya maendeleo na kukatwa miti bila kuwashirikisha .

Wakizungunza katika kikao cha dharura cha uongozi wa shule hiyo na wazazi, Grayson Yusufu alisema bodi hiyo chini ya Mwenyekiti, Stantaely Simon, wamekuwa wakifanya mambo bila kuwashirikisha wazazi, jambo ambalo linakwamisha maendeleo.

Alisema wamefikia hatua ya kutaka bodi ivunjwe kutokana na kushindwa kuwashirikisha katika miradi ya maendeleo ikiwamo kukata na kuuza miti ya shule.

"Uongozi wa shule unatupa sababu nyepesi eti kulikuwa na pesa zinahitajika, ukaamua kuuza miti hiyo bila kutushirikisha jambo ambalo sisi hatukubaliani nalo... kama kuna shida yoyote tulipaswa kushirikishwa," alisema Magdalena Zakaria na kuongeza:

"Miti hiyo tumeiotesha kwa garama kubwa sana... sisi kama wanakijiji na hatutamruhusu mtu yeyote kuikata kutokana na hali ya hewa ya ukanda wa chini, hivyo tunajitaidi kutunza mazingira yetu wenyewe."

Akijibu tuhuma hizo mwenyekiti wa shule hiyo, Stantaely Simon alikiri kuuzwa kwa miti hiyo na kusema fedha hizo zilielekezwa katika matumizi madogo madogo ya shule ambayo yameonyeshwa kwenye mapato na matumizi.

"Tulilazimika kuuza miti hiyo kutokana na kuwapo kwa wageni waliokuwa wakichimba kisima kama mradi wa maji katika kugharamia chakula cha mchana muda wote ambao walikuwa ya shule na matumizi mengine madogo madogo ya shule," alisema.

Akizungunzia madai ya kutowashirikisha wazazi,

alisema yapo baadhi ya matukio ambayo yanafanyika kwa udharura ingawa lengo ni kuwashirikisha wazazi kwenye vikao, lakini imekuwa ikishindikana kutokana na wazazi kukaidi wito wa vikao mara kwa mara.

Kwa upande wake Diwani wa kata hiyo, Rodrick Mmanyi, alipotakiwa kutoa ufafanuzi alikiri kutokupewa taarifa zozote juu ya ufujaji wa mali za shule na kutoshirikishwa kwa wazazi na kusema kufanya hivyo ni kinyume cha sheria na taratibu .

"Nitalifutaitilia kwa ukaribu suala hilo na kuhakikisha tunaliweka sawa na kama kuna viongozi wamekiuka miiko ya maadili yao , tutawachukulia hatua kwa mujibu wa sheria... ni haki ya wazazi kushirikishwa kwa kila jambo wanalofanya ili kutoa mawazo yao na maendeleo ya shule yao," alisema Diwani Mmanyi.

Naye Mkuu wa wilaya hiyo, Kippi Warioba, alipotakiwa kuzungunzia jambo hilo alisema hana taarifa hizo ila atalifutatilia.



Ukurasa 18

**JENERALI YAKUBU GOWON**

## MAKALA:

Sudan 'itakavyoishi' bila Al Bashir



Ukurasa 14

## MAKALA:



**Kura yapigwa kumruhusuel Sissi kutawala hadi 2030**

Ukurasa 17


# siasa

JUMATANO APRILI 24, 2019

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




Ukurasa 19

**Wabunge Democratic wagwaya kuwasha moto dhidi ya Trump**

FUNZO KWA AFRIKA, DUNIA

# Ni pale mchekeshaji anapomshinda rais uchaguzini

**Na Anil Kija**

UPO msemo kuwa 'hayawi hayawi, huwa', na sasa imetokea barani Ulaya ambako nchini Ukraine mchekeshaji wa luninga, aliyezoea kufamya mizaha kuhusu rais au akijifanya rais katika burudani, ameitwaa nafasi hiyo katika uhalisia baada ya kumshinda rais aliyeko madarakani.

Volodymyr Zelenskiy alikuwa akitabasamu na kutoa ishara za V (alama ya ushindi) ambayo imeacha dunia mdomo wazi, kushinda duru ya pili ya kura ya urais nchini humo.

Mchekeshaji huyo amekuwa akikosoa rushwa kwa nguvu katika nafasi hiyo ya 'urais' kwenye luninga, kumbe ikageuka kuwa maandalizi ya kuwaambia watu kuwa ana uwezo halisi kupambana na rushwa.

INAENDELEA UK.16



Kiongozi wa chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe. PICHA: MTANDAO

**Amerika ya Kusini kupeleka marais wastaafu rumande** Ukurasa 20

UCHAMBUZI

# Sudan 'itakavyoishi' bila Al Bashir



Jenerali Omar al Bashir. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mashaka Mgeta**

ALIYEKUWA Rais wa Sudan kwa takribani miaka 30, Omar al Bashir ameondolewa madarakani na jeshi la nchi hiyo limeshika hatamu.

Hatua hiyo ilitokana na maandamano ya muda mrefu yaliyounganisha nguvu ya umma wa Sudan. Hapakuwa na namna nyingine zaidi ya Al Bashir kuondolewa Ikulu.

Aliingia madarakani mwaka 1989 kupitia mapinduzi ya kijeshi na miaka 30 baadaye, yaani Aprili 11 mwaka huu, aliondolewa madarakani na jeshi la nchi hiyo kutwaa madaraka.

Baada ya kuingia madarakani kwa mapinduzi ya kijeshi, Al Bashiri alichaguliwa kwa njia ya kidemokrasia kuwa Rais wa kiraia mwaka 2011.

Kumbukumbu zinaonyesha kuwa safari ya Al Bashir kuingia Ikulu ya Khartoum kwa mara ya kwanza haikuwa rahisi, kwa vile taifa hilo lilikuwa limegubikwa na mapigano ya wenyewe kwa wenyewe yaliyodumu kwa miaka 21, wakati huo ikiwa ni kati ya Sudan Kaskazini na Sudan Kusini.

Al Bashir alituhumiwa na Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu wa Jinai (ICC) kwa kupanga uhalifu wa kivita na uhalifu dhidi ya binadamu katika eneo la Darfur.

Lakini kama vile kusudio hilo halikuwagusa raia wa nchi hiyo, Al Bashir alishinda Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 na ule wa 2015 ambao hata hivyo wapinzani waliususia.

> "Jumamosi iliyopita, Mratibu Mkuu wa maandamano hayo aliwaasa waendelee kuandamana ili kudai serikali ya kiraia ikiwa ni baada ya aliyekuwa Waziri wa Ulinzi, Awad Ibn Auf kujiuzulu.

Ushindi wa Al Bashir haukuwa na maana dhidi ya kusudio la ICC kwa vile hakuweza kusafiri nje mara kadhaa, akihofia kukamatwa.

Alifanikiwa kufanya ziara ya kidiplomasia katika nchi za Misri, Saudi Arabia na Afrika Kusini ambapo aliondoka ghafla Juni, 15 baada ya Mahakama kuhoji uwepo wake nchini humo na kuamuru akamatwe.

Baadhi ya tuhuma za ICC dhidi ya Al-Bashir ni pamoja na mauaji ya kimbari ya watu wa jamii ya Fur, Masalit na Zaghawa na kuwasababishia mfadhaiko mkubwa wa kimwili na kiakili, kuwaweka katika hali ngumu kwa kuwaharibia makazi yao.

Nyingine ni kushambulia raia katika jimbo la Darfur na kuiba mali katika miji na vijiji.

**BAADA YA KUNDOKA MADARAKANI**

Waandamanaji nchini humo wamehakikishiwa usalama wakati waliokuwa wafuasi wa Al Bashiri katika utawala wake wakiripotiwa 'kutiwa nguvuni.'

Shirika la habari za Reuters liliripoti mwanzoni mwa wiki iliyopita kuwa waliokuwa viongozi katika utawala wa Al Bashir wamekamatwa kwa amri ya Baraza la Mpito la Uongozi wa Kijeshi nchini humo.

Hata hivyo, taarifa hiyo ilieleza kutokuwapo sababu zilizowekwa wazi za kukamatwa kwa watu hao wala kutajwa majina na nyadhifa walizokuwa wanazishikilia.

Wakati hali ikiwa hivyo, Al-Bashir mwenyewe anaripotiwa kuwekwa kwenye kizuizi kwa matarajio ya kushtakiwa nchini humo.

**NGUVU YA UMMA ILIVYOTUMIKA**

Waandamanaji wamezidi kuwa na nguvu nchini humo kiasi cha kuwazuia askari waliokuwa wanataka kuondoa vizuizi walivyoweka barabarani, wakishinikiza kutekelezwa kwa matakwa yao.

Kutokana na 'u-ngangari' wa waandamanaji hao, askari waliokuwa kwenye magari ya kijeshi walilazimika kuomba msaada kwa raia, wengine wakisikika wakisema "tunaomba tusaidiane sote."

Maandamano yaliyofanyika nchini humo hadi kufika Makao Makuu ya Jeshi la nchi hiyo jijini Khartoum, yaliwezesha kuondolewa madarakani kwa Al Bashir madarakani, hivyo kufuta kipindi cha miaka 30 ya utawala wake.

**WAAPA KUENDELEZA MAANDAMANO**

Waandamanaji hao wameapa kuendelea na mpango huo hadi jeshi la nchi hiyo litakapokabidhi madaraka kwa serikali ya mpito ya kiraia.

Lakini shirika la habari za Aljazeera liliripoti taarifa za kuwa jeshi hilo lililotoa fursa kwa viongozi wanaoratibu maandamano hayo kulitangaza jina la Waziri Mkuu atakayesimamia mchakato wa kuelekea kumpata mrithi wa Al Bashir kupitia uchaguzi wa kidemokrasia.

Mwandishi wa Habari wa Al Jaseera, Hiba Morgan, aliripoti kuwa pamoja na kuwa tayari kuachia 'serikali ya mpito' kwa raia, jeshi la nchi hiyo limehitajika kuachiwa wizara za ulinzi na ile ya mambo ya ndani, ili kufanikisha kuwapo kwa amani na usalama.

**VYAMA VYA SIASA VYAGAWANYIKA**

Vyama vya siasa vinadaiwa kugawanyika, vikiwamo vinavyotaka serikali ya mpito kupewa miaka miwili wakati vingine vikihitaji kuwa miaka minne.

Pia mkanganyiko kwa vyama hivyo upo katika hoja ya namna ya kushughulikia masuala ya intelejinsia na usalama wa taifa. Wapo wanaotaka mfumo uliopo uondolewe kabisa na wengine wanataka ufanyiwe maboresho.

Kiongozi wa Kijeshi anayeiongoza Sudan baada ya kuangushwa kwa Al Bashir, Luteni Jenerali Abdel Fattah al-Burhan Abdelrahman, ameelezea nia na utayari wake wa kuzungumza na waandamanaji.

Luteni Jenerali Abdelrahman, alikuwa anashikilia nafasi ya tatu ya juu kwenye jeshi la Sudan na kuwa mtu anayefahamika sana kwa raia wa nchi hiyo.

Aliongoza jeshi la ardhini la Sudan lililopigana kwenye vita vya Yemen na anasadikiwa kuwa swahiba wa maofisa wa majeshi yaliyopo kwenye ukanda wa Ghuba.

Akizungumza kwa njia ya runinga kwa mara kwanza baada ya kutwaa `madaraka' hayo, Luteni Jenerali Abdelrahman alieleza kusitisha makatazo yaliyotolewa na Al Bashir ikiwamo kuwaondoa gerezani wafungwa wa kisiasa waliofungwa kwa mujibu wa sheria ya hali ya hatari.

Vikundi vinavyounda muungano wa waandamanaji vimeitikia rai ya kuzungumza na Luteni Jenerali Abdelrahman kwa matarajio ya kukutana mwishoni mwa wiki iliyopita kujadili namna bora ya kuipata serikali ya mpito ya kiraia.

Jumamosi iliyopita, Mratibu Mkuu wa maandamano hayo aliwaasa waendelee kuandamana ili kudai serikali ya kiraia ikiwa ni baada ya aliyekuwa Waziri wa Ulinzi, Awad Ibn Auf kujiuzulu.

Na aliyekuwa Mkuu wa Usalama nchini humo, Salah Abdallah Mohamed Saleh, maarufu kama Salah Gosh, alijiuzulu siku moja baada ya kujiuzulu kwa Auf.

Chama cha Wanataaluma wa Sudan (SPA) kinachoongoza maandamano ya kudai serikali ya mpito ya kiraia, kimetaka kuendelea kufanyika kwa maandamano.

Kabla ya kujiuzulu kwake, Auf alitangaza kwa njia ya runinga kwamba Luteni Jenerali Abdelrahman atakuwa kiongozi mpya wa baraza la kijeshi la uongozi wa mpito na Katibu Mkuu Kiongozi, Kamal Abdelmarouf al-Mahi kuwa Naibu wake.

"Kilichotokea kinaonyesha tupo katika mwelekezo mzuri na wenye kukidhi maslahi ya umma, sasa tunakaribia kwenye ushindi," anasema Rashid Saeed, Msemaji wa SPA alipokuwa akizungumza na Reuters.

***Makala haya yameandikwa kwa msaada wa vyanzo mbalimbali. Mawasiliano 0754691540 ama barua pepe:mgeta2000@yahoo.com***

MAKALA

# ACT- Wazalendo na utabiri wa kuzoa viti serikali za mitaa

Na Sabato Kasika

CHAMA cha ACT Wazalendo kimesema kwa jinsi ambavyo kinazidi kujipanga vizuri, kwa kuongeza wanachama wapya, kina uhakika wa kutwaa viti vingi katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu.

Katibu Wa Itikadi, Mawasiliano na Uenezi wa chama hicho, Ado Shaibu anasema ACT Wazalendo ilianza kama mchicha na sasa inazidi kupanuka na kupata umaarufu kila kona ya nchi.

"Ujio wa vigogo wa CUF umeongeza nguvu ndani ya chama chetu, kwani kilianza kama mchicha na sasa kinaendelea kujitanua kuwa kikubwa kama mti wa mbuyu," anasema.

Shaibu anafafanua kuwa wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, chama hicho kilikuwa na wanachama 200,000, lakini ghafla mwaka huu kimeongeza wanachama wapya kutoka CUF ambao wanaendelea kujiunga.

"Hatujakusanya takwimu kamili, lakini nina uhakika kwa vuguvugu hili linaloendelea sasa tutakuwa tumeshapata wanachama wapya wengi tu...kwa mfano kule Zanzibar tayari tuna wanachama wapya 125, 000," anasema.

Anabainisha kuwa mamia ya wanachama na wafuasi wa CUF hasa katika visiwa vya Zanzibar wamekuwa wakijiunga na ACT Wazalendo na sasa chama hicho kinaonekana kuwa ngome mpya ya upinzani.

Katibu huyo anasema wanaandaa utaratibu utakaotuwezesha kujua idadi ya wanachama wao nchi nzima na kwamba kwa upande wa Tanzania Bara watakuwa wengi hivyo kuna uwezekano mkubwa kwa chama hicho kupata ushindi katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwishoni mwa mwaka huu.

"Nina uhakika kwa mwendo huu tutatwaa viti vingi katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu, kwani ngome zote za CUF kwa sasa ziko chini ya ACT-Wazalendo,"anasema.

Shaibu anafafanua kwamba chama chao bado kinaendelea kupokea wanachama wengine zaidi, hivyo si rahisi kujua idadi yao mara moja, lakini baadaye watatoa maelekezo kwa viongozi wa chama kwenye mikoa mbalimbali kuhakiki idadi hiyo.

"Baadhi ya wanasiasa wamekuwa wakitubeza eti hatuna lolote, lakini moto wetu wameanza kuona, niwakumbushe tena kwamba tulianza kama mchicha na sasa tunaelekea kuwa mbuyu," anasema.

Anakiri kwamba chama ni wanachama na ndio ambao watakaovutia au kushawishi watu wengine wakiwamo wasio wafuasi wa vyama kukipakura chama hicho ili hatimaye lengo la kushika dola liweze kufanikiwa.




Moja ya mikutano ya Chama cha ACT-Wazalendo. **PICHA: MTANDAO**

> Kwenye suala la itikadi ni kwamba ukija katika siasa za nchi hii kunakosekana itikadi inayoeleweka ndani ya vyama vya siasa....

**KILIKOANZIA**

Katibu huyo anasema chama hicho kilianzishwa na kupata usajili wa kudumu Mei 5 mwaka 2014 na kisha kikashiriki katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 na kufanikiwa kupata madiwani 42 na mbunge mmoja.

Shaibu anasema chama hicho kilianzishwa na wapenzi wa demokrasia ya kweli inayoanzia ndani ya chama, uwazi, uwajibikaji na siasa safi baada ya kuvikosa vitu hivi kwenye vyama vyao vya awali.

"Kuzaliwa kwa ACT- Wazalendo ni mfano wa mto uliochota maji kwenye mikondo miwili kwani kundi la kwanza la waanzilishi wa chama lilitoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) wakiwa ni sehemu kubwa waliokuwa wanamuunga mkono Zitto Kabwe," anasema.

Anafafanua kuwa wengine ni waliokuwa viongozi wa chama cha Alliance for Democratic Change (ADC) ambao chimbuko lao la asili ni waliokuwa wafuasi wa Hamad Rashid ndani ya Chama cha Wananchi (CUF) na kwamba makundi hayo miwili yaliungana na kuanzisha chama cha ACT- Tanzania ambacho baadaye kilibadilishwa jina na kuitwa ACT- Wazalendo.

"Viongozi na wanachama wengi wa awali wa ACT- Wazalendo ni waathirika wa vitendo vya ukiukwaji na uminywaji wa demokrasia ndani ya vyama vyao vya awali," anasema.

Anasema hata hao wapya wanaoendelea kumiminika katika chama hicho nao wamekumbwa na hali hiyo, na kwamba kwa kukimbilia kwao huko, wameshusha tanga na kupandisha tanga, harakati za kisiasa zinaendelea.

"ACT- Wazalendo kilianzishwa ili kiwe chama mbadala wa uhakika wa siasa safi iliyokosekana kwingineko na kwamba ndivyo kilivyo na kitaendelea kuwa hivyo," anasema na kuongeza:

"Aidha, ACT-Wazalendo kilianzishwa ili kuwavutia wale ambao kwa miaka mingi hawajawahi kutamani kuwa wanachama wa vyama vya siasa kwa kuogopa ubabaishaji uliotamalaki kwenye vyama vingi."

Shaibu anasema wingi wa wanachama wapya wanaomiminika katika chama chao ni dalili tosha kwamba huku ndiko kwenye kimbilio lao, hivyo wapinzani wao watarajie kuona wakihenyeshwa kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa.

**UWAZI NA UWAJIBIKAJI**

Ni eneo jingine ambalo Shaibu anasema chama hicho kinajipambanua wazi.

Kwamba chama hicho ni cha uwazi na alama yake kuu ni mkono wenye vidole vilivyoachwa wazi kuashiria uwazi.

"Kwenye suala la itikadi ni kwamba ukija katika siasa za nchi hii kunakosekana itikadi inayoeleweka ndani ya vyama vya siasa.... ACT Wazalendo kiliasisiwa ili kuziba ombwe hilo," anasema.

Anabainisha wanachama wanaomiminika katika chama hicho kwa sasa, hawajakosea, kwa madai kwamba wameona ACT- Wazalendo ndilo kimbilio lao kwa siasa za Tanzania.

"Kuhusu demokrasia, kama nilivyosema awali ni kwamba viongozi na wanachama wengi wa awali wa ACT- Wazalendo ni waathirika wa vitendo vya ukiukwaji na uminywaji wa demokrasia ndani ya vyama vyao vya awali, huku tunafanya kila kitu kwa uwazi," anasema.

Anafafanua kuzaliwa kwa chama hicho ni zao la mapambano yenye sura tatu, yaani mapambano ya demokrasia, mapambano ya uwazi na uwajibikaji na mapambano ya kiitikadi.

MAKALA

# Ni pale mchekeshaji Ukraine anapomshinda rais uchaguzini

INATOKA UK.13

Waangalizi wa uchaguzi kutoka Jumuiya ya Usalama na Ushirikiano barani Ulaya walisifu kiwango cha uwazi katika upigaji kura duru hiyo ya pili, kukamilisha uhamishaji wa madaraka kidemokrasia na kwa amani.

Taarifa za vyombo vya habari zinasema kuwa rais mpya wa Ukraine hajawahi kushika nafasi yoyote ya mamlaka na alikuwa akiigiza katika burudani ya mwalimu wa shule aliyechaguliwa kuwa rais kumbe alikuwa anafuatilia ndoto yake yeye mwenyewe.

Hapakuwa na malalamiko yoyote kuhusu uchaguzi huo ulivyokwenda, licha ya kuwa rais aliyeko madarakani alikuwa hatarini kupoteza kiti; Ukraine inataka kuthibitisha ni nchi ya Magharibi.

Wakati kuhesabu kukielekea ukingoni katika duru ya pili ya uchaguzi, Zelenskiy alikuwa amepata asilimia 73 ya kura zote, akimshinda Rais Petro Poroshenki aliyekuwa akitaka muhula wa pili.

Msemaji wa Rais Vladimir Putin wa Russia, alitoa taarifa kuwa ilikuwa mapema mno kumpongeza Volodymyr Zelenskiy kwa kushinda uchaguzi wa rais nchini Ukraine, akisema kuwa ushindi huo ni chaguo la wapigakura wa Ukraine.

Kwa vile mchekeshaji huyo ametokea jamii ya Ukraine inayozungumza lugha ya Kirusi, bado ni mapema mno kuzungumzia uwezekano wa kukuza ushirikiano kati ya Russia na Ukraine, akiingia madarakani.

Russia inangoja hatua za kwanza za mchekeshaji hiyo asiye na uzoefu katika siasa, ikitazamia atajielekeza zaidi huko.

Rais Donald Trump wa Marekani alikuwamo kati ya waliotangulia kutambua ushindi hupo, taarifa ya Ikulu ikilenga kusisitiza kufanyika uchaguzi wa kidemokrasia na wa amani, akisisitiza kuhusu kuunga mkono uhuru wa Ukraine na uthabiti wa mipaka yake.

Ni hisia inayoelekezwa kwa Russia ambayo imetwaa Crimea kutoka Ukraine kuwa sehemu ya Russia, ambako wakazi wengi wanazungumza Kirusi.

Ilikuwa ni baada ya kura ya maoni ya hatma ya jimbo hilo.

Hata hivyo, hatua hiyo ilisababisha Russia kuwekewa vikwazo na nchi za Magharibi, ambavyo haielekei kuwa vitaondolewa hivi karibuni. Ni ushindani kati ya Russia na ukanda wa Magharibi, kwa itikadi ya uzalendo.

Katika taarifa fupi kupitia kwa msemaji wake, Trump alieleza utayari wake wa kushirikiana na Zelenskiy kufanya mabadiliko yanayojenga demokrasia, kuongeza ustawi nchini na kung'oa kabisa ufisadi.

Ili kuonyesha athari ya kisaikolojia ya ushindi huo kote Ukraine, gavana wa jimbo moja tu ambako Zelenskiy hakupata wingi wa kura katika uchaguzi huo wa rais alijiuzulu. Ufaransa na Ujerumani pia zilieleza kuridhishwa kwao na jinsi uchaguzi ulivyofanyika, wakisisitiza pia kuhusu mabadiliko na uthabiti wa mipaka ya Ukraine.



Rais Mteule wa Ukraine,Volodymyr Zelenskiy.

> Russia inangoja hatua za kwanza za mchekeshaji hiyo asiye na uzoefu katika siasa, ikitazamia atajielekeza zaidi huko.

Rais Emmanuel Macron wa Ufaransa alikwenda mbali akagusia juhudi za Ufaransa na Ujerumani kupata suluhu ya mzozo kati ya Ukraine na Russia, hasa kuhusiana na jimbo la Mashariki ambalo pia linataka kujitenga, kama Crimea awali.

Kutokana na mvutano usioisha kati ya Ukraine na Russia kuhusu mustakabali wa wanaozungumza Kirusi huko Ukraine, kuchaguliwa kwa mmoja kati yao kumeinua matumaini ya mzozo huo kuondolewa kwa amani, kwa diplomasia. Kansela Angela Merkel wa Ujerumani alieleza dhamira yake ya kuona Ukraine ikijikwamua na mizozo ya uongozi kuhusiana na wanaozungumza lugha ya Kirusi.

Wachunguzi wanasema kuna makubaliano yalifikiwa mwaka 2015 kuweka amani kati ya Ukraine na 'Russia kuacha mapigano, lakini hakuna makubaliano yoyote yaliyofikiwa kati ya nchi hizo nne - Russia, Ukraine halafu pia Ujerumani na Ufaransa kwa pamoja.

Kansela Merkel alisitiza zaidi mageuzi katika mifumo ya mahakama, kugatua mamlaka nchini huko na kupambana na rushwa, wakati wakuu wa Sekretariat ya Umoja wa Ulaya jijini Brussels huko Ubelgiji hawakubaki kimya.

Mwenyekiti wa Tume ya Ulaya, Jean-Claude Juncker na mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri la umoja huo, Donald Tusk, walisema mtawala huyo mpya asiye na uzoefu katika siasa "anaweza kutazamia kuendelea kuungwa mkono kwa dhati na Umoja wa Ulaya (EU) kuthibitisha uhuru wa Ukraine, kujiamulia mambo yake yenyewe na uthabiti wa mipaka yake."

Kimsingi Ulaya imefurahishwa na matokeo ya uchaguzi huo wakati furaha ya Russia ni ndogo, kuwa anaongea Kirusi hivyo wanaweza kuzungumza naye, ila hawapendi sera zake.

Salamu za viongozi wa EU zilikuwa kama mtiririko wa vipaumbele ambavyo serikali mpya ya Ukraine ikiongozwa na aliyekuwa mchekeshaji katika luninga inatazamiwa kufuata, hasa kuzingania mwelekeo wa mageuzi ya kisiasa na kiuchumi.

Juncker na Tusk walisisitiza kubaki katika mwelekeo wa mageuzi, ikiwa ni pamoja na kuimarisha utawala wa sheria, kupambana na rushwa, kusimamia uthabiti wa soko la fedha na kuendeleza mabadiliko ya msingi katika sekta ya nishati.

Walisema kuendelea kutekelezwa kwa mkataba wa ushirikiano (kama mwanachama mshirika wa umoja huo) kutachangia kwa kiasi kikubwa kufikia azma hiyo.

Wachambuzi wa habari wanasema kuwa kitakachomsaidia Zelenskiy kuleta mageuzi ni wingi wa kura alizopata katika duru ya pili ya uchaguzi.

Kuwa raia wa Ukraine wa jamii ya wanaozungumza Kirusi itampa pia uwezo wa kujadiliana na wale wanaotaka kujitenga kutokana na uhusiano wa lugha ya utamaduni na taifa kubwa la Russia.

Suala linaloelekea kuleta shida litakuwa kurudisha eneo la Mashariki ya Ukraine katika serikali kuu, kwani liko chini ya makundi yenye silaha yasiyokuwa na utii kwa serikali ya 'kimagharibi' ya Poroshenko.

Ni kama ilivyo hapa nchini kuwa mwelekeo wa kijamaa unaleta msisitizo wa lugha ya Kiswahili, soko huria likizaa 'kimombo.'

Kuchaguliwa kwa Zelenskiy kutaifadhaisha kwa kiasi fulani Russia katika kufuatia sera zake za kujenga upya mahusiano na wakazi wa nchi za iliyokuwa Urusi wanaozungumza lugha hiyo ambao sasa ni nchi tofauti.

Juhudi hizo ni pamoja na kuchochea viwango vya nini kifanyike katika eneo lenye Warusi wengi vinginevyo wajitoe, wawe huru na wawakaribie ndugu zao wa Russia.

Ni hisia inayotegemea zaidi kutokuwa na matumaini katika mazingira yaliyopo, ambako kuna mgawanyiko kati ya wanaotoka 'Ukraine ya jadi' na wale 'wakuja.' Jitihada ya Russia kujihalalisha katika kuwatenga wazumgumzaji Kirusi na nchi walizopo watapata pigo kubwa.



Rais wa Ukraine aliyeshindwa Petro Poroshenko. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

MISRI



Rais Abdel-Fatah el-Sissi

## Kura yapigwa kumruhusu el Sissi kutawala hadi 2030

WAMISRI wameyapigia kura mabadiliko ya katiba yatakayomruhusu Rais Abdel-Fatah el-Sissi abakie madarakani hadi mwaka 2030.

Mabadiliko hayo yatalizidishia nguvu jeshi na kupiga hatua ya ziada kuelekea kwenye utawala wa kiimla.

Kura hiyo ya maoni inaitishwa huku wakosoaji wakiandamwa kwa nguvu kupita kiasi.

Serikali ya el-Sissi imekamata maelfu ya watu, wengi wao ni wafuasi wa itikadi kali ingawa kuna wanaharakati wa kawaida ambao pia wamekamatwa kwa namna hiyo hiyo na hivyo kurejesha nyuma uhuru uliopatikana kutokana na vuguvugu la mwaka 2011 la kudai demokrasia.

Zoezi la kupiga kura lililoanza Aprili 20 lilitarajiwa kuwa la siku tatu ili kuwawezesha wapigakura kutoa sauti zao na limemalizika juzi.

Katika kipindi chote cha upigaji kura, kulikuwa na ulinzi mkali wa polisi na vikosi vya usalama.

Haja Khadija, bibi wa miaka 63, na mmoja wa walioshiriki katika kura hiyo anasema alishiriki katika shughuli hiyo kwa sababu ya 'usalama na utulivu' wa nchi.

"Tunampenda el-Sissi... amefanya mengi...ametuongezea malipo ya uzeeni," anasema.

Hata hivyo, sauti za upande wa upinzani zimenyamazishwa kutokana na jinsi kura hiyo ya maoni ilivyoitishwa kwa pupa.

Vyombo vya habari vinavyoelemea upande wa serikali vimekuwa vikifanya kampeni zao tangu wiki kadhaa na kuitaja 'kura ya ndio kuwa ni wajibu wa kitaifa.'

### UPINZANI HAUKURUHUSIWA KUENDESHA KAMPENI

Kuanzia mwanzoni mwa mwezi huu, jiji la Cairo lilijaa mabango na maandishi yanayowahimiza wapigakura waunge mkono mageuzi.

Mabango mengi yanasemekana yamegharamiwa na vyama vinavyoiunga mkono serikali, wafanyabiashara na wabunge.

Bunge linalodhibitiwa na wafuasi wa el-Sissi limeunga mkono kwa wingi mageuzi hayo wiki iliyopita.

Sauti 22 tu ndizo zilizopinga na moja kutoelemea upande wowote kutoka jumla ya wabunge 554 waliohudhuria kikao hicho.

Siku ya pili yake tume ya uchaguzi ikatangaza shughuli ya kupiga kura ambayo tayari imemalizika.

Mageuzi yanayotarajiwa yanatajwa na wakosoaji kuwa hatua ya ziada kuelekea utawala wa kimabavu.

Kura ya maoni inafanyika miaka minane baada ya vuguvugu la kudai demokrasia kumaliza utawala wa miongo mitatu wa Hosni Mubarak.

Lakini pia ikiwa ni miaka karibu sita baada ya el-Sissi kuongoza mapinduzi ya kijeshi yaliyomng'oa madarakani rais wa kwanza aliyechaguliwa kidemokrasia, mfuasi wa itikadi kali Mohammed Mursi.

Makundi mawili ya kimataifa, Human Rights Watch na halmashauri ya kimataifa ya wanasheria yameihimiza serikali ya Misri ibatilishe mageuzi hayo.

Kongamano la vyama vya kiliberali vinavyoelemea mrengo wa kushoto liliwahimiza Wamisri kuteremka kwa wingi vituoni ili kupiga kura ya 'hapana' dhidi ya mageuzi hayo.

Kongamano hilo linasema linatumia mtandao wa kijamii kueneza wito huo kwasababu limekatazwa kutundika mabango.

Mageuzi hayo yanarefusha muhula wa rais kutoka miaka minne hadi sita na kumruhusu atawale kwa mihula isiyopindukia miwili. **DW**

TUJIKUMBUSHE

# JENERALI YAKUBU GOWON

• Kiongozi wa tatu wa taifa la Nigeria, aliyeongoza kati ya mwaka 1966-1975

**Na Raphael Kibiriti**

KATIKA safu hii ya TUJIKUMBUSHE kwa leo tunawaletea moja ya majenerali maarufu wa Jeshi la Nigeria, waliowahi kuongoza taifa hilo lenye idadi kubwa ya watu barani Afrika, lakini pia likiwa na historia ya aina yake katika uga wa kisiasa.

Tunayemwangalia leo ni Jenerali Yakubu Gowon ambaye alizaliwa Oktoba 19, mwaka 1934. Alikuwa kiongozi mkuu wa serikali ya Shirikisho iliyoongozwa na Jeshi la Nigeria, kuanzia mwaka 1966 hadi mwaka 1975.

Aliingia madarakani, baada ya kufanya mapinduzi ya kijeshi dhidi ya serikali iliyokuwa ikiongozwa na Johnson Aguiyi-Ironsi, ingawa naye alipinduliwa na jeshi baadaye.

Wakati wa utawala wake, serikali ya Nigeria, ilifanikiwa kusitisha vita vya wenyewe kwa wenyewe katika eneo la Biafra, ambavyo vilipiganwa kuanzia mwaka 1967 hadi 1970.



Jenerali Yakubu Gowon

### MAISHA YAKE

Gowon ni wa kabila la Ngas (Angas) kutoka Lur, kitongoji kidogo kilicho chini ya serikali ya mitaa ya Kanke katika Jimbo la 'Plateau'.

Wazazi wake, walihamia Wusasa, mji ulioko eneo la Zaria, wakiwa watumishi wa Kanisa la Mtume 'Church Missionary Society' (CMS), Gowon akiwa bado mdogo.

Baba yake alijawa na faraja, baada ya kugundua kuwa alimwoa mama yake Gowon ikiwa ni siku hiyo hiyo aliyoolewa aliyekuwa Malkia mtarajiwa Elizabeth wa Uingereza na Mfalme mtarajiwa King George VI.

Jenerali huyo ni mzaliwa wa sita kati ya watoto 11 na alipata malezi ya awali akiwa eneo la Zaria, ambako ndiko alikopata elimu yake ya msingi.

Akiwa shuleni, Gowon alipenda michezo... alikuwa mwanariadha mzuri wa mbio ndefu na golikipa wa kutegemewa kwenye timu ya mpira wa miguu shuleni kwao.

Aidha, alikuwa mrusha mkuki wa kutegemewa. Aliwahi kuvunja rekodi ya kukimbia umbali wa maili moja, akiwa mwaka wa kwanza wa masomo yake ya chuo kikuu, huku akiwa kiongozi wa mchezo wa ngumi.

### SIASA

Gowon alijiunga na Jeshi la Nigeria mwaka 1954. Ilipofika Oktoba 19, 1955, alifanikiwa kupata kamisheni ndani ya Jeshi hilo katika cheo cha Luteni Usu, siku ambayo ilikuwa pia ni sherehe ya kutimiza miaka 21 ya kuzaliwa kwake.

Alihudhuria mafunzo ya kijeshi katika Chuo cha Unadhimu cha Kijeshi cha Sandhurst nchini Uingereza, kati ya mwaka 1955 na 1956, na mafunzo mengine ya kijeshi mwaka 1962 katika Chuo cha Camberley, halafu akachukua kozi ya unadhimu katika Chuo cha 'Joint Staff', mwaka 1965, humohumo Uingereza.

> Jenerali huyo ni mzaliwa wa sita kati ya watoto 11 na alipata malezi ya awali akiwa eneo la Zaria, ambako ndiko alikopata elimu yake ya msingi.

### OPERESHENI ZA ULINZI WA AMANI

Alishiriki katika operesheni ya Walinzi wa Amani wa Umoja wa Mataifa waliokuwepo Congo (sasa DRC), katika awamu zote mbili kuanzia mwaka 1960 hadi mwaka 1961, na nyingine ya mwaka 1963.

Aliendelea kupata madaraka jeshini, ambako mwaka 1966, alikuwa Mkuu wa Kikosi, akiwa na cheo cha Luteni Kanali.

Kipindi chote hiki Gowon hakujihusisha kwa hali yoyote na masuala ya siasa, hadi nchi hiyo ilipoanza kukumbwa na ghasia na kelele hasi zilizomlazimisha ajiingize katika majukumu ya kiuongozi.

Alikuwa mtu asiyefungamana na upande wa makabila ya Hausa na Fulani, na hakuweka mbele uzawa na itikadi za kiimani.

Msimamo wake huo ulimsaidia kuaminika na ikawa rahisi kwake kuchaguliwa katika ngazi za juu za uongozi katika taifa hilo lililokuwa katika mgawanyiko na mvutano mkubwa wa u-dini na u-kabila wakati huo.

### AWA MNADHIMU MKUU

Ilipofika Januari 1966, aliteuliwa kuwa Mnadhimu Mkuu wa Jeshi la nchi hiyo, akiwa na umri mdogo wa miaka 32.

Hali hiyo ilijitokeza kufuatia mapinduzi ya kijeshi yaliyofanikishwa na wanajeshi wa vyeo vya chini, wengi wao wakiwa wa kabila la Igbo, chini ya uongozi wa Meja Chukwuma Kaduna Nzeogwu, ambaye ndiye hasa aliyefanikisha kuiangusha serikali ya kiraia.

Wakati wa harakati za mapinduzi hayo, viongozi wengi waliokuwa na asili ya Kaskazini na Magharibi waliuawa, wakiwemo Sir Abubakar Tafawa Balewa na Waziri Mkuu Sir Ahmadu Bello.

Wengine ni Sardauna wa Sokoto aliyekuwa Waziri Mkuu wa eneo la Kaskazini, pamoja na Samuel Akintola, aliyekuwa Waziri Mkuu wa Jimbo la Magharibi.

Aidha, waliuawa Luteni Kanali Arthur Unegbe na viongozi wengine.

Wakati mapinduzi haya yakifanyika, ndicho kipindi ambacho Luteni Kanali Gowon kwa wakati huo alikuwa ametoka kurejea kutoka Ulaya alikokuwa amekwenda kwenye mafunzo ya kijeshi.

Inaaminika kuwa aliingizwa katika orodha ya waliopanga mapinduzi hayo ya kijeshi.

### SABABU ZA MAPINDUZI

Kwanza ilikuwa ni kukosekana kwa mwakilishi kutoka Kaskazini kwenye uongozi wa kitaifa katika karne ya 20.

Hilo lilikuwa ni doa kwani kwa mara ya mwisho mtu kutoka Kaskazini kuingia katika uongozi wa kitaifa ilikuwa ni mwaka 1919.

Mapinduzi hayo yalichagizwa pia na kushindwa kwa Meja Jenerali Johnson Aguiyi-Ironsi (ambaye alikuwa mkuu wa nchi wakati wa mapinduzi ya Januari 1966), kutanzua madai na malalamiko ya wananchi wa Kaskazini.

### MCHANGO VITA VYA BIAFRA

Akitegemea kuwa eneo la Biafra lingejitenga, Gowon alichukua hatua za haraka kudhohofisha ngome ya msaada ya eneo hilo kwa kutoa Amri ya Rais ya kuundwa kwa majimbo mapya 12 kuchukua nafasi ya manne yaliyokuwapo.

Sita miongoni mwa majimbo hayo mapya yalijumulisha makundi ya wachache ambayo yalikuwa yakipigania kuundwa kwa majimbo kutoka miaka ya 1950.

Mahesabu ya Jenerali Gowon yalikuwa sahihi kwamba wachache kutoka eneo la Mashariki wasingewaunga mkono watu wa kabila la Igbos, ikichukuliwa kuwa matarajio yao ya kuwa na majimbo yao binafsi iwapo juhudi zao za kujiondoa kutoka katika Shirikisho la Nigeria zingeshindwa.

Mengi ya majeshi ya shirikisho yaliyopigana katika Vita vya Kiraia vya Nigeria, pia vikijulikana kama Vita vya Biafra kulirejesha eneo la Mashariki ndani ya Shirikisho, yalikuwa yanatoka kwenye makabila ya wachache.

Vita hivyo vilidumu kwa miezi 30 na vikamalizika Januari 1970. Kwa kukubali kumalizka kwa vita vya Biafra bila ya masharti yoyote, Jenerali Gowon alitangaza kwamba hakungekuwa na mshindi wala mshindwa, wala uhasama.

Katika moyo huo huo, miaka iliyofuata ilitangazwa kuwa kipindi cha ukarabati, Ujenzi na upatanisho.

Kupanda kwa bei ya mafuta kulikoanza kama matokeo ya bei kubwa ya mafuta ghafi, eneo ambalo lilikuwa ndiyo chanzo kikubwa cha mapato ya nchi hiyo katika soko la dunia mwaka 1973, kuliongeza uwezo wa serikali ya shirikisho kukamilisha miradi yote iliyohusiana na ukarabati, ujenzi na upatanisho.

### MAZONGE KUFUATIA VITA VYA BIAFRA

Kuliibuka uhasama kati ya mikoa ya Mashariki na Serikali ya Shirikisho iliyokuwa ikitawaliwa na watu kutoka Kaskazini, chini ya Jenerali Gowon.

Mnamo Januari 4-5, mwaka 1967, kwa mujibu wa matakwa ya Chukwuemeka Odumegwu Ojukwu, Gavana wa eneo lililotoka kujitenga la Biafra ya kukutana ili kuzungumza, mkutano uliohudhuriwa na Jenerali Gowon, Ojukwu ma wajumbe wengine wa Baraza Kuu la Kijeshi ulifanyika Aburi nchini Ghana.

Mkutano huo ulirejea kusudio la kumaliza vita vyote na kuifanya Nigeria kama nchi inayoundwa na mikoa.

Matokeo ya mkutano huo ni kupatikana kwa Azimio la Aburi.

ITAENDELEA

KIMATAIFA

# Wabunge Democratic wagwaya kuwasha moto dhidi ya Trump

**Na John Kimbute**

VIONGOZI wa chama chenye wajumbe wengi katika Baraza la Wawakilishi nchini Marekani, wanaangalia kwa tahadhari kubwa uwezekano wa kuanza mchakato wa kupigiwa kura ya kutokuwa na imani na Rais Donald Trump.

Hatua hiyo inafikiwa endapo baraza hilo likishirikiana na Senate linakuwa na wingi wa kura kukubali hisia au mwelekeo wa kisheria kuwa rais aliyeko madarakani alitumia mamlaka yake kuzuia ukweli usipatikane kuhusu kuingilia kwa Russia katika uchaguzi mkuu wa Marekani mwaka 2016.

Ripoti ya mwendesha mashtaka maalum Robert Mueller, ilithibitisha kuwa kampeni ya Trump haikushirikiana na Russia, ila aliwakingia kifua.

Rais Trump amekuwa akifukuza maofisa wa ngazi za juu Ikulu kwa kupuuzia maelekezo yake kuhusu nini cha kufanya kwa suala hilo, akiwamo mwendesha mashtaka huyo ambaye aliwekwa katika nafasi hiyo baada ya kuondolewa kwa aliyekuwa mkuu wa Shirika la Upelelezi la Marekani (FBI), James Comey ,kutokana na kutaka 'kujua sana' wataalamu wa Russia walioingilia uchaguzi walikuwa wanafanya nini, na wakuu wa kampeni ya Trump walijua nini katika suala hilo. Mkurugenzi wa kampeni ya Trump, Paul Manafort, tayari anatumikia kifungo kwa maelezo ya uongo aliyotoa wakati wa kuthibitisha madai ya kuvuruga ushahidi kuhusu kodi na miamala ya kibenki iliyomhusu Trump, akatupwa gerezani na kupoteza leseni yake ya kufanya kazi kama wakili.

Historia na shughuli za Paul Manafort kama mkurugenzi wa kampeni ya Trump hadi mwezi Agosti 2016 ni kielelezo cha mielekeo ya walioko madarakani Marekani hivi sasa.

Manafort alikuwa mshauri na mfagiliaji (lobbyst) kwa wagombea urais wa chama cha Republican kwa miaka mingi, akiwa amewasaidia Gerald Ford, Ronald Reagan, George H.W. Bush na Robert Dole (ambaye alishindwa na Bill Clinton, 1996).

Mwaka 1980 alianzisha kampuni ya uwakala wa kisiasa ya Black, Manafort &Stone (wanasheria) akapata tenda za kusaidia watu kama Ferdinand Marcos wa Ufilipino, Mobutu Seseseko wa iliyokuwa Zaire, na kiongozi wa uasi nchini Angola, Jonas Savimbi kwa malipo manono.

Alijiandikisha kisheria kama wakala wa dola za kigeni Marekani.

Kutolewa kwa ripoti isiyo kamili kuhusu uchunguzi wa uingiliaji huo, licha ya mapengo katika muhtasari alioutoa Mwanasheria Mkuu wa Marekani, William Barr ili kulinda faragha za wahusika tofauti na mahitaji mengine ya kisheria, imezua mikondo ya hisia tofauti kuhusu nini kifanyike.

Wengi kati ya wajumbe wa Democrat katika Baraza la Wawakilishi wanaamini kuwa upo ushahidi wa kutosha kumtundika Trump endapo hoja ya kuandaa azimio la kushtakiwa kwake itapelekwa bungeni (yaani Wawakilishi na Senate, kwa pamoja likiitwa Congress).

Eneo ambalo ushahidi haupingiki ni kuzuia ukweli kujulikana, ambalo Mueller aliashiria kuwa Bunge liangalie.

Hata hivyo, baadhi ya wataalamu wa masuala ya uwakala wa kisiasa na mwelekeo wa wajumbe wa mabaraza yote mawili ya Bunge wanahisi kuwa Democrats wanaweza wakaingia katika mtego endapo wataanza mkakati wa kushtakiwa Trump mbele ya Bunge.

Hoja kama hiyo ikipata kura za kutosha ina maana kuwa rais aliyeko madarakani aachie ngazi ili aweze kushtakiwa, ingawa mara nyingi kujiuzulu kabla ya kushtakiwa inakuwa ni adhabu tosha kwa kilichotokea, na Bunge (Congress) linakuwa halina sababu ya kuendeleza suala hilo tena.

Tatizo ni kuwa wajumbe wa Republican wanaona Trump anafanya kazi nzuri, wasijihatarishe kuanza mkakati.

> Kama wapigakura wa Republican bado wana imani ya kutosha na Trump, wajumbe wao katika Bunge hawataweza kuasi.

Licha ya kuwa mkusanyiko wa ushahidi wa kutaka kuzuia kilichotokea kisiwekwe wazi, bado wachunguzi wa habari wanaona kuna uwezekano wa Rais Trump, pindi mkakati huo ukianza, kujionyesha kama ambaye anasakamwa, licha ya kutokuwapo ushirikiano kati ya kampeni yake na mawakala wa Russia.

Wanasema ataanza tena 'mantra' yake ya uchaguzi mkuu 2016 kuwa 'hii ndiyo nafasi yetu ya mwisho' kurekebisha kila kinachofanywa na wanasiasa wazoefu wa mabaraza yote mawili, hasa wakilengwa Democrats.

Kama wapigakura wa Republican bado wana imani ya kutosha na Trump, wajumbe wao katika Bunge hawataweza kuasi.

Yako maeneo mengine ya kitaaluma kuhusu matokeo ya kuanzisha mkakati wa kushtakiwa Trump bungeni, kuwa wajumbe wa Democrat katika mabaraza hayo ya Congress hadi sasa hawana uwezo wa kushindana na Trump katika kufikisha ujumbe kwa wapigakura.

Wanaweza kuwa na hoja za kutosha kuhusu mwenendo wake kuanzia wakati wa kampeni hadi akiwa madarakani, panga pangua ya washauri Ikulu na maelezo kadhaa yenye utata wakati uchunguzi huo ukiendelea ambako alipelekewa maswali hapa na pale asaidie mwendesha mashtaka maalum kufikia tamati ya mwenendo wa suala hilo. Ambacho hawana uhakika nacho ni jinsi wengi kati ya wapigakura watakavyopokea ujumbe huo kwa upande mmoja, na athari za mashambulizi ya Trump.

Imefikia mahali hali ya kutokujiamini inafanya baadhi ya wataalamu wa masuala ya kampeni wanaosaidia kambi tofauti za watangaza nia upande wa Democratic kujiuliza mara mbili kuhusu uhusiano au mwingiliano kati ya mkakati wa kumshtaki Trump na kuendesha kampeni ya kumshinda uchaguzi mkuu mwakani.

Baadhi yao wanaona wazi kabisa kuwa mjadala kuhusu Trump utafunika sera zao, na kuumiza kampeni zao kwa njia isiyotibika endapo kuelekeza macho na hisia zote kwa Trump kutampa nafasi kujieleza na kuwavuta wapigakura kama alivyofanya 2016.

Wanakiri kuwa hawakutazamia Trump angefikia hatua ya kugombea, ashinde.

Mjadala miongoni mwa wataalamu wanaojaribu kushauri watangaza nia watarajiwa na waliotoa ishara hiyo kwa ajili ya uchaguzi wa rais mwakani unajikanganya kwa hisia tofauti na miparaganyiko ya kimkakati.

Jambo ambalo halina ubishi ni kuwa mkakati wa kumwondoa Trump kwa kumshtaki bungeni siyo lelemama kwa chama cha Democratic, na tatizo siyo tu kupata kura kutoka kwa wajumbe wa Baraza la Senate upande wa Republican, ambako wana wingi wa viti.

Ni pale tu wanapokuwa na uhakika wana ujumbe unaoeleweka kwa wapigakura ndipo wanaweza kuingia katika mkakati wa kumshtaki Trump, lakini uhakika hauwezi kuwapo bila kampeni.

Wataalamu wengine wanang'aka kuwa wanasiasa wa Democratic wameota usugu wa kupoteza nafasi za kujipambanua na kujenga hoja, mkakati wa kuweza kubadili hali ilivyo nchini humo.

Wanaona wazi kabisa kuwa kuna nafasi ya kufanya mashambulizi na kushinda kutokana na uzito wa ushahidi uliopo wa udanganyifu na dhamira mbaya ya Trump katika uchunguzi huo, kiasi kwamba mgombea urais wa Republican uchaguzi wa 2013 (aliyeshindwa na Barack Obama), Mitt Romney, alitoa taarifa kuwa udanganyifu wa Trump unamchefua.

Tatizo ni kuwa katika maeneo mengi wapigakura wa Republican wanaona kuwa anafanya kazi nzuri, na katika medani ya uchumi Marekani inatenda itakavyo katika ulimwengu na hakuna wa kushindana nayo, hali ambayo inahusiana na maamuzi ya Trump.

Amediriki kuvunja miiko na kuzidhoofisha nchi shindani, akamudu vyema.



Spika wa Bunge la Marekani, Nancy Pelosi. **PICHA: MTANDAO**

MAKALA

# Amerika ya Kusini kupeleka marais wastaafu rumande

## • Peru yavuna mabua



Aliyekuwa Rais wa Peru, Alan Garcia. **PICHA: MTANDAO**

**Na Ani Jozeni**

NCHI ya Peru katika bara la Amerika ya Kusini ilitangaza siku tatu za maombolezo ya kitaifa kutokana na kifo cha rais mstaafu Alan Garcia, aliyekuwa na umri wa miaka 69 wakati alipokufa kwa kujipiga risasi.

Taarifa zilisema kuwa polisi walikuwa wanaelekea nyumbani kwake kumkamata ili afunguliwe kesi mahakamani kwa madai ya rushwa.

Kwa wengi kati ya raia wa nchi hiyo Alan Garcia hakuwa mtu wa kawaida, kwani alionyesha kipaji cha siasa akiwa bado mtoto, akatoa hotuba ya kusisimua kumsifu mwanzilishi wa chama cha Aprista ambacho kilimfikisha madarakani baadaye.

Alitawala katika vipindi tofauti, kwanza Julai 1985 hadi Julai 1990 halafu Julai 2006 hadi Julai 2011, kuonyesha kuwa hakuwahi kuchuja katika siasa za Peru, akichaguliwa angali bado kijana.

Kuelewa mazingira ya rais huyo mstaafu kufikia uamuzi huo labda siyo suala gumu kisaikolojia, kuwa hakutaka kuingia katika mazingira ya aibu, lakini kwa vile siyo jambo la ajabu kwa wanasiasa kutuhumiwa kwa rushwa, inawezekana yako maeneo mengine yaliyomtia uchungu, si tuhuma peke yake.

Kwa upande mwingine, nchi aliyoiongoza siyo maskini hata kidogo, kwani kwa takwimu za Benki ya Dunia uchumi wa nchi hiyo ni wa 39 kwa ukubwa duniani, na kipato chake cha wastani ni cha kati ya ngazi za juu, zaidi ya dola za Marekani 12,000 kwa kila mwananchi.

Kimsingi imefuata misingi ya kiliberali ya uchumi ila kuna misuguano hivyo kunakuwapo vipindi tofauti vya mwelekeo wa utawala, vya kutetea uchumi wa ndani (haki za wafanyakazi, kampuni za ndani) na vipindi vya uhafidhina (soko huria, haki ya kila mjasiriamali, wa ndani au nje). Garcia alikuwa kundi la kwanza.

> Mzunguko huo wa tuhuma umeendelea hadi majuzi ambako polisi walitumwa nyumbani kwake kwenda kumkamata, akajiua kwa risasi kabla ya kuingizwa hali ya ufungwa.

Akiwa kijana, Garcia alisoma sheria katika Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Peru, na akapata shahada katika Chuo Kikuu cha San Marcos (Mtakatifu Marko) mwaka 1971.

Aliondoka Peru kwenda Hispania kusoma shahada ya juu (uzamivu) ambayo alisema aliipata lakini ushahidi wa baadaye unaashiria kuwa hakumaliza masomo hayo (sababu mojawapo ni kuwa alikuwa mwanamapinduzi, na enzi hizo Hispania inaongozwa na Jeneralissimo Francisco Franco, mtawala wa kiimla asiyetaka harufu ya mapinduzi hata kwa kilomita moja.

Garcia aliende Ufaransa ambako nyakati hizi fikra za kimapinduzi zilikuwa zinashamiri, akasoma katika chuo kikuu cha Pantheon Sorbonne, moja ya vyuo vikuu vikongwe na vyenye sifa za hali ya juu nchini Ufaransa.

Licha ya kuwa Garcia alikuwa kimsingi ni mwanamapinduzi, aliposhika usukani wa madaraka lengo lake halikuwa ni kuondoa mfumo wa kibepari au 'ukoloni mamboleo' kama wanaharakati wanavyoita bali kuingiza mabadiliko katika mifumo ya kodi na matunizi ya fedha za serikali, kutatua changamoto zinazowakabili wananchi walio wengi.

Takwimu za Benki ya Dunia (WB) zinaonyesha kuwa umaskini nchini Peru ulipungua kwa kasi kubwa, kutoka asilimia takriban 60 ya wananchi wote mwaka 2004 hadi kufikia asilimia 25.8 mwaka 2012.

Ni takwimu za mwaka uliotanguliwa Garcia kutwaa madaraka kwa mara ya pili, na mwaka uliofuata alipoondoka.

Vipindi vyake vya utawala nchini humo vilitofautiana sana, kwani kipindi cha kwanza, mwaka 1985 hadi 1990 kiligubikwa na hali ngumu ya uchumi (enzi ambako mfumo wa fedha bara la Amerika ya Kusini uliparaganyika kutokana na mabadiliko ya thamani katika uchumi wa dunia, kufanya madeni yao yasilipike).

Hata hivyo, jina lake lilibaki katika midomo ya wananchi wa Peru baada ya kutoka madarakani, na mwaka 2001 akashindwa katika duru ya pili ya uchaguzi wa rais, nyuma ya mhafidhina Alejandro Toledo.

Miaka mitano baadaye akawa ndiyo 'shushu' wa wapiga kura hasa wa hali ya kawaida akaingia madarakani, lakini kipindi hiki kilikuwa kigumu kwake kutokana na mifarakano hasa na watu wa makabila ya jadi kutaka maeneo yao yasiguswe na 'wakuja.'

Pia kulikuwa na tatizo la rushwa ambalo viongozi wengi wanaharakati wanajaribu kupambana nalo lakini wa jumla wanakwama, kwani siasa inategemea sana kuchangiwa na watu wenye ushawishi katika maeneo tofauti ya uchumi na jamii.

Wana maslahi halisi wanayotazamia kuwa anayeingia madarakani kwa ridhaa au misaada na wawezeshaji wao atayafanyia kazi, na akichukua hatua hizo siyo ajabu ipatikane njia ya kumhusisha kutumikia 'wenye mali,' kama aliyokuwa akisema Mwalimu Nyerere katika maongezi na waandishi wa habari mwaka 1995.

Ni katika kufuatilia sera za kiliberali na mkazo katika kodi ambako alikuwa upande wa wawekezaji katika mzozo na wenyeji wa maeneo tofauti, na hivyo kulaumiwa kufumbia macho matukio ya uvunjaji wa haki za binadamu.

Garcia alikuwa mshiriki wa siasa za uadui na urafiki kati ya wanamapinduzi na wahafidhina katika bara hilo, ambalo alikuwa na uelewano mzuri na rais mwanaharakati wa Brazil, Luiz Ignacia Lula da Silva, ambaye sasa anatumikia kifungo cha miaka 12 kwa madai ya rushwa.

Garcia alijaribu tena kugombea mwaka 2016 akapata asilimia 5.8 ya kura mzunguko wa kwanza, hivyo akafikia tamati yake kisiasa.

Vyombo vya habari nchini Peru viliripoti kuwa mwezi Mei 2012, akiwa ameondoka madarakani, alipewa dola 100,000 kutoa hotuba kwa viongozi wa kibiashara nchini Brazil, huko Sao Paulo, ambayo baadaye vyombo vya habari vikasema ni milungula kutoka kwa kampuni ya ujenzi ya Brazil, Odebrecht.

Mzunguko huo wa tuhuma umeendelea hadi majuzi ambako polisi walitumwa nyumbani kwake kwenda kumkamata, akajiua kwa risasi kabla ya kuingizwa hali ya ufungwa.

Mwaka 2016 na 2017 mawaziri wake watano wa zamani walifunguliwa mashtaka ya rushwa na mfumo wa sheria wa nchi hiyo, ambako hakimu jaji ndiye anaitisha uchunguzi ili afungue kesi, na siyo lazima polisi au mamlaka nyingine ifikishe kesi kama hiyo mahakamani.

Mawaziri hao ni Yehude Simon (aliyekuwa waziri mkuu), Rosario Fernandez (sheria), Mercedezs Cabanillas (mambo ya ndani), Antero Flores Araoz (ulinzi) na Luis Nava (uzalishaji).

Mwezi Novemba mwaka jana mahakama ilimzuia kusafiri nje kutokana na kashfa ya Odebrecht iliyokuwa inaendelea kuchunguzwa.

Aliingia maskani ya balozi wa Uruguay jijini Lima hapo Novemba 17 mwaka jana lakini ombi lake la hifadhi ya kisiasa lilikataliwa.

Ni kashfa ambayo imelazimu kukamatwa marais wa zamani wa Peru walio hai waliokuwa madarakani kuanzia mwaka 2000 ambao ni Alejandro Toledo, Ollanta Humala na Pedro Kucyzynski.

Ni hali aliyoshindwa kuizoea akajiua April 17.

Ni mazingira ambayo bado yanaleta mijadala miongoni mwa wanaharakati na wasomi wa masuala ya katiba, suala la kuwapo katiba inayowezesha nusu ya serikali iliyotangulia kukamatwa kwa madai ya rushwa, na katika hili la Peru, marais wastaafu watatu waliotawala tangu 2000 wote wanakamatwa kuhusiana na rushwa.

Badala ya kuwa kielelezo cha kuenea kwa rushwa nchini Peru inakuwa ni kielelezo cha udhaifu wa katiba na mifumo ya sheria, hasa kutokana na kanuni ya kimapinduzi ya hakimu au jaji kuidhinisha mashtaka, na siyo lazima yatoke chombo rasmi kinachoweza kuendesha mashtaka ya jinai, kama polisi au idara ya upelelezi, tume ya rushwa, n.k.

Kwa njia hiyo mahakama zinakuwa ni washikadau wa siasa, kufungua kesi kwa kuangalia wasichokitaka.





# Wafanyabiashara wasubiri kwa shauku ziara ya JPM

**Na Grace Mwakalinga**, MBEYA

WAFANYABIASHARA katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, wamesema ujio wa Rais John Magufuli, utafungua fursa za kibiashara kutokana na kupatiwa ufumbuzi kwa baadhi ya miradi mikubwa ya maendeleo inayoonekana kususua.

Wamesema miradi hiyo likiwamo Soko la Mwanjelwa, barabara, ujenzi wa soko la uhindini pamoja na Uwanja wa Ndege wa Songwe, imeshindwa kukamilika kwa wakati na baadhi imeshindwa kutekelezwa kabisa.

Wakizungumza na Nipashe jana kwa nyakati tofauti, wafanyabiashara hao wa Soko la Uhindini, walisema kwa kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais Magufuli nchini, baadhi ya miradi mikubwa imetekelezwa lakini kwa Mkoa wa Mbeya hususani Jiji la Mbeya miradi hiyo imeshindwa kufanya vizuri.

"Ukiangalia soko la uhindini tangu liteketee kwa moto mwaka 2010 hakuna ujenzi unaofanyika licha ya halmashauri kuwa na mikakati mingi mizuri, Soko la Mwanjelwa tangu watuhumiwa wa ubadhirifu wa fedha wakamatwe hadi sasa linashindwa kufanya vizuri," alisema Mwajuma Mwakanyamale na kuongeza kuwa hata uwanja wa ndege wa Songwe eneo la abiria hadi sasa halijakamilika.

Alitupia lawama Wakala wa Barabara za Vijijini na Mjini Jiji la Mbeya (TARURA) kwa kushindwa kutekeleza kwa wakati ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya barabara.

Alisema miundombinu ya barabara hasa za ndani ya Jiji la Mbeya zimekuwa ni kikwazo kikubwa cha maendeleo kwani magari yamekuwa yakishindwa kuingia kwenye maeneo ya biashara ambayo yametengwa na halmashauri kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo.

Mwenyekiti wa Soko la Sokoine, Joseph Mwakitalima, alisema amefurahishwa na ujio wa Rais Magufuli jijini Mbeya, kwani masuala mengi ya maendeleo ambayo yalisimama na kuzua sintofahamu yatapatiwa ufumbuzi.

Akizungumzia ujio huo, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mbeya, Afrey Nsomba, aliwataka wakazi wa Jiji la Mbeya kutumia nafasi hiyo kuwasilisha kero, malalamiko na changamoto za maendeleo kwa Rais wao ili ziweze kupatiwa ufumbuzi badala ya kuendekeza siasa zisizo na msingi.

Hivi karibuni, Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), Mbeya, Mhandisi Alberto Kindole, alisema Sh bilioni 12 zimetolewa na Serikali kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara na madaraja.

Alisema shughuli za ujenzi zinaendelea na kwamba wakandarasi wanaendelea na kazi usiku na mchana kuhakikisha barabara hizo zinakamilika ifikapo mwezi Septemba mwaka huu.

## Chunya wapata fedha za kuchimba visima

**NA Grace Mwakalinga,** CHUNYA

SERIKALI imetoa Sh. bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa visima vya maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya na kwamba kukamilika kwa visima hivyo kutawaondolea wananchi adha ya kupata huduma ya maji.

Hayo yalisemwa jana na Mbunge wa Jimbo la Chunya, Victor Mwambalaswa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa shughuli za maendeleo.

Mwambalaswa alisema wananchi wa Wilaya ya Chunya kwa kipindi kirefu wamekuwa wakikabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa maji na kwamba maji wanayotumia hayakidhi mahitaji kutokana na idadi kubwa ya wananchi.

Alisema kutokana na changamoto hiyo, Serikali imetoa kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya ujenzi wa visima vya maji ambavyo vitajengwa karibu kila kata na kwenye maeneo ya kutolea huduma za kijamii ikiwamo hospitali na shule.

"Wilaya ya Chunya inakabiliwa na changamoto kubwa ya maji lakini mimi Mbunge nimekuwa nikiwasilisha hoja hii kwenye vikao mbalimbali vya bunge na wadau wengine na sasa tumepata fedha hizo ambazo zitasaidia kupunguza changamoto hiyo na mipango yangu ni kumaliza kabisa kero hiyo," alisema Mwambalaswa.

Alisema mradi huo wa visima utawahudumia zaidi ya wananchi 2,000 na kwamba lengo ni kuwafikia wananchi wote wa Wilaya ya Mbarali na kuwaomba wananchi kuendelea kuitunza na kuilinda miradi hiyo ya maji ili iwanufaishe.

Baadhi ya wananchi wa Wilaya ya Chunya akiwamo Nicodemas Mwaihojo, alisema changamoto ya maji imesababisha madhara makubwa katika familia ikiwamo ugomvi wa mara kwa mara.

Alisema ndoa nyingi huvunjika kwa sababu ya kufuata huduma ya maji maeneo ya mbali lakini pia maji yanayopatikana siyo safi na salama.



Watoto wadogo wa Kituo Shikizi cha Ibututu katika kijiji cha Ilota, Kata Mshewe, wilayani Mbeya, mkoa wa Mbeya, wakinawa mikono kabla ya kupata uji shuleni hapo wiki iliyopita. Kituo cha satelaiti ni mojawapo ya vituo 23 vinavyofadhiliwa na Unicef. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**.

# CCM Mbeya yafurahia mafanikio ya TASAF

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

CHAMA Cha Mapinduzi Wilaya ya Mbeya Mjini, kimeeleza kufurahishwa na utendaji kazi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), ulivyotekeleza mpango wa kuzisaidia Kaya masikini kwa asilimia 99.

Hayo yalisemwa jana na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mbeya, Afrey Nsomba, katika kikao na waandishi wa habari ambapo alisema walengwa wa mfuko huo jijini Mbeya wamenufaika kwa asilimia 99.

Alisema CCM ilifanya ziara ya kutembelea maeneo ya wanufaika na kuongea nao ambapo walieleza namna mfuko huo ulivyowasaidia kujikwamua na umasikini.

Alisema wanufaika hao wamefanikiwa kupiga hatua za maendeleo kwa kufungua miradi mbalimbali ya kujiingizia kipato na kuomba Serikali kuendelea kuwasaidia ili watimize ndoto zao.

"Tunapongeza jitihada zilizofanywa na mfuko wa tasaf hakika wananchi wamenufaika matokeo haya yanatokana na jitihada za usimamizi mzuri wa fedha ambazo zimetolewa kwa walengwa naomba viongozi mwendelee na moyo huo," alisema Nsomba.

Baadhi ya wananchi walionufaika na mpango huo walisema umechangia kuendesha maisha yao ya kila siku yakiwemo mahitaji ya familia.

Mmoja wa wanufaika, Beatrice Mwanisongole, ambaye ni mjane anayeishi na wajukuu zake watatu katika Kata ya Iyela, alisema TASAF imekuwa msaada kwake kwani fedha alizopewa zimemsaidia kuendesha familia yake ikiwamo kuwanunulia sare za shule wajukuu zake na chakula.

Naye Eva Mbonile alisema fedha za TASAF zimesaidia kuanzisha miradi mbalimbali na kwamba mpaka sasa anaendelea na ufugaji wa kuku wa nyama na mayai.

Alisema ufugaji wa kuku umemtengenezea faida kubwa ambayo imemwezesha kuanza ujenzi wa nyumba.



# Askofu Mwamasika aonya wanasiasa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ASKOFU Mstaafu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Dodoma, Dk.Peter Mwamasika, amewataka wanasiasa kutowatumia viongozi wa dini kwa lengo la kutimiza matakwa yao binafsi.

Dk. Mwamasika alitoa kauli hiyo kwenye ibada iliyoandaliwa na Umoja wa Madhehebu ya Kikristo Mkoa wa Dodoma kwa lengo la kuliombea taifa, viongozi wa kiserikali, kisiasa na kidini.

Akitoa salamu zake kwa waumini kutoka madhehebu mbalimbali ya dini, alisema kuwa ifike hatua viongozi wa kisiasa waache kuwatumia viongozi wa dini kwa ajili ya kufanikisha malengo yao.

Aidha, alisema viongozi hao wa serikali na kisiasa wanatakiwa kuhakikisha wanawajibika katika kushiriki ibada ili waweze kupata mafundisho ambayo yatawafanya kuwa na hofu ya Mungu kwenye utendaji wao.

"Nataka kuwaeleza leo nyie viongozi wa madhehebu ya dini mliokusanyika katika ibada hii, msikubali kutumiwa na viongozi wa kisiasa au wa kiserikali ili kufanikisha mambo yao wakati wao hawapo tayari hata kushiriki kwenye mikusanyiko wa kidini kama hii," alisema.

Aliongeza: "Ni lazima niwaambie nyie viongozi wa dini msiogope kuwaambia ukweli kwa wanasiasa na viongozi wa serikali na mnatakiwa muwaambieni ukweli na zaidi hakikisheni mnawahimiza pia wafanye Ibada kama ilivyo kwa wengine."

Pamoja na hayo, alisema viongozi wa dini wahakikishe wanafuatilia wanasiasa na viongozi wa serikali wahudhurie ibada na wasipowaona katika shughuli hizo za ibada wawafuatilie ili wajue walipo.

Kwa upande wake, Mchungaji Vincent Malendaa, akihubiri katika ibada hiyo, alisema kuwa umefika wakati wa kuisimamia amani ya nchi sambamba na kuimarisha umoja kati ya serikali na viongozi wa dini.

Naye, Mwenyekiti wa umoja huo, Padri Job Tharael, alisema kuwa umoja huo unatarajia kufanya usajili kwa lengo la kuwaunganisha viongozi wa dini na serikali.

Kiongozi huyo alisema mkakati mwingine wa umoja huo ni kuhakikisha Wakristo katika mkoa wa Dodoma waliopo chini ya mwavuli wa TEC, CCT na CPCT unawaweka pamoja ili kuondoa utofauti ambayo mara nyingi imekuwa ikikwamisha huduma za kiroho na kimwili.



Spika wa Bunge, Job Ndugai (katikati), akiongoza kikao cha Kamati ya Uongozi kilichofanyika ofisini kwake bungeni, jijini Dodoma. **PICHA: OFISI YA BUNGE**.

# RPC Muroto ataka wahalifu mitandaoni wapate taabu sana

**Na Mwandishi wetu,** DODOMA

KAMANDA wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, ameitaka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Kanda ya Kati, kushirikiana na kampuni za mitandao ya simu kuwadhibiti wahalifu wanaotumia mitandao kuwatapeli wananchi.

Muroto alitoa kauli hiyo jijini hapa wakati akifungua mkutano wa wadau wa huduma za mawasiliano mkoa wa Dodoma.

Alisema kumezuka wimbi la wahalifu wengi wanaotumia majina ya viongozi ili kufanya uhalifu.

"TCRA ishirikiane na kampuni za simu ili kudhibiti uhalifu maana wananchi wetu wanaumizwa sana," alisema.

Muroto alisema wizi umehamia kwenye mitandao ya simu hivi sasa na kuwataka kujipanga ipasavyo kukabiliana nao.

"Watu wanapigwa sana fedha hata viongozi wanapigwa hawasemi tu," alisema.

Hata hivyo, Mkuu wa TCRA mkoani Dodoma, Antonio Manyanda, alikiri kuwa kuna uhalifu mkubwa kwa njia za mtandao na wanashirikiana na kampuni za simu kuzipitia changamoto za mawasiliano.

Kwa upande wake, Afisa biashara wa Haloteli mkoani hapa, Steven Komu, alisema wamekuwa wakiwataka watumiaji kuthibitisha polisi kadi zao za simu ili kuruhusu kampuni kuwatengenezea kadi nyingine mpya kama ya awali imepotea.

Naye, Meneja wa Vodacom mkoa wa Dodoma, Balikulije Mchome, alisema wateja wamekuwa wakisajili kadi zao za simu kwa kutumia vitambulisho vinavyotambulika na watajitahidi kwa njia zote kuhakikisha kadi zinazotumika ziwe na majina kamili.

# Waziri aonya watendaji wanaokaidi agizo la Rais

**Na Mwandishi Wetu,** KONDOA

SERIKALI imesema itamchukulia hatua mtendaji yeyote au taasisi itakayobainika kukaidi amri ya Rais John Magufuli ya kutowasumbua wananchi wanaoishi katika vijiji na vitongoji vilivyo karibu na maeneo ya hifadhi hadi hapo kamati iliyoundwa itakaposhughulikia suala hilo.

Onyo hilo lilitolewa juzi na Naibu Waziri Maliasili na Utalii, Contantine Kanyasu, alipokuwa akizungumza na wakazi wa kijiji cha Kisondoko ambacho ni miongoni mwa vijiji vilivyopo karibu na pori la akiba la Mkungunero wilayani Kondoa.

Hatua hiyo ya Kanyasu ilitokana na malalamiko kutoka kwa wakulima na wafugaji wanaoishi katika vijiji na vitongoji kuzunguka pori hilo kudai kuwa wanabughudhiwa na kukamatwa na baadhi ya viongozi.

Akizungumza na wananchi hao, Kanyasu alisema mtendaji yeyote wa wizara au taasisi atakayewasumbua wananchi atachukuliwa hatua kwa kuwa kamati ya mawaziri saba iliyoundwa na Rais bado inashughulikia suala hilo.

"Ni makosa makubwa kudharau agizo la Rais, Rais anaweza hata kufuta hii Mkungunero yote... alisema maeneo ambayo hakuna wanyama watu wapewe wafuge, walime anasema hivi anafahamu kuwa Watanzania tunaongezeka," alisema.

Naibu Waziri huyo alisema uamuzi wa Rais sio wa kupuuza na kamati bado inashughulikia.

"Tumegundua kuna vijiji na vitongoji 822 ambavyo vina mgogoro na wala sio 336... tumeandaa taarifa imekamilika na Rais atakabidhiwa wiki hii akikabidhiwa tutajua vijiji gani vinatolewa kutokana na unyeti wake," alisema Naibu Waziri huyo.

Alisema unyeti wenyewe ni kama maeneo hayo ni vyanzo vya maji na kama kuna kijiji kitakuwa na unyeti huo, wananchi watatolewa na kuhamishiwa eneo lingine.

"Tayari tumeshafanya mpango huo, na tutakapoamua kuwatoa tutawapeleka hapa, hakuna atayaketolewa tukamwambia atafute pa kwenda," alisisitiza.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Kondoa, Sezaria Makota, alisema tatizo kubwa lililopo ni baadhi ya wenyeji kuwakaribisha wageni kutoka mkoani Manyara na kuingiza mifugo katika pori hilo.

Nao, baadhi ya wananchi waliiomba serikali kushughulikia suala hilo haraka ili wananchi waendelee na shughuli zao za maendeleo.



## HABARI ZANZIBAR

# CCM yaonya wanaohatarisha amani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Abdulla Mabodi, amesema chama hicho kimejidhatiti kutatua kero za wananchi pamoja na kusimamia demokrasia kwa kukemea vitendo viovu vinavyohatarisha amani na utulivu wa nchi.

Alitoa kauli hiyo katika ziara yake ya kukagua uhai wa chama na utekelezaji wa Ilani ya CCM katika Jimbo la Makunduchi Wilaya ya Kusini Unguja.

Alisema vipaumbele vya CCM ni kutekeleza kwa kasi ahadi ilizotoa kwa wananchi kupitia Uchaguzi Mkuu uliopita.

Alisema CCM inaendelea kuaminiwa, kupendwa na kuthaminiwa na mamilioni ya Watanzania kutokana na usimamizi mzuri wa utekelezaji wa sera zake na kwa kutatua changamoto za kijamii kwa wakati.

Aidha, alisema katika kusimamia demokrasia, CCM haitasita kukemea vitendo viovu vinavyoashiria kuvunja sheria za nchi, hasa vinavyotekelezwa na baadhi ya vyama vya upinzani.

"Tumekubali kuingia katika mfumo wa vyama vingi ili tushindane kwa sera na siyo kushindana kwa vituko na vurugu hivyo ni muhimu kila mwanasiasa ajitathimini kuhusu mwenendo wake kwa jamii anayoiongoza," alisema Dk. Mabodi.

Alisema CCM mpya imekuwa kimbilio la wananchi wanaoamini katika siasa za maendeleo ambao wametelekezwa na vyama vyao na kupokelewa vizuri ndani ya CCM ili wanufaike na demokrasia ndani ya chama hicho.

Aliwataka viongozi na watendaji wa CCM kutowawekea vikwazo wananchi wanaotaka kujiunga na chama hicho na badala yake wapewe fursa hiyo bila masharti magumu.

Aliwaagiza wabunge, wawakilishi na madiwani kufanya mikutano katika maeneo yao na kuwaeleza wananchi mafanikio yaliyofikiwa katika utekelezaji wa Ilani ili wananchi hao wawe mabalozi wa kufikisha taarifa hizo kwa jamii.

Aliwaambia wananchi kuwa CCM imesimamia kwa ufanisi miradi ya maendeleo ukiwemo Mpango wa Kusaidia Kaya Maskini (TASAF) ambao upo katika Ilani ya CCM ya mwaka 2015/2020, ambao umewaondoa wananchi katika wimbi la umasikini na kuwa na kipato cha kati.

Naye Mwakilishi wa Jimbo la Makunduchi, Haroun Ali Suleiman, alisema tayari Ilani ya CCM ndani ya Jimbo hilo imetekelezwa kwa asilimia 90 na kwa sasa wanaendelea kutatua baadhi ya changamoto ili kuzimaliza kabla ya 2020.

Kwa upande wake, Mbunge wa Jimbo hilo, Ameir Haji Timbe, alisema maendeleo yaliyopatikana katika Jimbo hilo yametokana na ushirikiano mkubwa uliopo baina ya viongozi na wananchi.

Mwenyekiti wa Maskani ya CCM ya Kisonge iliyopo Makunduchi, Abdallah Hassan Haji alisema wanaendelea kuvuna wanachama wapya kutoka vyama vya upinzani huku wakijipanga kufuta masalia ya upinzani ndani ya Jimbo hilo.

Alisema ziara hiyo imezaa matunda kwani wamejionea na kujifunza mambo mbalimbali ikiwemo ufugaji wa samaki.



Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Itilima, wilayani Kishapu, Athumani Katundu, akitoa mada kwa wanawake na watoto namna ya kutunza ushahidi dhidi ya matukio ya ukatili wa kijinsia, ili watuhumiwa wapate kutiwa hatiani na kufungwa jela, katika semina iliyofanyika wilayani humo juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Mwakilishi ataka wananchi wadumishe Muungano

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANANCHI wametakiwa kuenzi, kuthamini na kudumisha Muungano ili kuendeleza amani na kuharakisha maendeleo.

Hayo yalisemwa jana na Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni, Rashid Makame Shamsi, wakati alipofanya ziara na ujumbe wa watu 85 kutoka Kata ya Mbagala Kuu jijini Dar es Salam.

Ziara hiyo ilifanyika katika hifadhi ya samaki Fukuchani ambapo walifanya mazungumzo na uongozi wa Jimbo la Nungwi Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema Muungano umeleta mafanikio katika nyanja mbalimbali kama vile kielimu, kiuchumi na kukuza uhusiano mwema.

Aidha, alisema viongozi walioasisi Muungano huo wametumia busara na hekima katika kuunganisha nchi mbili hizo ili kuleta maendeleo kwa wananchi wake.

Hata hivyo, aliwataka wananchi kuhakikisha wanaulinda na kuudumisha Muungano huo kwa nguvu zote kwa faida yao na taifa kwa ujumla.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi, Kata ya Mbagala Kuu, Khamis Shaaban Malenda, alisema ushirikiano waliouanzisha wa Kata ya Sogea na Kata ya Mbagala Kuu utasaidia kupata mbinu za kubuni vyanzo vya mapato na kukuza uchumi.

# Serikali yapigia debe elimu ya jinsia

**Na Rahma Suleiman, Z**ANZIBAR

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Dk. Idrisa Muslimu Hija, amesema ipo haja ya kuwapa mafunzo vijana kuhusu umuhimu wa elimu ya jinsia.

Aliyasema hayo jana wakati akifunga warsha ya kuwajengea uwezo Wakuza Mitaala wa Vyuo Vikuu na Taasisi mbalimbali za serikali na binafsi katika ukumbi wa Mtakwimu Mkuu wa Serikali Mazizini mjini Unguja.

Alisema elimu hiyo itawasaidia vijana kupunguza mmomonyoko wa maadili katika jamii kutokana na kukua kwa utandawazi.

Alisema kurejesha maadili mema kunahitaji ushirikiano baina ya wazazi, walezi na walimu ili kutengeneza jamii yenye mmwelekeo mwema.

Aidha, Dk. Idrisa alisema kuwachanganya wanafunzi wenye mahitaji maalum na wanafunzi wa kawaida darasa moja kutasababisha wanafunzi hao kujisikia kwamba jamii inawajali katika kupata elimu bora.

Alisema upo umuhimu kwa vyuo vinavyosomesha walimu kuingiza somo la elimu jumuishi ili kila mwalimu ajue jinsi ya kuwasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Elimu Jumuishi na Stadi za Maisha, Mpaji Ali Maalim, alisema kitengo chake kitahakikisha kinaweka mikakati imara ili kuleta mafanikio katika elimu jumuishi kwa jamii ili wanafunzi wapate elimu inayostahiki na inayokidhi kitaaluma.

Alisema watu wenye mahitaji maalum hukosa elimu ya lazima kutokana na kukosa uangalizi maalum kwa walimu ambao unatokana na kutokua na mbinu madhubuti katika kuwaelimisha.

Kwa upande wao, washiriki wa warsha hiyo walisema kuna ulazima kila shule kuwekewa mwalimu maalum wa ushauri nasaha kwa lengo la kukuza elimu ya jinsia na madhara yatokanayo na udhalilishaji.

Warsha hiyo iliandaliwa na Kitengo cha Elimu Jumuishi na Stadi za Maisha chini ya ufadhili wa Shirika la Kimataifa la Elimu Duniani (UNESCO).

## Jeshi kuunda serikali ya kiraia muda wowote

**KHARTOUM,** Sudan

MSEMAJI wa Jeshi la Sudan, Jenerali Shamseldin Kibashi, amesema uongozi wa baraza la mpito la kijeshi unafanya mazungumzo na pande zote za kisiasa kupata jina la Waziri Mkuu ili kuunda serikali ya kiraia.

Kupitia taarifa yake, Jenerali Kibashi alitoa tamko fupi la nia ya kuunda serikali ya kiraia ingawa hakutoa kauli yoyote juu ya matakwa ya waratibu wa maandamano ambao wanataka kuundwa kwa serikali ya kiraia haraka.

Mvutano umezidi kuwa mkubwa Sudan baada ya mazungumzo kati ya waandamanaji na baraza la mpito la kijeshi ambalo linaongoza nchi hiyo tangu Rais wa zamani Omar al Bashir alipoondolewa madarakani Aprili 11 mwaka huu kuvunjika.

Waandamanaji hao wanautuhumu uongozi mpya wa kijeshi kwamba una tofauti ndogo kulinganisha na Al Bashir aliyeng'olewa kwenye kiti chake baada ya maandamano yaliyoanza mwezi Desemba mwaka jana.

Waratibu wa maandamano hayo wameapa kuyaendeleza maandamano hadi pale matakwa yao yote yatakapotimizwa.

Hata hivyo, Jenerali Kibashi jana akijaribu kuupoza mvutano unaoendelea, aliwaambia waandishi wa habari kwamba baraza la mpito la kijeshi la Sudan linachunguza na kuyafanyia kazi madai ya waandamanaji na kwamba watawasiliana na kila mmoja ili kufikia muafaka.

Naye kiongozi wa Baraza la mpito la kijeshi, Jenerali Abdel Fattah Burhani alihaidi kwamba baraza hilo litawapa madaraka wananchi baada ya makubaliano na pande zote mbili. **DW**

## Tshisekedi, Kabila wakutana

**KINSHASA,** Congo

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Felix Tshisekedi, amekutana na Rais wa zamani wa nchi hiyo, Joseph Kabila kujadili jina la Waziri Mkuu mpya.

Wawili hao walikutana na kuzungumza kuhusu nafasi ya Waziri Mkuu ambayo imekuwa wazi kwa muda wa miezi minne baada ya uchaguzi wa urais uliompa ushindi Tshisekedi.

Awali Tshisekedi na mtangulizi wake Joseph Kabila walikuwa hawaelewani kufuatia mvutano wa kisiasa uliokuwa umeikumba DRC na kisha baada ya uchaguzi wa urais wawili hao waliamua kufanya kazi kwa ushirikiano wakiwa katika muungano mmoja wa kisiasa.

Rais Tshisekedi na Joseph Kabila walikuwa hawajakutana kwa wiki kadhaa kutokana na ziara za kikazi za Tshisekedi nje ya nchi.

Mazungumzo kati ya wawili hao kuhusu uteuzi wa waziri mkuu na uundwaji wa serikali yalidumu kwa muda wa saa moja.

Mwanzoni, wawili hao walikuwa wamechagua timu za mazungumzo lakini hayakufanikiwa. **RFI**

# Tawheed Jamaat wanyooshewa kidole milipuko Sri Lanka

**COLOMBO,** Sri Lanka

ZIKIWA zimepita siku tangu kutokea kuwa milipuko Sri Lanka katika makanisa matatu na hoteli moja na kuuwa watu wapatao 290, Kundi la kigaida la Tawheed Jamaat nchini humo linadaiwa kuhusika na shambulio hilo.

Msemaji wa Serikali ya Sri Lanka, Rajitha Senaratne alisema dalili za mwanzo zilizotokana na uchunguzi zinaonyesha mashambulio hayo yamefanywa ili kulipiza kisasi kwa mauwaji yaliyotokea katika misikiti miwili ya mji wa Christchurch, kusini mwa New-Zealand marchi, mwaka huu ambapo watu 50 waliuawa.

Jeshi la Polisi nchini humo limesema watu 40 wanashikiliwa kuhusiana na mashambulio hayo ambayo ni ya kikatili na hayajawahi kutokea tangu vita vya wenyewe kwa wenyewe vilipomalizika nchini Sri Lanka mwongo mmoja uliopita.

**Muda mfupi baada ya dakika tatu hizo za maombolezi, msemaji wa polisi alisema idadi ya watu waliouawa imefikia watu 310.**

Mashambulio hayo ni mabaya kuwahi kutokea dhidi ya jamii ya wachache ya wakristo wanaofikia asili mia saba ya wakazi milioni 21 wa Sri Lanka.

Senaratne alisema uchunguzi bado unaendelea kuhusu kundi hilo kama endapo lilipata msaada kutoka nje ya Sri Lanka.

Ofisi ya Rais Maithripala Sirisena ilisema wamepokea habari kwamba makundi ya kigaidi ya kimataifa yamewasidia wahalifu wa ndani na kwamba Sri Lanka itaomba msaada wa kimataifa kulichunguza suala hilo.

Baada ya kutokea kwa tukio hilo, Wasrilanka milioni 21 walikaa kimya kwa dakika tatu kuomboleza na kuwakumbuka watu waliofariki katika shambulio hilo.

Bendera zilipepea nusu mlingoti katika majengo ya serikali na watu kuinamisha vichwa chini na kuomboleza kimya kimya.

Muda mfupi baada ya dakika tatu hizo za maombolezi, msemaji wa polisi alisema idadi ya watu waliouawa imefikia watu 310.

Maafisa bado wanachunguza kwanini hatua za tahadhari hazikuchukuliwa baada ya onyo lililotolewa April 11 kwamba kundi la Tawheed Jamaat-NTJ linapanga kufanya mashambulio makanisani.

Marekani imesema raia wake wanne wameuawa, huku Uholanzi ikisema raia wake watatu wameuawa. **DW**



Mbunge wa Jimbo la Kyadondo nchini Uganda, Robert Kyagulanyi ambaye amezuiliwa kutoka ndani ya nyumba yake na Jeshi la Polisi. **PICHA: AP**

# Bobi Wine Jeshi 'afungiwa' nyumbani

**KAMPALA,** Uganda

POLISI na Jeshi nchini Uganda jana jioni walizingira nyumba ya Mbunge wa Kyadondo mashariki, Robert Kyagulanyi maarufu kama Bobi Wine, saa kadhaa baada ya kutangaza mpango wake wa kutembea hadi polisi katika maandamano ya umma kupinga ukatili dhidi ya tamasha lake la muziki na wanasiasa wa upinzani.

Bobi Wine aliwataka Waganda wote wenye hasira kuungana nae katika mapambano hayo dhidi ya ukosefu wa haki.

Kutokana na uamuzi wake huo, Bobi Wine aliwekwa katika kizuizi cha nyumbani katika kile ambacho polisi walisema ilikuwa ni hatua ya kumzuia mwanasiasa huyo wa upinzani kufanya mikutano iliyo kinyume cha sheria.

"Hizo zilikuwa ni hatua zilizochukuliwa chini ya sera ya kuzuwia ili kulinda sheria na utulivu wa umma. Wakati bado anatishia kufanya mikutano kinyume cha sheria, maafisa wetu wa ujasusi watatusaidia kumpata na tutaweza kuona ni nini kitakachofuatia," alisema memaji wa polisi Fred Enanga na kuongeza:

"Hata hivyo hadi sasa tutaendelea kwa sababu hili limekuwa ni suala la usalama wa taifa" alisema.

Bobi Wine alikuwa ametangaza mpango wa kufanya maandamano ya umma kote nchini kupinga hatua ya polisi kuendelea kuweka vikwazo dhidi ya matamasha yake ya muziki na ukatili dhidi ya wanasiasa wa upinzani.

Alitangaza uamuzi huo alipokuwa nyumbani kwake Magere, Kasangati katika wilaya ya Wakiso muda mfupi baada ya polisi kumzuia asubuhi kufika katika makazi yake ya ufukweni ya One Love Beach yaliyopo eneo la Busabala.

"Nilitaka kuiambia dunia kile kinachofuatia na hicho ndicho polisi hawakutaka kukisikia," alisema Wine.

"Tumetumia njia zote za kisheria polisi wasitusimamishe kuzuia maonyesho yangu na kuwatesa wapinzani lakini wameshindwa kuelewa. Ninatoa wito wa kuwapo kwa mbinu nyingine za kisheria ambazo ni kupinga," Bobi Wine alivieleza vyombo vya habari kwenye makazi yake ya Kasangati. **BBC**

# Makonda awatangazia neema mafundi magari

Na Mary Geofrey

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, amesema Serikali imejipanga kutoa mafunzo kwa mafundi wa magari pamoja na wauzaji wa vyuma ili kupatiwa vyeti na kuweza kutambulika.

Alisema serikali itawalipia gharama za masomo katika vyuo vya Mamlaka ya Ufundi Stadi (Veta) ili kutambulika na kufanya kazi kwa weledi.

Makonda alitoa ahadi hiyo jana wakati akizungumza na mafundi magari wa Manispaa ya Ilala katika muendelezo wa ziara yake ya kutembelea miradi ya maendeleo katika mkoa huo.

"Hawa mafundi wa magari pamoja na watu wa vyuma tuna mpango wa kuwapeleka Veta na Serikali italipia gharama zao na watapata vyeti vya kutambulika katika kazi zao," Makonda alisema.

Alisema pia serikali ya awamu ya tano imesimama na kutetea wanyonge kwa upande wa afya, elimu pamoja na miundombinu.

Alisema wananchi waishio katika hali ya chini wamepata nafasi ya kupata haki sawa bila kuweka matabaka kama ilivyokuwa hapo awali.

"Naomba niweke sawa neno wanyonge kwa jinsi ninavyofahamu wanyonge ni wale wananchi waliokandamizwa kwa muda mrefu kwa kupoteza haki yao, hawa wafanyabiashara wamachinga, mama ntiliye walikuwa hawajulikani lakini chini ya Rais wetu John Magufuli wametambulika na wanapambaniwa kwa kupewa haki yao," Makonda alisema.

Katika hatua nyingine Makonda alimpongeza Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Sophia Mjema, kwa kuongeza kasi katika kusimamia na kuhakikisha miradi iliyopo ndani ya Halmashauri hiyo inaenda vyema.

Katika ziara hiyo alitembelea mradi wa soko la Kisutu, mradi wa Barabara ya Kwagude iliyopo kata ya Kiwalani, Barabara ya Kampala iliyopo Gongo la mboto, Hospitali ya Wilaya ya Ilala, inayoendelea kujengwa katika kata ya Kivule, majengo mapya ya wodi ya wazazi pamoja na chumba cha Upasuaji katika kituo cha Afya cha Vingunguti Mnyawami.



Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, akimtunuku Shahada ya Uzamivu ya Kiswahili, Ali Saleh Khalfan, wakati wa hafla ya Mahafali ya 14 ya SUZA, yaliyofanyika Tunguu Zanzibar jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

## Rais Magufuli aiongezea muda Bodi Utalii

Na Mwandishi Wetu

RAIS John Magufuli, ameongeza muda wa miaka 3 kwa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) iliyokuwa imalize muda wake jana.

Taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, ilieleza kuwa Mwenyekiti na Wajumbe wote wa bodi hiyo wameongezewa muda hadi April 23, 2022.

Bodi hiyo inaongozwa na Mwenyekiti, Jaji Mstaafu Thomas Mihayo na wajumbe 6 ambao ni Augustine Kungu Olal, Zabein Muhaji Mhita, Richard Rugimbana, Mark Leveri, Ally Hussein Laay na Ibrahim Mussa.

# Wagonjwa 15 kuzibuliwa mishipa ya damu

Na Mwandishi Wetu

MADAKTARI Bingwa wa Magonjwa ya Moyo wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), kwa kushirikiana na mwenzao wa Hospitali ya Meditrina ya India, wanaendesha kambi maalum ya matibabu ya moyo kwa siku tatu ya kuzibua mishipa ya damu ambayo imeziba kwa kiwango kikubwa na hivyo kushindwa kupitisha damu vizuri.

Kambi hiyo ni maalum kwa ajili ya kuwasaidia wagonjwa wenye matatizo hayo ambao bila ya kupata mtaalamu mwenye ujuzi wa hali ya juu wa kuzibua mishipa hiyo wangefanyiwa upasuaji mkubwa wa moyo.


"Matibabu hayo yanafanyika kwa kutumia mtambo wa Cathlab ambapo mgonjwa anatobolewa tundu dogo katika paja ambalo linapitishwa vifaa maalum vya kuzibua mishipa ya damu ya moyo," alisema.

Katika kambi hiyo wataalamu wa afya wa JKCI watapata elimu ya jinsi ya kuzibua mishipa ya damu ya moyo ambayo imeziba kwa kiwango kikubwa.

Jumla ya wagonjwa 15 ambao mishipa yao ya damu mmoja hadi mitatu imeziba wanatarajiwa kutibiwa katika kambi hiyo iliyoanza leo tarehe 23 hadi 25 mwezi huu na hadi sasa wagonjwa watano wameshatibiwa na hali zao zinaendelea vizuri.


**Jipatie Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro kwa Bei Elekezi za Rejareja kama Ifuatavyo:-**

- Nusu Lita (500ml) – TSHS. 500/=
- Lita Moja na Nusu (1.5L) – TSHS. 1,000/=
- Bei Hizi Elekezi ni Kwa Nchi Nzima
- Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro ni Maji ya Kuaminika Kila Siku



TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

***Kwa Habari Motomoto***

***usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku***

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI
IDARA YA UHAMIAJI

**MAOMBI YA URAIA**



Mrs NINA ATO O. GUSWERA

Mwenye picha hapo juu, anaomba Uraia kwa Mh. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Utaifa wake wa sasa ni KENYA Nchi atokayo KENYA shughuli zake H/WIFE yupo hapa nchini tangu mwaka 2001 pamoja na kuishi DAR ES SALAAM.

Kwa yeyote mwenye taarifa/sababu za kwanini mwombaji asipewe Uraia wa Tanzania, atume taarifa ya maandishi kwa Kamishina Mkuu wa Uhamiaji. S.L.P 512, Dar es Salaam. Kumb. Na. DN 29957.

*1151191202*

---

**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**AT BUKOBA**
**LAND APPEAL NO 11/2018**
**MOHAMED AKIBARU KADURU..............................APPELLANT**
**VERSUS**
**SADAT MTEGAGURA.............................. 1ST RESPONDENT**
**AMINI AKIBARU....................................... 2ND RESPONDENT**

**TO: AMINI AKIBARU**
**Karutanga area,**
**Magata karutanga ward,**
**MULEBA DISTRICT**

**RE: NOTICE OF MENTION**

Where the above mentioned Appellant lodged an appeal registered as land appeal No 11/208 against you at the high court of Tanzania at Bukoba.

**TAKE NOTICE** that the above mentioned Appeal has been scheduled for mention on 22nd day of may, 2019 at 9:00 am before Hon KAIRD J

Take further notice that in default of your appearance on the said date and time hearing of an appeal may proceed against you, without further notice

Given under my Hand and the seal of the court this 9th day of APRIL 2019

DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
BUKOBA

115192002

---

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

Festo Kayambabila anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili wa namba T 724 DDG aina ya NISSAN EXTRAIL, yenye chasis namba NT30067744, engine namba LE4F04EFT44.


Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa :
**KJN/RB/2388/19**

*115189602*

---

**KUPOTEA KWA CHETI**



**Eugen Dickson** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.1141/0099 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 2008 katika shule ya Sekondari Swilla.

**Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa:**
**MW/RB/7175/2018**

*115190602*

---

**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

Gs Group Limited anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili wa namba MC 461 AXQ aina ya HAOJUE, yenye chasis namba LC6PCJK27F0030451.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa :**
**KBA/RB/3673/19**

*115190002*

---

**NJOO UTANGAZE**

**BIDHAA YAKO**


**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz

au piga simu: 0767 22 33 11

---

**KUPOTEA KWA CHETI**



**Eugen Dickson** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.1141/0099 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 2008 katika shule ya Sekondari Swilla.

**Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa:**
**MW/RB/7175/2018**

*115190602*

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo
MJINI MOROGORO
Usimamizi wa mirathi No;90/2019

Ombi la STEVEN GEORGE NJAMA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu CHED PETER MATAULA

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 30/04/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 09/04/2019.

215191302

---

**JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?**

**Nipashe**

NI JIBU LAKO

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI MICHEZO

# KLOPP: SITAANGALIA MAN CITY VS UNITED



**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amebainisha kwamba hadhani kama Manchester United inaweza kupata matokeo dhidi ya Manchester City leo Jumatano.

United inaingia kwenye mchezo huo wa leo huku ikitoka kuchezea kichapo cha mabao 4-0 kutoka kwa Everton Jumatano.

Hata hivyo, 'Mashetani Wekundu' hao wanaweza kupata matokeo mazuri na kuifanya Liverpool kuendelea kuongoza katika msimamo wa Ligi Kuu England.

Mashabiki wa Liverpool kwa namna yoyote watakuwa wakiishangilia United ili waweze kushinda na wao kupata nafasi ya kuendelea kuongoza huku ikipigania kutwaa ubingwa wa ligi hiyo msimu huu.

"Nafikiri nitaangalia mchezo huo kama sitakuwa na kitu cha kufanya," alisema akiliambia Gazeti la Daily Mail.

"Sioni uwezekano kwamba Man Utd watapata matokeo... matokeo ya 3-0? 4-0? Sidhani.

"Hivyo tutaangalia, City itakuwa tayari kwa ajili ya kupata matokeo mazuri na tutaangalia kama United watakuwa tayari pia.

"Ni mchezo wa kawaida, ni mchezo wanaotakiwa kucheza, tulicheza pale na tulitaka sare."

# De Bruyne hatimaye kumalizia msimu nje

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER City inapanga kumaliza kipindi cha msimu huu kilichobaki bila Kevin De Bruyne baada ya kuumia misuli ya nyama za paja mwishoni mwa wiki.

De Bruyne mwenye umri wa miaka 27, alitolewa nje wakati wa ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Tottenham katika dakika ya 38, akiibua shaka kwamba huenda asicheze tena kipindi kilichobaki.


Huku kiungo huyo wa kimataifa wa Ubelgiji akiwa anaukosa mchezo wa leo dhidi ya wapizani wao wa jiji moja, Manchester United, Gazeti la Times limeripoti kwamba mchezaji huyo hatacheza mechi zilizobaki.

Gazeti hilo limedai kwamba De Bruyne atakosa mechi zilizobaki za City dhidi ya Burnley, Leicester City na Brighton, wakati ikiwania kulitwaa taji la ligi hiyo ambalo walilitwaa msimu wa 2017/18.

Man City kwa sasa ipo nyuma kwa pointi mbili mbele ya vinara Liverpool, huku wakiwa na mchezo mmoja mkononi na kama leo itashinda pale Old Trafford itapanda kileleni.

Akiwa alicheza kama mchezaji muhimu msimu uliopita, De Bruyne amekuwa nguzo muhimu kwa kikosi hicho.





# 4-bora kuamua hatima ya De Gea na Lukaku

**MANCHESTER,** England

WACHEZAJI wa Manchester United, David de Gea, Paul Pogba na Romelu Lukaku, wanatarajiwa kuthibitisha kuendelea kubaki ndani ya klabu hiyo endapo United itasalia kwenye nafasi nne za juu katika msimamo wa Ligi Kuu England ambao utawawezesha kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Hali hii tata ya wachezaji hao kuanza kuonyesha kutafuta mlango wa kutokea imekuja mara baada ya United kukubali kipigo cha mabao 4-0 kutoka kwa Everton Jumapili na hivyo kuwaweka kwenye nafasi ngumu ya kuingia nne-bora.

Hadi sasa De Gea hajakubaliana na United juu ya mkataba wake mpya ambao umesalia mwaka mmoja ukitarajiwa kumalizika ifikapo mwaka 2020.

Endapo timu hiyo itamaliza nje ya nne-bora itakuwa ngumu kwa mlinda mlango huyo kubaki kwenye klabu hiyo.

Pogba ambaye amesajiliwa akitokea klabu ya Juventus Agosti mwaka 2016 kwa mkataba wa miaka mitano, amekuwa akitakiwa na Barcelona hali iliyosababisha wengi kuamini angeondoka kipindi cha kiangazi.

Lukaku mwenye umri wa miaka 26 mkataba wake unamalizika mwaka 2021, ameshindwa kuwa kwenye kikosi kinachoanza chini ya kocha Ole Gunar Solskjær ukijumlisha na kama watashindwa kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya bila shaka hatoweza kubaki.

HABARI MICHEZO

# HUDSON-ODOI: MSIMU HUU KUCHEZA BASI




**LONDON,** England

WINGA wa Chelsea, Callum Hudson-Odoi hatarajii kucheza tena msimu huu baada ya kuumia kifundo cha mguu juzi Jumatatu katika mchezo wa sare ya mabao 2-2 dhidi ya Burnley.

Licha ya kucheza soka la kuvutia kwa Chelsea, Hudson-Odoi alilazimika kutolewa nje na sasa nyota huyo mwenye umri wa miaka 18, anaamini hatapata tena nafasi ya kucheza.

Ingawa vipimo vinaonyesha kwamba hajaumia sana, lakini Hudson-Odoi anaamini kwamba hataweza kucheza hapo Stamford Bridge hadi mwisho mwa msimu huu.

"Naona kwamba siwezi kucheza tena msimu huu, baada ya kuumia kifundo cha mguu," alisema.

"Sasa nimebakiwa na kazi ngumu ya kuaribu kuangalia uwezekano wa kurudi tena kucheza msimu huu."

# Aaron Ramsey kuikosa Wolves



**LONDON,** England

ARSENAL imethibitisha kwamba, Aaron Ramsey ataukosa mchezo wa leo Jumatano dhidi ya Wolves wakati nyota huyo wa kimataifa wa Wales akiendelea kuuguza misuli ya nyama za paja.

Ramsey aliuumia kwenye mchezo wa Ligi ya Europa dhidi ya Napoli wiki iliyopita ambapo walifuzu hatua ya nusu fainali. Kiungo, Denis Suarez ambaye anacheza hapo kwa mkopo kutoka Barcelona pia hatakuwapo kwenye mchezo huo kutokana na matatizo ya nyonga.

Lakini pia Granit Xhaka anaweza kucheza mchezo huo kutokana na ukweli kwamba hali yake kwa sasa imeimarika. Wachezaji, Danny Welbeck, Hector Bellerin na Rob Holding bado wanaendelea kuwa nje ya mchezo huo.

Kwa upande wa Ramsey, bado ataendelea kuwa nje kutokana na kuendelea kuuguza majeruhi hayo.

Baada ya kuivaa Wolves kwenye dimba la Molineux Jumatano, Washika Bunduki hao wamebakiwa na mechi sita kumaliza msimu huu.

Kocha wa Arsenal, Unai Emery, amesema kwamba kuna uwezekano Ramsey akarudi baada ya mchezo wa leo Jumatano, kwani hali yake si mbaya.

"Naamini atakuwa uwanjani baada ya mchezo wa leo, nina imani kubwa atapona kwa haraka inavyowezekana," alisema Unai akinukuliwa na Gazeti la Daily Mail.

Aliongeza kusema kuwa wachezaji wengine ataendelea kuwakosa kutokana na kuendelea kuuguza majeruhi yao.

# *Pogba: Tumeivunjia heshima Man United*

**MANCHESTER,** England

KUINGO wa Mchester United, Paul Pogba amekiri kwamba, matokeo ya kipigo cha mabao 4-0 kutoka Everto ni kuishushia heshima klabu hiyo.

Jumapili Man United ilikubali kipigo cha aibu cha mabao 4-0 kutoka kwa Everton kwenye mchezo wa Ligi Kuu England hali iliyosababisha kufifisha matumaini ya timu hiyo kuingia kwenye nafasi nne za juu ili kupata fursa ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Akizungumzia matokeo ya mchezo huo, Pogba raia wa Ufaransa alisema: "Kwa namna tulivyocheza, na uwezo tuliouonyesha kama timu, kila mmoja wetu tumejivunjia heshima."

Pogba aliongeza: "Tumeshindwa kujiheshimu hata sisi wenyewe, klabu au mashabiki wetu. Kila kitu kimekwenda ovyo."


"Tumemwacha kocha ameongea, benchi limezungumza kwenye chumba cha kubadilishia nguo na waliongea ukweli.

"Wamesema kile kilichotokea kwenye mechi na hii si heshima kwetu kwa kile tulichofanya uwanjani si heshima hata kwa wachezaji wenzetu, kwa mwenyekiti na wafanyakazi na watu wote."

Pogba alisajiliwa akitokea klabu ya Juventus Agosti mwaka 2016 kwa mkataba wa miaka mitano, amekuwa akitakiwa na Barcelona hali iliyosababisha wengi kuamini angeondoka kipindi cha kiangazi, kwa matokeo ya juzi yanawafanya watu kufikiria kuwa wachezaji hao wameshindwa kuipa heshima timu hiyo.



# DO ZA SOKA MA YA ULAYA




# MILNER: LEO NITAISHANGILIA UNITED MARA YA KWANZA

## ●●● Lakini sitaitazama mechi, huko ni kupoteza nguvu kidogo, pengine nitaweka simu yangu mbali…

**Liverpool,** England

KIUNGO wa Liverpool, James Milner, ataishangilia Manchester United kwa mara ya kwanza katika maisha yake, lakini ataepuka kuitazama mechi yao hiyo dhidi ya Manchester City leo.

Mechi hiyo ya Mahasimu wa Manchester ['Manchester derby'] ni muhimu katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu England, EPL, wakati huu vijana hao wa Jurgen Klopp, Liverpool wakiwa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo kwa pointi mbili zaidi ya Man City ambayo ina mechi moja mkononi.

**Kiungo huyo wa zamani wa Man City na Leeds United, Milner alisema atakuwa akikishangilia kikosi cha Ole Gunnar Solskjaer, United.**

"Mara ya kwanza katika maisha yangu," alisema.

"Lakini sitaitazama. Ni kupoteza nguvu kidogo, sitafanya lolote kuhusu hili. Pengine nitaweka simu yangu mbali kwa saa chache na kutazama baadaye. Sina wazo halisi ya nitakachokifanya, labda kutoka kwa ajili ya kwenda kupata chakula."

Na wakati huu zikiwa zimebaki mechi tatu, Liverpool ipo kileleni mwa msimamo wa ligi ikiwa na pointi 88 na inaweza kumaliza msimu ikiwa na alama 97, lakini haijatwaa ubingwa wa ligi hiyo tangu mwaka 1990.

Wakati Liverpool ikiwa imebakiza mechi dhidi ya Huddersfield Town, Newcastle United na Wolves, Manchester City itakutana na Burnley, Leicester City na Brighton and Hove Albion baada ya mechi hiyo ya 'dabi'.

"Kuna mechi tatu zimebaki baada ya [dabi]. Watu wanadhani United ni changamoto, lakini si yenyewe pekee," Milner alisema. "Ni mawazo yaliyopitwa na wakati, lakini EPL ni ngumu- yeyote yule unayecheza naye, timu zinapigana mkiani."

## ZISIKUPITE

### BALE ANUKIA MKOPO UNITED

REAL Madrid itatazama uwezekano wa kumuuza mshambuliaji wa kimataifa wa Wales, Gareth Bale, 29, majira haya ya joto - ama kumtoa kwa mkopo endapo hatapatikana mnunuzi sahihi na anaweza kujiunga na Manchester United kwa mkopo kwa pauni milioni tano. ***(Marca)***

### TOURE KUTIMKIA MAREKANI

KIUNGO wa zamani wa Manchester City, Yaya Toure, 35, amefungua milango ya kutua Ligi Kuu ya Marekani [MLS] ama kujiunga na timu za Asia. ***(Goal)***

### WENGER AMWONA VIEIRA

KOCHA wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger anaamini kocha wa Nice, Patrick Vieira, 42, ambaye aliwahi kuichezea 'Gunners', ameonyesha ubora wa kutosha kuweza kuinoa miamba hiyo ya Emirates kwa baadaye. ***(Times)***

### VIDAL KUONGEZEWA MWAKA

BARCELONA inatarajia kumuongeza mkataba wa mwaka mmoja kiungo wa kimataifa wa Chile, Arturo Vidal, 31, katika mkataba wake wa sasa ambao unamalizika mwaka 2021. ***(Sport)***

### POGBA, LUKAKU, DE GEA KUSEPA

KIPA Mhispania David de Gea, 28, kiungo Mfaransa Paul Pogba, 26, na straika Mbelgiji Romelu Lukaku, 25, watatazama mustakabali wao wa baadaye kama Manchester United haitafuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Guardian)***

### RODRI KUVUNJA REKODI CITY

MANCHESTER City ipo tayari kuvunja rekodi yake ya usajili ya pauni milioni 60 ili kumsajili nyota wa kimataifa wa Hispania, Rodri, 22, kutoka Atletico Madrid ikiwa ni mpango wao wa muda mrefu wa kumwandaa kumrithi kiungo Mbrazil Fernandinho, 33. ***(Telegraph)***

### SESSEGNON VITANI SPURS, JUVE

JUVENTUS ipo tayari kutoa changamoto kwa Tottenham majira haya ya joto katika mbio za kuinasa saini ya beki wa kushoto wa Fulham, Ryan Sessegnon, 18. ***(Express)***

### MUSTAFI SOKONI ARSENAL

UNAI Emery atapitisha panga Arsenal majira haya ya joto- na beki Mjerumani Shkodran Mustafi, 27, ni miongoni mwa wachezaji watakaouzwa. ***(Mail)***

### GREALISH KUMRITHI ZAHA

CRYSTAL Palace itamfuata kiungo wa Aston Villa, Jack Grealish, 23, endapo itampoteza mshambuliaji Muivory Coast Wilfried Zaha, 26. ***(Mail)***

### MOYES AITOA UNITED 4-BORA

KOCHA wa zamani wa Manchester United, David Moyes, haamini kama klabu hiyo itamaliza nafasi nne za juu msimu huu. ***(Sun)***

### VAN DIJK AIANGUKIA UNITED

BEKI wa Liverpool, Virgil van Dijk, 27, ameiambia Manchester United wanapaswa "kuwasaidia wenyewe" katika mechi ya 'dabi' kwenye Uwanja wa Old Trafford leo. (Express)

## HABARI MICHEZO

# Nigeria: Tumefuata Kombe Afcon U-17

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI timu ya soka ya vijana ya umri chini ya miaka 17 ya Nigeria ikishuka dimbani leo kuwavaa yosso wenzao wa Guinea katika mchezo wa kwanza wa hatua ya nusu fainali ya michuano ya Afrika ( Afcon U-17), utakaochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, kocha wa kikosi hicho, Manu Garba, amesema alichofuata ni kombe na si kitu kingine.

Nigeria ilitinga hatua hiyo baada ya kuongoza Kundi A ikimaliza na pointi saba na kufuatiwa na Angola iliyojikusanyia pointi sita wakati Kundi B timu zilizosonga mbele ni Cameroon na Guinea.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Garba alisema wamejiandaa kucheza soka la kiwango cha juu ili kutwaa ubingwa wa michuano hiyo.

Alisema wamejipanga pia kukutana na ushindani kutoka kwa Guinea ambayo ilionyesha kiwango kizuri katika mechi zake za Kundi B.

"Tulikuja hapa kwa lengo la kuchukua kombe, tulijua tukishinda ndio tayari tutakwenda Kombe la Dunia, kwa hiyo bado hatujamaliza kazi iliyotuleta Tanzania katika michuano hii, lakini tumepata faida sana kupitia michuano hii, wachezaji wangu wamezidi kujifunza," alisema kocha huyo.

Mechi nyingine ya nusu fainali ya michuano hiyo ambayo pia itachezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini itakuwa ni kati ya Cameroon dhidi ya Angola.

Michuano hiyo itaendelea tena Jumamosi kwa kusaka mshindi wa tatu wakati pazia la mashindano hayo yanayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (Caf) litafungwa Jumapili.

### MSIMAMO LIGI KUU BARA



| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Yangas | 32 | 23 | 5 | 4 | 51 | 23 | 74 |
| 2. Azam | 32 | 19 | 9 | 4 | 49 | 19 | 66 |
| 3. Simba | 25 | 20 | 3 | 2 | 53 | 10 | 63 |
| 4. Mtibwa Sugar | 32 | 14 | 6 | 12 | 33 | 24 | 48 |
| 5. Lipuli | 33 | 12 | 12 | 9 | 30 | 28 | 48 |
| 6. Ndanda | 32 | 11 | 10 | 11 | 22 | 30 | 43 |
| 7. Kinondoni MC | 31 | 9 | 15 | 7 | 32 | 22 | 42 |
| 8. TZ Prisons | 32 | 10 | 12 | 10 | 26 | 25 | 42 |
| 9. Coastal Union | 33 | 9 | 14 | 10 | 29 | 33 | 41 |
| 10. Singida United | 33 | 10 | 10 | 13 | 24 | 32 | 40 |
| 11. Kagera Sugar | 32 | 9 | 12 | 11 | 28 | 33 | 39 |
| 12. JKT Tanzania | 32 | 9 | 12 | 11 | 19 | 26 | 39 |
| 13. Stand Utd | 33 | 11 | 6 | 16 | 30 | 41 | 39 |
| 14. Mbeya City | 31 | 10 | 7 | 14 | 30 | 34 | 37 |
| 15. Mwadui | 33 | 10 | 7 | 16 | 37 | 43 | 37 |
| 16. Mbao | 33 | 9 | 10 | 14 | 19 | 33 | 37 |
| 17. Alliance | 33 | 9 | 10 | 14 | 23 | 35 | 37 |
| 18. Ruvu Shooting | 33 | 8 | 12 | 13 | 28 | 39 | 36 |
| 19. Biashara Utd | 31 | 8 | 10 | 13 | 22 | 29 | 34 |
| 20. African Lyon | 33 | 4 | 10 | 19 | 19 | 43 | 22 |

# MGOSI AKERWA KUICHAPA YANGA PRINCESS DHAIFU

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI timu yake ikiibuka na ushindi wa pili mfululizo, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Mussa Hassan "Mgosi", amewataka viongozi wa Yanga kuimarisha timu yao ya Yanga Princess ili kuleta ushindani kwenye Ligi Kuu ya Soka ya Wanawake Tanzania.

**Simba Queens juzi iliichapa Yanga Princess 5-1 wakati mchezo wa mzunguko wa kwanza Wekundu wa Msimbazi hao walipata ushindi mnono wa mabao 7-0.**

Akizungumza baada ya mchezo huo wa watani wa jadi kumalizika, Mgosi alisema anahitaji kuona Yanga Princess inakuwa imara ili kuongeza ushindani na vile vile kusaidia maendeleo ya soka la wanawake.

Mgosi alisema endapo watani wao watashindwa kukijenga na kukiimarisha kikosi chao, ushindani na utani wa jadi hautakuwa na maana kwa upande wa soka la wanawake.

"Nataka kuona kama timu yangu inashinda, basi inashinda kweli kweli, kwa kucheza na timu inayoonyesha ushindani, napenda kuona tunacheza 'dabi' ya ukweli, nawashauri wajipange na msimu ujao waje wakiwa wameimarika," Mgosi alisema.

Kocha huyo aliongeza kuwa kikosi chake kimejipanga kufanya vema katika mechi zote za mzunguko wa pili wa ligi hiyo na anawapongeza wachezaji wake kwa kushinda mchezo wa pili mfululizo.

Matokeo mengine ya ligi hiyo yalikuwa ni JKT Queens ilipata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Alliance Girls wakati Mlandizi Queens yenyewe iliwachapa Baobab Queens ya Dodoma 2-0 huku Evergreen ikitoka suluhu na Mapinduzi Queens ya Njombe.

Kigoma Sisterz iliyokuwa ugenini kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza ilitola sare ya bao 1-1 na wenyeji Marsh Queens.

Ligi hiyo inayoshirikisha timu 12 inatarajiwa kuendelea tena keshokutwa na mabingwa watetezi JKT Queens wenye pointi 45 ndio vinara katika msimamo wakifuatiwa na Mlandizi Queens yenye pointi 35 wakati nafasi ya tatu inashikwa na Simba Queens yenye pointi 34 na anayoburuza mkia ni Mapinduzi Queens ambao wana pointi sita.



Gonzalo Higuain akiifungia Chelsea bao la pili kabla ya Burnley kuchomoa na kufanya matokeo kuwa 2-2, kwenye mechi hiyo ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Stamford Bridge juzi. **PICHA: MTANDAO**

# *Maxime afunguka anapoishika Simba*

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kufanikiwa kuibuka na ushindi katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara wiki iliyopita dhidi ya Simba, Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, amesema kuwa timu yake itaendelea kuwafunga mabingwa hao watetezi, kwa sababu inafahamu vema kuidhibiti "nguvu" yao ilipo na kwamba hata watakaporudiana Mei 5, mwaka huu wanaweza kufanya vizuri.

Kagera Sugar ilifunga Simba mabao 2-1 na kufikisha pointi 39 na kupaa kutoka nafasi ya 17 hadi nafasi ya 11 kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha klabu 20 kutoka mikoa mbalimbali.

Akizungumza na gazeti hili, Maxime, alisema kuwa ligi hii ni ngumu na unapofanikiwa kumwahi mpinzani wako kwa kumfunga, inatakiwa ucheze kwa "mahesabu makali" ili usiharibu.

Maxime alisema ushindi walioupata utawaongezea hamasa ya kufanya vema katika michezo inayofuata ya ligi hiyo na hatimaye kukaa kwenye nafasi salama katika msimamo wa ligi.

"Haikuwa mechi nyepesi, Simba wako katika vita ya ubingwa na sisi hatukuwa kwenye nafasi nzuri, kwa kifupi wote tulikuwa katika majaribu, tunashukuru Mungu tumeshinda na kuendeleza rekodi nzuri," alisema Maxime.

Kocha huyo aliongeza kuwa bado wataendelea kupambana na anaamini wana nafasi ya kupata ushindi katika mchezo wa marudiano utakaochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam Mei 5, mwaka huu.

Naye nahodha wa timu hiyo, Paul Ngalyoma, alisema kujipanga kwao vema na kudhamiria kupata ushindi ndio siri kubwa ya kuondoka na pointi tatu katika mchezo huo uliochezwa kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba.

"Tumefungwa mechi tatu mfululizo zilizopita, tukasema tujipange imara, twendeni tukapambane ili kusaka ushindi, tumejitahidi na tunamshukuru Mungu tumepata ushindi," alisema nahodha huyo.

Hata hivyo, Ngalyoma alisema mechi nyingine ambazo wamekuwa wakipoteza, zinatokana na changamoto ya kutorushwa hewani mubashara.

Michezo
Jumatano Aprili 24, 2019
Nipashe



Milner: Leo nitaishangilia Utd mara ya kwanza UKURASA 30



JUU KWA JUU...

Beki wa Chelsea, David Luiz, akiucheza mpira kwa kichwa baada ya kuruka juu mgongoni kwa mchezaji wa Burnley, wakati wa mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Stamford Bridge juzi na kumalizika kwa sare ya mabao 2-2. **PICHA: MTANDAO**

# Simba wakifakamia kiporo cha Alliance

## ●●● Niyonzima, Okwi watia ndimu, sasa waji-andaa kula cha KMC kesho kabla ya kuifuata...

**Na Somoe Ng'itu,** MWANZA

BAADA ya kiporo cha Kagera Sugar kuchacha kwa Simba kukubali kipigo cha mabao 2-1 wiki iliyopita, hatimaye 'ndimu' zilizotiwa kwenye kiporo cha Alliance FC na Haruna Niyonzima na Emmanuel Okwi, ziliwawezesha mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Bara kukifakamia mbele ya mashabiki wao katika Uwanja wa CCM Kirumba jana.

**Lilikuwa ni bao lililofungwa na Niyonzima kipindi cha kwanza kabla ya kipindi cha pili mtokea benchi, Okwi kutupia la pili na kuipa Simba ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Alliance FC katika mechi hiyo ya Ligi Kuu iliyopigwa jana.**

Simba ambao wamecheza mechi 25 sasa imefikisha pointi 63, ikiwa imezidiwa pointi 11 na watani zao, Yanga ambao wanaongoza katika msimamo wa ligi hiyo ambayo msimu huu inachezwa bila ya kuwapo kwa mdhamini mkuu.

Alliance FC ambao jana walicheza mechi yao ya 33 na wanaoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya kwanza, matokeo hayo yanawafanya kuendelea kubaki na pointi zao 37, lakini wakishuka kwa nafasi moja hadi ya 17.

Bao la kwanza la mabingwa hao watetezi lilifungwa na Niyonzima katika dakika ya 20 baada ya kumalizia krosi ndefu iliyopigwa na Muzamiru Yassin huku beki wa Alliance FC, James Joseph akiacha mpira utoke nje na badala yake ukamkuta kiungo huyo Mnyarwanda aliyepiga shuti lililotinga wavuni moja kwa moja.

Likiwa ni bao la kwanza la Niyonzima kwa msimu huu wa 2018/2019 ambao unaelekea ukingoni, ambalo liliwafanya Simba waende mapumziko wakiwa mbele kwa bao 1-0.

Dakika ya 75, Okwi aliyeingia kuchukua nafasi ya Adam Salamba, aliifungia Simba bao la pili baada ya kupokea mpira kutoka kwa Nicholas Gyan na kuwachambua mabeki wa Allaince na kupiga shuti lililoingia wavuni moja kwa moja.

Mechi hiyo ambayo ilikuwa na faulo za mara kwa mara, ilianza kwa kasi na kupitia Hassan Dilunga, Simba ilifanya shambulizi la kushtukiza, lakini mpira ulikuwa mwingi na kupaa langoni katika dakika ya kwanza na ikafanya tena shambulizi lingine dakika ya sita kupitia kwa Salamba, likaokolewa na beki wa Alliance FC, Joseph James.

Alliance FC walikaribia kupata bao la kusawazisha kwa kupiga vema 'frikiki' kupitia kwa nahodha wake, Siraju Juma, lakini iliishia kutua mikononi mwa kipa wa Simba, Aishi Manula huku mlinda mlango huyo wa Taifa Stars akidaka tena shuti la Hussein Javu alilopiga akiwa ndani ya boksi na kuwanyima wenyeji hao nafasi ya kupata bao.

Kipindi cha pili kilianza pia kwa kasi, kwa kila upande na Simba ndio walikuwa wa kwanza kufanya shambulizi, lakini kipa wa Alliance FC, John Mwenda, alidaka mpira uliopigwa na Salamba aliyeunganisha pasi fupi ya Said Ndemla katika dakika ya 48.

# Yondani, Moris nje Yanga vs Azam FC

**Na Mwandishi Wetu**

BEKI wa kati wa Yanga, Kelvin Yondani, amefungiwa kucheza mechi tatu kutokana na kumpiga kiwiko mchezaji wa Kagera Sugar wakati timu hizo mbili zilipokutana kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba na vinara hao kupata ushindi wa mabao 3-2.

Kutokana na adhabu hizo, sasa rasmi Yondani ataukosa mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Azam FC utakaochezwa Jumatatu pamoja na mechi ya hatua ya nusu fainali ya Kombe la FA dhidi ya Lipuli, sawa na Aggrey Moris wa Azam FC ambaye naye amefungiwa mechi tatu kutokana na utovu wa nidhamu.

Moris amefungiwa mechi tatu na kutozwa faini ya Sh. 500,000 kutokana na kitendo chake cha kumpiga mchezaji wa Mbao FC wakati klabu hizo zilipocheza hivi karibuni na Paul Peter wa Azam naye amepata adhabu kama hizo baada ya kumpiga ngumi mchezaji wa Mbeya City.

Aidha, wakati Yondani akikutana na kifungo hicho, timu yake, Yanga ya jijini Dar es Salaam imepigwa faini ya Sh. milioni tatu kutokana na kutumia mlango usiokuwa rasmi kuingia kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona ulioko mkoani Mtwara wakati wakishuka dimbani kuivaa Ndanda FC Aprili 4, mwaka huu.

Mbali na adhabu hiyo, Yanga pia itatakiwa kulipa kiasi cha Sh. 500,000 kutokana na mashabiki wake kuwapiga kwa chupa waamuzi wa mechi hiyo iliyomalizika kwa kugawana pointi.

Taarifa iliyotolewa jana na Bodi ya Ligi ilieleza kuwa pia Ndanda FC nayo imetozwa faini ya Sh. milioni 1.5 kwa kosa la kutumia mlango usiokuwa rasmi wakati walipoikaribisha Yanga katika mchezo wa ligi.

"Ndanda wametozwa kiasi hicho cha faini kwa sababu ndio mara yao ya kwanza wanatenda kosa hilo," ilisema sehemu ya taarifa hiyo ya Bodi ya Ligi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002

Nipashe
Jumatano Aprili 24, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0579900
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



## Madaktari Muhimbili wabaini ugonjwa unaomtesa Mariam

UKURASA 3


MAKALA:
Sudan 'itakavyoishi' bila Al Bashir
Ukurasa 14
JENERALI YAKUBU GOWON
Ukurasa 18
MAKALA:
siasa
JUMATANO APRILI 24, 2019
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU
Kura yapigwa kumruhusuel Sissi kutawala hadi 2030
Ukurasa 17
FUNZO KWA AFRIKA, DUNIA
Ni pale mchekeshaji anapomshinda rais uchaguzini
Na Anil Kija
UPO msemo kuwa 'hayawi hayawi, huwa', na sasa imetokea barani Ulaya ambako nchini Ukraine mchekeshaji wa luninga, aliyezoea kufamya mizaha kuhusu rais au akijifanya rais katika burudani, ameitwaa nafasi hiyo katika uhalisia baada ya kumshinda rais aliyeko madarakani.
Volodymyr Zelenskiy alikuwa akitabasamu na kutoa ishara za V (alama ya ushindi) ambayo imeacha dunia mdomo wazi, kushinda duru ya pili ya kura ya urais nchini humo.
Mchekeshaji huyo amekuwa akikosoa rushwa kwa nguvu katika nafasi hiyo ya 'urais' kwenye luninga, kumbe ikageuka kuwa maandalizi ya kuwaambia watu kuwa ana uwezo halisi kupambana na rushwa.
INAENDELEA UK.16
Wabunge Democratic wagwaya kuwasha moto dhidi ya Trump
Ukurasa 19
Kiongozi wa chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe. PICHA: MTANDAO
Amerika ya Kusini kupeleka marais wastaafu rumande Ukurasa 20

UKURASA 13

# Ripoti IMF yazua jambo bungeni

• **Prof.** Lipumba atoa ushauri kwa serikali...*Uk.2*





Mamia ya wakazi wa maeneo ya Moshono, Sekei na Moivaro, jijini Arusha, wakiangalia tukio la uokoaji wa watu watano waliofukiwa katika machimbo ya moramu, ambapo watu watatu walipoteza maisha na wengine wawili kujeruhiwa. **PICHA: ALLAN ISACK**

## Kibano kipya wakopaji elimu ya juu wabanwa

UKURASA 4

## Mgodi waua watu watatu

UKURASA 2

MASUMIN
PRINTWAYS & STATIONERS LTD
WYSEN
FiveStar
mondi business paper
CASIO
hp
Canon
nashuatec
DELL
EPSON
APC
Microsoft
KYOCERA
Datacard
CITIZEN
kangaro
NATARAJ
DYMO
Pritt
logitech
ZEBRA
Fellowes
UNOMAT
SanDisk
uni-ball
FALCON SAFE
The World's Trusted Safe
215189702
Masumin Tower, Jamhuri / Mrima Street, P.O. Box 20073, Dar es Salaam, Tanzania
Mob: +255 (0) 626 333 000 / (0) 622 325 488 / (0) 713 325 488
Tel: +255 (22) 2117090, Email: info@masumin.co.tz
BEST OF TANZANIA
TOLL FREE: 0800-11-00-24
www.masumin.co.tz
Masumin printways